ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 20 Julai, 2012

((Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadiro ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2012/2013

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaanza kazi yetu ya kujadili, naomba nitoe taarifa kwamba hadi hivi sasa ratiba tupo siku mbili nyuma. Sasa hivi hapa juu ya meza nina wachangiaji 15 na siku ni siku ndogo. Kwa hivyo ningeliomba kila anayepata nafasi aende kwenye *points* moja kwa moja na tutumie dakika 20, anayeweza kuzimaliza sawa na asiyeweza kuzimaliza wenzake watatumia dakika hizi.

Mhe. Nassor Salim Ali (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii na mimi kutoa mkono wa pole kwa msiba ambao umetukuta, na msiba huu ambao ni wa kwetu sote ni wajibu wetu kuwaombea dua wale ambao wameshatangulia mbele ya haki na kuwaombea uzima wa haraka wale ambao waliopata majeruhi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii naomba kuwasilisha muhutasari wa kamati hiyo kuhusu bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo na Amali kwa mwaka wa 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima wa afya na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya yetu ya kila siku ambayo yanawezesha kuendeleza kujenga taifa letu.

Aidha, ninachukua fursa hii kukushukuru kwa niaba ya kamati kutupa fursa ya kuweza kuwasilisha maoni yetu juu ya makadirio ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Pia ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa kamati yetu kwa kuweza

kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuweza kuishauri serikali inavyostahiki.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda kuwatambua na kuwataja Wajumbe wa kamati yetu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdu Haji - Mjumbe
4. Mhe. Ashura Sharif Ali - Mjumbe
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
6. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
7. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe
8. Mhe. Saleh Nassor Juma - Mjumbe
9. Ndg. Asha Said Khatib - Katibu
10. Ndg. Talib Enzi Talib - Katibu

Mtazamo wa jumla wa Mwelekeo wa Bajeti ya 2012/2013:

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu kwa kweli imeona kwamba kwa muda mrefu bajeti za serikali katika sekta za elimu zimekuwa hazingatii ipasavyo faida ya moja kwa moja inayohitajika kumfikia mwanafunzi wa Zanzibar katika sekta hiyo.

Ingawa baadhi ya mafanikio ya utekelezaji wa bajeti hiyo huonekana kiujumla jumla hasa katika maeneo ya miradi ya maendeleo. Kwa mfano mchango mkubwa wa washirika wa maendeleo katika miradi ya ujenzi wa maskuli.

Mhe. Naibu Spika, katika hatua ya Kamati, Kamati yetu ilijadili na hatimae kupitisha Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tarehe 3/06/2013 kwa mustakbali ule ule wa kufuata utaratibu wa Baraza lako tukufu na maelekezo ya Kanuni za Baraza ambazo zinaelekeza miongoni mwa majukumu ya Kamati yetu ni kupitia na kuijadili Bajeti za Serikali na kushauri. Hivyo tumelitekeleza jukumu hilo, lakini katika hali isiyoturidhisha, kwa msingi ule ule wa kutokuwepo kwa mazingatio ya faida ya moja kwa moja inayohitajika kumfika mwanafunzi wa Zanzibar katika sekta ya elimu.

Mhe. Naibu Spika, ubora wa Taifa lolote duniani, unajengeka kwa elimu wanayoipata wananchi wake. Hivyo na sisi hatuna budi pamoja na umasikini wetu kuwekeza ipasavyo katika Elimu, kwani ndio njia pekee itakayotuwezesha kufika kule ambako tuna ndoto ya kufikia.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti mpya ya Wizara ya mwaka huu , matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka bajeti ya shilingi bilioni 45, milioni mia tatu na nane kwa mwaka wa fedha 2011/2012 hadi kufikia bajeti ya shilingi bilioni 71 na milioni 50 kwa mwaka mpya wa fedha 2012/2013. Mhe. Naibu Spika, hili ni ongezeko la shilingi bilioni 25 nukta 7 sawa na zaidi ya asilimia 56. Fungu hilo la matumizi ya kawaida ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengine ya kawaida yasiyokuwa mishahara.

Fungu la bajeti kwa matumizi yasiyokuwa mshahara ni shilingi bilioni 20 nukta 7. Katika fungu hilo la shilingi bilioni 25, kiwango cha fedha ambacho kinamrudia mwanafunzi moja kwa moja ni shilingi bilioni moja nukta 4 ambazo zitanunuliwa madawati na vifaa vya kufundishia na zinazobaki zaidi ya shilingi bilioni 19 zimeelekezwa katika kazi za kawaida za uendeshaji.

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio hali halisi ya bajeti ya uendeshaji ambayo karibu ya thuluthi ya matumizi zitatumika kukidhi maslahi ya utawala wa elimu na uendeshaji.

HALI YA MAPATO

Mhe.Naibu Spika, kamati yetu inaipongeza Wizara kwa kuwepo ongezeko la mapato katika makisio ya bajeti kwa mwaka mpya wa fedha, kutoka shilingi milioni 15 hadi kufikia shilingi milioni 22. Hatua hiyo imetokana na Wizara kubuni mbinu mpya za vyanzo vya mapato. Hata hivyo nguvu zaidi zinahitajika ili wizara iweze kufikia zaidi ya kiwango cha asilimia 57 cha mwaka uliopita.

Aidha Kamati yetu inaishauri wizara kuhakikisha kuwa inakamilisha mahitaji yake ya ajira, hasa za walimu wa sayansi kwa nafasi ilizonazo, kwa lengo la kuongeza vyanzo vya mapato kupitia vyanzo vya leseni za walimu pamoja na kuwa na walimu watakaosaidia katika masomo ya sayansi.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inaikumbusha wizara kuwa, bado kuna malalamiko kutoka kwa wadau wa sekta ya elimu, juu ya kuwepo kwa vyanzo zaidi vya mapato, ambavyo wizara haijawa tayari kuvisaidia katika bajeti kuu ya Serikali kama ni mapato ya umma. Mapato hayo ni pamoja na malipo ya walimu wanaosoma katika vyuo vya ualimu, michango ya wajibu ya walimu wote wa Zanzibar na michango ya wazazi maskulini.

Pamoja na kuwa kuna sababu za kuonesha kuwa fedha hizi hazifiki kwenye Wizara moja kwa moja, lakini ukweli ni kuwa fedha zinachangwa na wananchi na zinaingia mikononi mwa wizara.

Mhe. Naibu Spika kamati yetu itahakikisha kuwa, inafanya uchunguzi ili kubaini mwenendo mzima wa mapato hayo na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinaainishwa katika mapato ya Serikali.

CHUO KIKUU CHA TAIFA (SUZA)

Mhe. Naibu Spika**,** katika ripoti ya utekelezaji wa kazi za Kamati yetu katika Mkutano wa Saba wa Baraza hili, nilieleza wazi kuhusu kushindwa kwa chuo chetu kikuu cha taifa kufikia malengo yake kwa zaidi ya asilimia 70. Hilo limetokana na Serikali kushindwa kuzingatia umuhimu wa bajeti itakayotosheleza, au ile ya angalau ya kukiwezesha chuo kumudu gharama ya uendeshaji pamoja na mipango yake iliyojipangia. Na leo hii Mhe. Naibu Spika nathubutu kusema tena kuwa, Kamati yetu tayari imeshapata majibu ya utekelezaji wa malengo ya chuo hicho kwa bajeti ya 2012/2013.

Mhe. Naibu Spika**,** makadirio ya SUZA katika bajeti yake hii mpya yalikuwa ni shilingi bilioni 23, ukitoa shilingi bilioni 7 nukta 8 kwa ajili ya mishahara na kuongeza walimu ili kuondokana na wimbi la kuajiri walimu wa muda wenye gharama kubwa. Lakusikitisha Mhe. Naibu Spika, chuo hichi kimepangiwa ceiling ya Bajeti ya shilingi bilioni 4 nukta mbili kwa ajili ya mishahara na Uendeshaji. Serikali ipo makini katika kutekeleza ipasavyo uendeshaji wa taasisi muhimu kama hii, ambayo ni hazina na tegemeo la wengi hasa hasa kwa Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulipa taarifa Baraza lako tukufu kuwa hali ya Chuo chetu Kikuu cha SUZA sio ya kuridhisha na huko tunakoelekea tusitegemee kuvuna ufanisi kwa bajeti kama hii isiyotekelezeka. Wakati umefika Mhe. Naibu Spika, Serikali ni lazima ijipinde kuhakikisha kuwa inapanga viwango vya “angalau” katika bajeti za taasisi zake muhimu kama Chuo chetu kikuu cha SUZA.

SHERIA YA MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Naibu Spika, utakumbuka kuwa Baraza lako tukufu lilipitisha sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Katika utaratibu wa uendeshaji wa chombo hiki, kuna ruzuku inayotolewa na Serikali na “Kodi ya Ushuru wa kuongeza ujuzi (SDL) ambayo hutozwa waajiri binafsi kwa lengo la kusaidia uendeshaji wa Mamlaka hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa taarifa, Wizara ya Fedha imekuwa ikipatiwa shilingi milioni mia tatu na hamsini kwa mwezi na TRA kupitia makusanyo yatokanayo na mapato hayo.

Mhe. Naibu Spika, ni kipindi cha miaka miwili sasa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, Serikali imeshindwa kuipatia Mamlaka hiyo chanzo hicho cha mapato kama sheria zinavyoelekeza. Hali hiyo inapelekea Mamlaka hiyo kukosa ufanisi na kushindwa kufikia malengo.

Mhe. Naibu Spika, ni muhimu kwa Serikali kuwa ni mfano wa kufuata na kutekeleza sheria zinazoanzishwa na Baraza lako hili tukufu. Kuendelea kusita kuipatia Mamlaka fedha hizo ni tatizo katika utekelezaji wa shughuli za Mamlaka.

Hata hivyo, Kamati yetu inaunga mkono wazo la kurekebisha Sheria ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ili Mamlaka hiyo iweze kupatiwa moja kwa moja asilimia 40 ya Kodi ya Ushuru wa kuongeza ujuzi na asilimia 60 itumike kwa ajili ya Elimu ya Juu. Uamuzi huo ni mzuri kwavile mgao huo unaweza kusaidia katika utekelezaji wa mahitaji ya fedha kwa maeneo hayo.

KUHUSU MISHAHARA YA WAFANYAKAZI KATIKA MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imekuwa ikipata malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Unguja na Pemba dhidi ya Wizara husika, kufuatia kukosa kupatiwa mishahara mipya ambayo imedaiwa kuingizwa kwa kipindi cha miaka miwili sasa. Kamati yetu Mhe. Naibu Spika, tumelifuatilia kwa karibu suala hili na kubaini yafuatayo:-

1. Fedha hizo za mishahara kimsingi zimetumika kinyume na utaratibu.
2. Kamati imepata wasi wasi juu ya udhibiti wa matumizi yanayofanywa katika fungu la mishahara mipya ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.
3. Wafanyakazi wa Mamlaka hawakufaidika na nyongeza ya mishahara mipya

Hivyo Mhe. Naibu Spika, kutokana na hali hiyo Kamati yetu tunamuagiza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa Mamlaka hiyo wanalipwa haki yao mara baada ya bajeti hii kwa mujibu wa utaratibu uliyopo.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mkaguzi mkuu wa Elimu, Baraza la Mitihani na Taasisi ya Elimu ni taasisi muhimu za wizara katika suala zima la usimamizi wa elimu nchini. Kamati yetu inaishauri Wizara kuangalia kuzipa uzito wa kibajeti vyombo hivi ili viweze kusimamia ipasavyo sekta hiyo.

Elimu ya Maandalizi

Mhe. Naibu Spika, elimu ya maandalizi ni sehemu ya elimu ya lazima kwa kila mtoto wa Zanzibar, ni jambo la faraja kuona kuwa idadi ya Skuli za Maandalizi zinaongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo tunaishauri Wizara kuzifanyia ukaguzi Skuli hizo na kuzitolea miongozo ya njia bora za kuwafundisha watoto.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa skuli nyingi za maandalizi zimeonekana kuweka mkazo kwa watoto, kujua kusoma na kuandika. hali ya kuwa kutokana na umri wao, walitakiwa kupangiwa utaratibu wa kuwa na muda wa kucheza zaidi na kufunzwa tabia zetu nzuri zinazoendana na utamaduni wetu wa Zanzibar, ili waweze kukua katika misingi ya maadili mema ya maisha yao.

Mhe. Naibu Spika. tunaiagiza Wizara ya Elimu kuhakikisha kuwa Skuli zote za maandalizi hasa zile za binafsi zinafanyiwa ukaguzi wa kina ili kuweza kufahamu maendeleo ya skuli hizo.

Ofisi ya Ukaguzi wa Elimu

Mhe. Naibu Spika, kamati inapongeza uwamuzi wa Wizara, wa kuifanya Idara ya ukaguzi kuwa ni Ofisi ya ukaguzi ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Ofisi hiyo bado inakabiliwa na Changamoto kubwa kwani idadi ya skuli zilizokaguliwa ni kidogo kulingana na idadi ya skuli zilizopo, hasa hasa skuli za maadalizi na zile za binafsi. Tunaiomba Wizara kuhakikisha kuwa, ukaguzi wa maskuli unakwenda sambamba na idadi ya Skuli zilizopo ili kuweza kusaidia kupima ufanisi wa maendeleo katika sekta ya elimu. Aidha kuna haja kwa wizara, kuharakisha mataarisho ya rasimu ya uanzishwaji Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ili kuipauwezo ofisi hiyo kisheria.

KITENGO CHA URAJISI PEMBA

Mhe Naibu Spika**,** kamati yetu tunaishauri Wizara kukiimarisha kitengo hiki ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo hasa ukizingatia kuwa ni taasisi inayosimamia mapato ya wizara. Aidha ipo haja kwa wizara kuandaa mongozo wa kuweka makisio ya kiwango maalum cha ukusanyaji wa mapato kupitia kitengo hiki.

Baraza la Mitihani

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inaipongeza wizara kuona umuhimu wa kuamua kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013 mitihani yote ya taifa ya kidato cha nne, Sita na Ualimu ambayo inaendeshwa na Baraza la Mitihani

Tanzania, kusimamiwa na Baraza letu la Mitihani Zanzibar badala ya Kamati za mitihani ya Mikoa. Hatua hiyo tunaamini itasaidia kuimarisha usimamizi katika mitihani ambayo imeonekana kushuka sana.

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu
Mhe. Naibu Spika, kamati inaihimiza Bodi ya Mikopo kuhakikisha inasimamia ipasavyo utaratibu wa urejeshwaji wa mikopo ili mikopo hiyo iweze kurejeshwa kwa ufanisi. Kasi ya kurejeshwa kwa deni la mikopo ya wanafunzi la shilingi bilioni 8 ni ndogo na inaathiri upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wengine.

Kamati yangu inaipongeza Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Tanzania kuanzisha ofisi zao hapa Zanzibar. Hatua hiyo itasaidia kuiweka karibu Bodi hiyo kiutendaji na wanafunzi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, tunapongeza juhudi zilizochukuliwa na Serikali kwa kuwashajihisha wanafunzi wa kike kupenda masomo ya Sayansi na Hesabati. Tunaishauri Wizara, kuandaa mazingira mazuri kwa kuwa na vivutio na motisha katika masomo ya sayansi, ili kuweza kusaidia kuwa na mpango wa muda mrefu wa kukabilina na kuondokana na tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi Zanzibar.

Changamoto kwa Serikali katika Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

- **Uhalisilia wa bajeti na fedha zilizopangwa**

Mhe. Naibu Spika, kutokana na fedha zinazopangwa katika taasisi nyingi za wizara, thamani halisi ya fedha haifikiwi na huathiri dhana nzima ya thamani ya fedha.

Tunaiomba Serikali kuhakikisha kuwa, fedha ambazo zitaidhinishwa na Baraza hili kwa ajili ya bajeti ya Wizara katika mwaka huu wa fedha zinapatikana zote kwa asilimia mia moja.

- Ushirikishwaji wa wadau wengine wa Elimu, Kamati inaona kuwa bado ushirikishwaji wa wadau wengine wa elimu hauridhishi. Tunaikumbusha wizara kuzingatia hilo ili kuiwezesha bajeti kuzingatia vipaumbele ambavyo vipo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika**,** aidha bado kuna tatizo la ukosefu wa hati miliki kwa majengo mengi au karibu yote ya skuli za Serikali. Hili Mhe. Naibu Spika tushalisema sana. Skuli nyingi zinamiliki ramani tu za majengo na kwamba zimevamiwa na makaazi na taasisi za watu binafsi.

Mhe. Naibu Spika**,** suala hili linaendelea kuzusha migogoro mingi na kesi nyingi za kuvamiwa maeneo ya skuli, hivyo tunaomba Serikali itoe muongozo kuhusu utaratibu wa upatikanaji wa hati miliki za majengo ya skuli ili kuepusha migogoro zaidi isitokee, ni mategemeo yetu kuwa Serikali itawajibika katika kutoa muongozo huo haraka iwezekanavyo.

Mwisho Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inapendekeza Serikali kuwa na mpango wa muda mrefu katika kufikia kutumia asilimia 20 ya bajeti kwa ajili ya elimu. Ni vyema tukaanza kuchukuwa hatua ya kuipandisha bajeti yetu ya Elimu ili iweze kufikia asilimia ya viwango vya kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa na mimi naomba kuchangia kidogo hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kama Kanuni ya Baraza inavyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, ninachukua fursa hii kusema kwamba tatizo hili la hati miliki kwa skuli mbali mbali za serikali ni tatizo kubwa na ni tatizo ambalo sisi kama kamati huwa tunatembea katika skuli mbali mbali tumeliona kuwa ni tatizo sugu. Ningemuomba Mhe. Waziri kulivalia nguga suala hili kuhakikisha kwamba skuli zetu zinapatiwa hati miliki ili kuondoa yale matatizo ambayo yanakuwa yanavamiwa na taasisi mbali mbali pamoja na wafanyabiashara kujenga maduka na nyumba za makaazi. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, Waswahili wanasema, “Mtu hujipatia kwake nyumbani”. Katika Jimbo langu la Rahaleo kuna skuli takriban nne za serikali. Ikiwemo Skuli ya Mwembeladu – Sekondari, Skuli ya Rahaleo, Skuli ya Mwembeshauri na Skuli ya Makadara.

Mhe. Naibu Spika, katika Skuli ya Mwembeladu, skuli ile ina matatizo ya uvujaji wa mapaa ya majengo yale. Halikadhalika matatizo ya madawati katika skuli zote hizi.

Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba katika skuli zetu hizi, katika ule mgao unaokuja wa madawati basi tuweze kupatiwa madawati ili watoto wetu wasiweze kukaa chini ili waweze kupata elimu iliyo bora, halikadhalika katika yale maeneo yanayovuja basi Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri alifanyie kazi suala hili ili kuondoa tatizo hilo la uvujaji katika jimbo langu la Rahaleo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, na mimi kunikushukuru kupata nafasi hii katika asubuhi ya leo. Lakini kabla sijachangia naomba uniruhusu angalau dakika moja basi nitoe neno dogo tu kutokana na janga la taifa lililotokezea, niwape pole wale ambao wote wameguswa kwa namja moja au nyengine katika janga hili, wale ambao wamefariki Mwenyezi Mungu awalaze pema peponi na wale ambao wamepata manusura basi Mwenyezi Mungu awajaalie afya zao ziimarike haraka sana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoa neno dogo hilo naomba sasa nichukue nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Nimshukuru kwa hotuba yake nzuri ambayo amejipangia kwenye mwelekeo mzuri sana wa kuboresha elimu yetu hapa Zanzibar.

Kama ulivyozungumza Mhe. Naibu Spika, kwamba muda ni mdogo na wachangiaji ni wengi, siku mbili zimetupita na mimi naomba niende katika point moja kwa moja.

Naomba nichangie katika eneo la ukurasa wa 65 kuhusu Bodi ya Mikopo. Mhe. Naibu Spika, nimshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi wake kwa kumchagua Ndugu yetu Iddi Khamis Haji kuwa Mkurugenzi wa Bodi ya Mikopo. Kila mtu anamfahamu kijana huyu, ndugu yetu ni kijana mahiri, tunamjua alikuwa Shirika la Bima, bima kaiboresha vizuri sana, kaiacha na jengo la kisasa, biashara imetanuka mpaka Tanzania Bara na faida imekuwa imepatikana nyingi kwenye Shirika letu la Bima. Sasa imani yangu uteuzi wake huu ulikuwa haujakosewa na mategemeo yangu kwamba Bodi hii itaimarika siku hadi siku.

Pamoja na pongezi hizo kitu kizuri chochote basi kinahitaji mashirikiano na kinahitaji kuwa na nyenzo bora. Mhe. Naibu Spika, vijana wetu hawa wa Bodi ya Mikopo, kitengo hiki kwa kweli kina matatizo makubwa sana. Niiombe serikali basi matatizo yaliyokuwepo wayasaidie ili ndugu zetu hawa waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Moja ya changamoto inayokabiliwa Mhe. Naibu Spika, kwamba sote tunafahamu kuwa lile jengo limeshauzwa na mwenyewe ninasikia analihitaji kutaka kulifanyia ukarabati. Sasa niiombe serikali ichukue jitihada za kutosha, tusije tukasubiri mpaka taasisi ile ikaanza kuzungushiwa mabati wamo ndani ya eneo lile na taasisi ya serikali ambayo ina kazi nzito sana.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kwamba jengo linalotumiwa na Bodi ya Mikopo kwamba limeshauzwa, bado kuna changamoto kubwa ambayo imewakabili ndugu zetu katika jengo lile. Lile jengo ni chakavu. Hicho kipindi ambacho hivi sasa wanafanya kazi Mhe. Naibu Spika, katika mazingira magumu tena sana na hayastahiki kufanya kazi katika eneo lile. Inaponyesha mvua inakuwa aibu tupu katika taasisi ile, humjui mkurugenzi, karani, wala mhasibu, watu wote wanajikusanya katika eneo moja, wanajikunyata na kazi hazifanyiki.

Sasa hili ni tatizo Mhe. Naibu Spika, niombe kwa dhati kabisa, serikali iangalie eneo lile kwa kuweza kulifanyia marekebisho ili watu waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Kwa sababu zote changamoto mbili ni nzito. Moja ni kuwa jengo bovu lakini la pili kuwa jengo si letu. Sasa hii si nzuri kufanya kazi katika jengo la mtu ambaye yanakuwa yale makero mara kwa mara.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuelezea hali halisi ya jengo ambalo wenzetu wanalifanyia kazi, basi nilikuwa ninataka kuzungumzia suala jengine tu ambalo ninashukuru kwamba Bodi hii wameshaliona. Suala la kupeleka wanafunzi nje ya nchi wakati fani ile katika nchi yetu ipo.

Hili naomba nitoe msisitizo zaidi na niombe Bodi bado iendelee kutoa msisitizo kwa zile fani ambazo zinapatikana ndani ya nchi basi si vyema wakaruhusu watu kuwapeleka nje ya nchi.

Ninasema hivi kwa sababu gani Mhe. Naibu Spika. Ninatoa mfano mdogo tu. Mhe. Naibu Spika, kumpeleka mwanafunzi mmoja kwa mfano China anahitaji ada ya Dola elfu sita na posho Dola elfu nne kwa mwaka, almost kwa hesabu za haraka haraka ni karibuni ni Dola elfu kumi, mtu yule anasoma kwa miaka mitano. Kwa miaka mitano inakuwa ni Dola hamsini. Kwa mahesabu ya haraka haraka karibu milioni sabini. Mhe. Naibu Spika, pesa hizo kwa mtu mmoja na kwa heabu ambazo hivi sasa tumezifanyia kazi tuna karibu wanafunzi wa nje mia mbili. Sasa hii ni hatari kubwa sana.

Sasa niombe kwa dhati kabisa na niombe Bodi iendelee kujenga msisitizo pamoja na serikali kwa zile fani ambazo zinazoweza kupatikana katika nchi yetu basi tuutumie uwezo huo kwa kuwasomesha vijana wetu katika vile vyuo vya ndani ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, hili si tatizo kwa upande wa watu wa fedha nyingi zinazotumiwa na wanafunzi hawa wa nje, lakini pia inakuwa ni vigumu kwa wanafunzi hawa baada ya kumaliza masomo yao, wanapoajiriwa katika urejeshaji wa madeni yao. Mhe. Naibu Spika, gharama ya shilingi milioni

sabini kwa mwanafunzi wetu, kwa malipo ya mshahawa wa Zanzibar sijui ataumaliza kwa muda gani.

Sasa na wakati kuna watu ambao bado wanahitaji kupata yale marejesho ili na wao yaweze kuwasaidia. Sasa ninaendelea kutoa msisitizo kwamba kuangalia zaidi vyuo vyetu vya ndani kwa zile fani ambazo tunahisi zinaweza kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho nilikuwa naiomba serikali ikiangalie kitengo chetu cha bodi, kile kitengo kimeanzishwa hivi karibuni, lakini kwa bahati mbaya au bahati nzuri kitengo kile kinakabiliwa na changamoto nyingi.

Changamoto ya kwanza bodi yetu ya mikopo haijawa na wataalamu wa kutosha katika fani mbali mbali za kuweza kusaidia ili ile bodi iweze kuimarika. Ukiachilia ukosefu wa wataalamu wa fani za kutosha katika kuweza kusaidia bodi ile, bodi yetu bado inakabiliwa na vitendea kazi. Kama tunavyofahamu taasisi ni mpya na vitendea kazi vyake bado havijawa vya kutosheleza pamoja na suala zima la usafiri, bado bodi haijawa na gari, wanatumia gari zao binafsi kufanya shughuli zao katika kufuatilia masuala mbali mbali, hususan katika kufuatilia masuala ya madeni, sasa hii inakuwa ni kadhia kwao. Kwa hivyo, niiombe serikali kuweza kukiimarisha kitengo kile ili kiweze kufanyakazi katika hali ya ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kuiomba serikali, kuna haja ya kuiangalia bodi yetu ya mikopo. Vijana wetu wengi wanaohitaji mikopo wengi wao ni maskini. Mtoto wa tajiri Mhe. Spika, hafukuzii kwenda kutafuta mkopo serikalini, anayekwenda kutafuta mkopo serikalini ni mtoto wa mkulima na mkwezi. Mwaka jana tulikuwa na mapungufu makubwa ya watu ambao walikuwa na sifa lakini serikali haikuwa na uwezo, lakini serikali ilijitahidi. Kwa hivyo, niiombe serikali tuendelee kujitahidi zaidi kutafuta *fund* za kuweza kusaidia bodi ya mikopo ili kuweza kuwasaidia vijana wetu.

Pia Mhe. Naibu Spika, niwaombe sana wale ambao mwaka jana walikuwa na sifa ya kupata mkopo, lakini serikali haikuwa na uwezo wa kuwakopesha, basi serikali itowe kipaumbele kwa vijana wale ili baadae tuangalie na wale ambao wameanza kuomba mwaka huu hiyo mikopo ili iweze kuwasaidia.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, nina neno moja tu ambalo nataka kulizungumzia baada ya kutoka katika muhtasari wa kitabu, nilikuwa nataka nipate ufafanuzi wa vifungu tu kidogo. Mhe. Naibu Spika, kuna vifungu vinanipa mashaka. Kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyopiga kelele kuhusu masuala ya viburudishaji bado yanatupa mashaka sana. Katika fungu dogo la 220105. Mwaka jana waliomba milioni

8,350,000, lakini mwaka huu wameomba 41,900,000. Hili ni ongezeko kubwa sana Mhe. Naibu Spika, tunataka maelezo kwa Mhe. Waziri atakapokuja atueleze, lakini na fungu dogo vile vile la 220200, mwaka jana ilikuwa shilingi milioni 2,800,000 na mwaka huu ni milioni 25,110,000, ongezeko ni kubwa na linatupa mashaka Mhe. Naibu Spika.

La mwisho linalonipa mashaka ni fungu 0701. Mhe. Naibu Spika, fungu dogo, safari za ndani na safari za nje, linanipa mashaka kwa sababu linatofauti kubwa sana. Tegemeo letu ni kwamba safari za nje ndio zichukuwe fungu kubwa zaidi kuliko safari za ndani, lakini pamoja na hayo na ndivyo ilivyokuwa mwaka jana. Mwaka jana safari za ndani zilikuwa milioni 14,000,000 na safari za nje ndio zilikuwa milioni 16,000,000. Lakini mwaka huu ongezeko limekuwa kubwa sana na ongezeko kubwa limekwenda kwa safari za ndani. Mwaka huu safari za ndani zimewekewa milioni 80,000,000 badala ya milioni 14,000,000 na safari za nje ni milioni 62, 000, 0000 badala ya milioni 16,000. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja naomba anisaidie ufafanuzi katika fungu hili na maeneo mengine naomba niwaachie wenzangu. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa asubuhi hii kunipatia nafasi ya kuweza kutoa machache juu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo tunaijadili.

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha tukiwa wazima na afya kuweza kuja hapa katika kikao chetu hiki. Pili, nitowe pole kwa Wazanzibari wote tuliokumbwa na msiba mkubwa uliotokea juzi kwa kuwapoteza ndugu, jamaa, wake, watoto na waume. Hii ni kama tumepata jaraha juu ya kovu, kwa sababu ndani ya mwaka mmoja tumekutwa na majanga mawili makubwa. Kwa hivyo, natoa pole kwa Wazanzibari wote na hata waliokuwa sio Wazanzibari ambao msiba huu umewakumba. Niwatakie marehemu wa Kiislamu Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, amin.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze mchango wangu kwa elimu ya juu kwa wanafunzi wanaoingia katika vyuo vyetu vya juu na hasa wale wana wanaochukua masomo ya Art, lakini zaidi wale wanaochukua masomo ya dini na Kiarabu. Mhe. Naibu Spika, jambo ambalo mimi linanisikitisha, kunihuzunisha na kuona kuwa sijui mwelekeo wetu ukoje kwa masomo haya ya dini kuwa leo ndani ya Zanzibar hayana soko. Anayechukua masomo haya kwa hapa Zanzibar ni kama anatafuta elimu tu, lakini asiwe na tamaa yoyote ya kupata ajira ndani ya serikali yake. Kwa sababu hata anapohitaji mkopo, kwa sababu anachukua masomo haya, tayari anaambiwa hawa hawakopeshwi. *Innalillah Wainna Ilahiraajiun.* Wazanzibari tunaidharau dini yetu, tena bila

kificho tunawaambia kuwa hawa mikopo kwao sio haki, hawapati. Hii ni kweli kwa sababu hata kwenye kusomeshwa kwao katika ngazi za sekondari hata vitabu na kiongozi wa mwalimu, masomo haya hayana. Kwa hivyo, kama hayana soko na hayatakiwi basi ni bora kwa serikali sio kwangu mimi wakayaondoa. Kwa sababu wasiwapotezee vijana muda wao na kumbe hawana haja nao.

Mhe. Naibu Spika, ifikirie zaidi hivi ni kweli dini ya Kiarabu hapa Zanzibar haina haja tena, ni kweli mafunzo ya Kiislamu hapa hayatakiwi tena. Mhe. Naibu Spika, hili ni moja.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wanafunzi wetu mara maandalizi yao mara nyingi wanafeli wanapoingia darasa la kumi na mbili, kutokana na maandalizi yetu ya mwanzo. Kwa sababu Zanzibar inamuandaa mtoto kutoka darasa la tisa kwenda darasa la kumi ili aweze kuingia darasa la kumi na moja. Kwa hivyo, hapa huwa tuna *syllabus* yetu ya Kizanzibari.

Anapoingia darasa la tisa anaandaliwa, sio aingie darasa la kumi na mbili na darasa la kumi na tatu, lakini anaandaliwa aingie darasa la kumi na moja. Lakini wenzetu wa upande wa pili, ambao tunafanya mtihani mmoja, mtoto anapoingia darasa la tisa anaandaliwa kufanya mtihani wa darasa la kumi na mbili, sisi tunamuandaa aingie darasala kumi na moja.

Mwisho wa siku Mhe. Naibu Spika, hawa wanakuja kufanya mtihani mmoja wote wa darasa la kumi na mbili. Hapo zamani mtihani wa darasa la kumi na mbili masuala yake yanaanzia darasa la tisa, kumi, kumi na moja na machache ndio yanatoka darasa la kumi na mbili. Lakini anavyoandaliwa mwanafunzi wa Zanzibar leo, anapata maandalizi ya kufanya mtihani wa darasa la kumi na mbili kwa miaka miwili tu, badala ya miaka minne, hapa tunatarajia afanye nini na ndivyo alivyoandaliwa.

Kwa hivyo, mpango wa elimu ya Zanzibar ni wa makusudi kuwadumaza wanafunzi wa Kizanzibari, kwa sababu wana hakika kwamba mtihani wa mwisho wa darasa la kumi na mbili wanafanya pamoja na watu wa Bara, lakini wao wamemuandaa mpaka darasa la kumi na moja tu, huku darasa la kumi na mbili anapokuja maandalizi yake ni ya miaka miwili tu, atapasi vipi. Kwa hivyo, huu ni mpango wa makusudi kuwadumaza watoto wetu iwe hawana elimu inayostahiki baada ya kumaliza masomo yao.

Kwa hivyo, ningewaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali suala hili walione, wasitudumazie watoto wetu, wapate elimu inayostahiki.

Mhe. Naibu Spika, siku hizi tunayo mafunzo ya awali, yaani skuli za maandalizi ambayo yameenea sana sehemu za mjini na ziko chache huko vijijini kwetu. Sasa mtoto anapoingia darasa la kwanza anaanza kufundishwa kwa sentensi, ambapo huko nyuma walikuwa wanaanza kufundishwa kwa a, e, i, o, u kwa *alphabet.* Sasa leo anaanza kwa sentensi, hapa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imechukua kwa jumla, kwa sababu wamefika katika maandalizi ni kuwa haya wameshafundishwa.

Lakini huko vijijini kuna sehemu nyengine hizo skuli za maandalizi haziko, sasa unapomsomesha kwa sentensi moja kwa moja huwa hafahamu kitu. Ndio maana mara nyengine anamaliza skuli mtoto mwaka wa kwanza, wa pili na watatu kuandika jina lake hajui, kwa sababu hakupata maandalizi ya kutosha. Suala hili ndio linawadumaza watoto wetu kupata elimu inayostahiki. Ningewaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, suala hili walione kuwa ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya watoto wetu kufanya mitihani ya darasa la saba na la kumi, hatua inayofuata ni usahihishaji wa mitihani hiyo. Mhe. Naibu Spika, hapa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haiwashirikishi ipasavyo walimu wa Pemba kwenye usahihishaji wa mitihani. Mhe. Naibu Spika, inasemekana, katika mitihani iliyofanyika mwaka jana 2011, darasa la saba walimu walioshiriki katika kusahihisha walikuwa ni 307. Walimu 300 walitoka Unguja na walimu saba waliobakia walitoka Pemba.

Mtihani wa darasa la kumi inasemekana walisahihisha walikuwa ni walimu 460. Walimu 445 wanatoka Unguja na walimu 15 tu wanatoka Pemba. Je, wizara haioni kuwa inawadhulumu hawa walimu wa Pemba katika masuala haya, kwa hoja yoyote atakayojenga, nataka hili walione kuwa hawawafanyii haki walimu wa Pemba. Kwa hoja yoyote waliyokuwanayo kama hawana pesa au hawana pahala pa kuwaweka ni kuwadumaza walimu wa Pemba na wao wanakata tamaa.

Mhe. Naibu Spika, kwenye cabinet ya mitihani hiyo kulikuwa na watu 45 inasemekana. Watu 43 wanatoka Unguja na watu wawili kamili wanatoka Pemba. Maafisa waliokwenda kushiriki katika mtihani huo walikuwa 33. Maafisa 30 wanatoka Unguja na maafisa 3 walitoka Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hii ndio hali halisi ya Wizara ya Elimu na Mafuzo ya Amali juu ya Wapemba, tunakwenda wapi. Hii ndio hali halisi ya wizara juu ya kisiwa cha pili, *what are they doing*?

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inawafanyakazi wake ikiwa wengi ni walimu na wengine wanapewa vyeo na kuwaita walimu

wakuu katika skuli zake za msingi na za *secondary* na wanawapa posho kwa vyeo vyao hivyo. Yule mwalimu mkuu wa *primary* anapewa posho la shilingi 10,000 kwa mwezi na msaidizi wake anapewa shilingi 6,000 hilo ni posho la mwalimu mkuu. *Secondary* anapewa shilingi 13,000 na *primary* anapewa shilingi 8,000. Mhe. Naibu Spika, kwa Pemba posho hili akienda kwenye mikutano miwili, itabidi atumie mshahara wake ambao pia huo mshahara hana, kwa sababu mshahara wote Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora alipofanya marekebisho mwezi uliopita wote aliuchukua, kama kwa makosa au kwa vipi, lakini wote aliuchukua. Kwa hivyo, inabidi atudai mshahara wake ambao pia hanao.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ningeiomba Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali, iangalie kwa makini kuwafanyia walimu *scheme of service* ili walimu wapate haki zao. Mhe. Naibu Spika, tukitizama kuna walimu ambao tayari wamefanyakazi kwa miaka 30, keshokutwa wanastaafu, mwalimu ana mshahara kasoro katika maisha haya ya Kizanzibari ya shilingi 200,000, keshokutwa anapostaafu katika mshahara duni kama huo, mtu aliyefanyakazi kwa miaka 30. Kwa hivyo, ningeomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, iwaangalie kwa jicho la huruma ya juu tena walimu hawa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nizungumzie kidogo katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi Kengeja. Mhe. Naibu Spika, nasema kuwa wanafunzi walioitwa pale ni kama wanaokuja kutupwa, wamekuja kugewa, wamekuja kupotezwa. Kwa sababu kile ni chuo cha ufundi. Lakini kwa taarifa nilizonazo ni kuwa ile skuli ina idara mbili. Idara ya Ufundi na Idara ya Masomo ya kawaida. Kwa hivi sasa hii idara ya ufundi ambayo moja wapo ya masomo yanayoshughulikiwa ni ya umeme, lakini haina mwalimu hata mmoja.

Lakini hivi karibuni waziri katika kujibu maswali mbali mbali, nasikitika alisema wamepeleka mwalimu mmoja wa sayansi katika Skuli ya Ufundi Kengeja, lakini mpaka asubuhi hii mwalimu huyo hajafika, labda anaogelea. Mwalimu huyo aliyekuwa kapelekwa tokea kikao kilichopita, anaogelea bado hajafika Kengeja Ufundi.

Mhe. Naibu Spika, walimu waliajiriwa wengi, nadhani 800 kama alivyotuambia ni jambo la kusikitisha kwamba sidhani hata 200 wanafika waliopelekwa Pemba. Maombi yapo, walimu wapo, lakini ajira hawana tunawasomesha bure Wapemba lakini hatuwaajiri. Ni kuwa tunatumia pesa zetu, jasho la wazee wao ambalo hatimaye ni kama tunaotia maji pakachani.

Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Hewallah ahsante. Hivi ndivyo ilivyo. Nina pongezi ndogo tu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa chuo hiki. Ni kwamba yale madarasa manne waliyoyataja wameyajenga kweli, lakini kile chuo kina wanafunzi kama 160 uwezo wake katika wanafunzi wale ni 56 tu, hawa wengine hawana pahala pa kulala, kwa hivyo wanalala kwenye madarasa. Kwa hivyo, yale madarasa manne waliyojenga na kukusudia kuwa ni ya kusomea, mawili yamekua dakhalia, kwa hivyo wanalala wanafunzi.

Isitoshe Mhe. Naibu Spika, kile chuo kimeungiwa umeme huu wa kisasa mnaoita sijui ndio Luku. Lakini huko nyuma kile chuo kina madeni kadhaa ya umeme, sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kila mwezi inawaingizia shilingi 100,000 kwa ajili ya malipo ya umeme, lakini Shirika la Umeme kwa vile inakidai kile chuo pesa nyingi sana, basi walivyoziingiza zile pesa zote wenyewe wamezichukua. Kwa hivyo, chuo kinakuwa na umeme kama siku nne, tano au kama wiki moja halafu baadae kunakuwa kiza kitupu.

Mhe. Naibu Spika, kile chuo kina wanafunzi wa kike na wa kiume na wote wanalala hapo hapo kwa sababu pakulala hawana, wamekaa kama kuku banda lao lilovunjwa. Kuku banda lao likivunjwa wengine wanalala juu ya paa na wengine wanatafuta sehemu wakalala. Ndivyo walivyokuwa wale wanafunzi wa Skuli ya Ufundi Kengeja hawana pa kulala na ni watoto. Je, litakalotokea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itatuambia nini na wao wanafanya kusudi vile, wajengeeni dakhalia wale watoto ili wapate pahala pa kukaa au msiwapeleke tena.

Wazee mnaowapeleka watoto wenu pale, ni kwamba wale watoto wamefanywa mayatima ambao hawana baba, mama, jirani wala hawana mjomba. Kwa kweli kile chuo ni matatizo matupu, hakuna kilichopo, hizo nyumba zilizojengwa za walimu ni mbovu wala hakuna huduma yoyote ya msingi iliyopatikana. Sijui Skuli ile ya Ufundi haina fungu lilotengewa na kama lipo Mhe. Naibu Spika, nadhani halitumiki kama linavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, ningewaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kuwa ile skuli ni yao kama kilivyo chuo cha Mikunguni, nayo ile kule Pemba Kengeja ni ya wizara hii. Nasema hivyo, sio kwa sababu iko katika jimbo langu tu. Watoto wanaoingia pale asilimia 99 ni kutoka skuli mbali mbali za Pemba, lakini inanipa uchungu kwa sababau iko ndani ya jimbo langu na haina huduma yoyote, ingekuwa inag'oka ningeing'oa nikajakuitua hapa ili Mhe. Waziri aione, lakini haing'oki.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa umeniambia bado dakika tano, basi nimalizie kwa kusema kwamba narudia kuwapa pole Wazanzibari wenzangu tuliofikwa

na maafa, huu ni msiba wetu sote, tuwe na subra na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia, huwenda serikali ikaona umuhimu wa kuwa na meli nzuri na nzima ya serikali, ambayo itatusaidia katika kutusafirisha baina ya hapa na pale, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, ulipoanza kutaja jina langu, nilipoanza kusimama machozi yamenitoka kutokana na vifo vya wenzetu vilivyotokezea, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu awajaalie awape amali njema na wale waliofiwa na jamaa zao wawe na subra. Mhe. Naibu Spika, kwa kutanguliza hayo Mwenyezi Mungu pia awape moyo wa subra viongozi wetu ili twende nao pamoja katika kuomboleza janga hili kubwa lililotokezea.

Mhe. Naibu Spika, tunaijadili hii hotuba ya bajeti, lakini tumo katika huzuni kubwa sana ya kuweza kuijadili hotuba hii. Mhe. Naibu Spika, lengo kuu hasa sisi Waheshimiwa Wawakilishi, hasa *backbenchers* ni kuielekeza serikali majukumu yake na utendaji wake, ndio lengo letu kubwa. Nataka watufahamu wananchi jinsi ambavyo tunawasaidia na kuwatetea haki zao na tunapofika pahala wao wenyewe waone jinsi ambavyo hapa tayari tumeshagonga ukuta waheshimiwa wao ukweli ndio huo, hakuna sasa hivi kufichana.

Mimi nimeapa kwamba nitatetea haki za wafanyakazi kwa kupitia walimu kwenye hotuba hii na huko nyuma tulikuwa tukitetea hivyo hivyo, jinsi gani wananchi wetu wapatiwe vyombo vya kisasa na tumesema mpaka tumechoka, hatimaye yaliyotutokezea ndio hayo ni majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, lakini tutafika pahala ambapo Mwenyezi Mungu alipotujaalia salama tutafika.

Mheshimiwa aliyekaa kitako kasema iko haja Mhe. Naibu Spika, ya kutafuta chombo, kila siku tumeshachoka kuimba nyimbo tu, tumeshachoka watu wanateketea. Tukisema ukweli tunatafsiriwa vibaya, lakini hawajui kama mnawapotosha wananchi, tunatetea haki za wafanyakazi na wananchi za kupatiwa maslahi yao, kupatiwa mtu kitu cha uhakika au chombo cha uhakika. Tulikuwa na MV Maendeleo na tulikuwa na MV Mapinduzi, sasa leo ziko wapi kwa nini tusiseme.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee kujadili hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu, kwanza niingie katika ukurasa wa 17. *Message sent.* Mhe. Naibu Spika, kifungu cha mradi wa uimarishaji wa elimu mbadala amani. Mhe. Naibu Spika, serikali inakuwa na nia nzuri, hata katika programu zake za upangaji, mimi hapo sina tatizo, kwa sababu ndio lengo, unapokuwa unataka jambo lako lolote ni lazima uwe na programu maalum, lakini ufanyaji wake wa kazi unakuwa ni hafifu kabisa. Tunakuwa na malengo mazuri lakini hatimaye tunakuwa hatutekelezi yale malengo tuliyokuwa nayo.

Mhe. Naibu Spika, tuna vyuo hivyo vizuri sana, lakini la kusikitisha sasa hivi wamestopishwa kupewa fedha za kujiendeleza, vijana wanatoka pale hawana lolote, imekuwa ni bure tu, hiyo inakuwa ni wimbi la kwanza au tunatoa mikopo halafu hatufuatiliii ile mikopo kwa kuweza kuwatafuta wengine ambao wamekwisha kuomba. Mhe. Naibu Spika, hili nalo ni janga, hatuwakidhi haja hawa, inasikitisha kusema ukweli. Kwa sababu tunapowakusanya vijana wetu tunawapa taaluma basi tuwaendeleze nao, wakitoka kule tuwape zile *tools* za kufanyiakazi na hatimaye tunawaachia na kuingia katika mambo ambayo hayastahiki na baadae wazazi tunabakia kugombana na watoto wetu bure.

Mhe. Naibu Spika, katika fungu lake kuu nitakuja kuzuia fungu hilo, kama si hivyo Mhe. Waziri aje anieleze vizuri sana alipofikia tena asilimia kubwa ndipo nitakapomuachia fungu lake, kwa sababu kwenye buku kubwa kuna kasoro nyingi na tutakuja kuweka sawa huko. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niingie kwenye Idara ya Utumishi na kitabu kimejieleza uzuri hapa kwenye sentensi yake. Lakini hivi karibuni Mhe. Naibu Spika, tumeajiri walimu wengi tena wa fani mbali mbali na zile kada ambazo tulikuwa tunazitaka tayari tumewaajiri.

Mimi nilisema kwenye Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora ah! Kwamba kuna watu wameajiriwa na mishahara yao wakapewa nusu na wala Wizara ya Nchi (OR), Utumishi hawakunipa jibu nilishangaa, kwa sababu nilitegemea Wizara ya Utumishi watafuatilia ni sababu gani, isipokuwa kubwa kazi yangu naambiwa niwapeleke tu, kwani kuwapeleka watu sio *solution* na *solution* ni kuwatekelezea watu lile lao ambalo wanalitaka.

Kwa kweli watu wamepewa mishahara midogo na hilo sio lengo. Kwa hivyo, sasa naomba Wizara husika na nipewe sababu maalum tena nione *voucher* gani iliyotumiwa ya kuweza kuwalipa wale walimu walioajiriwa wapya na nataka nilitewe hapa. Mhe. Naibu Spika, siku ile nilisema na Wizara ya Nchi (OR), Utumishi hawakufuatilia na wala hawakutafuta na sasa nataka nione hapa.

Mhe. Naibu Spika, watu wameajiriwa tarehe 02/04 na mafao yao wamepewa kidogo sana. Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Waziri aangalie kuanzia tarehe hiyo na wamekuja kupewa mwezi wa juzi tu mshahara huo na sijui sababu gani zinazoelekeza hata tuwape mishahara hiyo.

Mhe. Naibu Spika, tunaomba sana jambo hili na tuko *serious* na ninaomba *voucher* iliyotumika kama ndiyo ya Wizara ya Fedha yenyewe au ya kupoteza wakati mambo ya siku hizi ya madudu maneno ya Babu yangu mmoja Juma, basi naomba ije. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika utumishi wao kuna utaratibu ambao hawa walimu kuwapa fedha za likizo kila baada ya miaka mitatu. Kwa kweli waajiriwa wengi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanalia na sijui kwa nini suala hili limekuwa sugu katika Mawizara mengi sana, lakini leo naizungumzia Wizara hii, kwamba hawalipwi ipasavyo na kama watalipwa basi watalipwa kirafiki.

Kwa mfano, mimi nitakuwa rafiki yangu mhusika ambaye ni mhasibu na mambo mengine kama hayo, lakini kama si rafiki yangu basi huna kitu unachokipata, wakati sisi kwenye bajeti tunaweka fungu *special* kwa ajili ya likizo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri afanye utafiti, kwa kuwa wewe ni mpya na wala sidhani kama aliyeondoka amekuachia manyago hayo, basi mimi naamini kwamba suala hili utalifuatilia na utatekeleza kwa wale na hata kwa wale wa nyuma kama kuna utaratibu wa sheria, basi hata zile *arrears* zao iwajibike na waweze kupewa wale watu ambao hawajaenda likizo wapewe haki yao, kama sheria inasema hivyo wale wenye malimbikizo ya likizo sasa haki zao na wao wapewe Mhe. Naibu Spika.

Kwa kweli tunaomba sana Mhe. Waziri, kwa sababu walimu ni watu ambao ni hatari sana, kwa sababu wanatukimbia tena suala hili tunasema sana. kwa mfano, sisi tukionekana na mtu akitoka nje anakwenda kusema aaa! Yule siye, siye nani? Na mimi ndiye Mshimba, unasema siye vipi? kwa sababu ninachokisema ni kitu cha ukweli walimu wanatukimbia maslahi yao yanakuwa pungufu. Sasa sisi kazi yetu nini hapa kama si kuwatetea wao kwa mujibu wa utaratibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi pamoja na Katiba ya Zanzibar zinavyoeleza, kazi yangu ndio hii mimi sasa.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba ajitahidi sana kwa walimu kuhusu maposho yao, kama vile *transport allowance* pamoja na mambo mengine, yaani kila kitu chao tunaomba sana wakamilishiwe na wala tusiwadharau hawa.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuna jambo ambalo nimefarajika au ninasikitika sana kuhusu Idara ya Mafunzo ya Ualimu, suala hili liko kwenye ukurasa wa 47 kifungu cha 66. Mhe. Naibu Spika, tunajitahidi sana kusomesha na tunatoa fedha nyingi sana za wavuja jasho, lakini hawa wenye vyeti huko nje

tunawafanya nini? Hebu tujiulize na kwa nini tukawapa elimu kama hatutaki kuwaajiri, sasa na wao tuwafikirie Mhe. Naibu Spika. Ah! Haya mambo ya kada yamekuja juzi baada ya masuala ya utumishi na kutaka kujiweka vizuri, ni sawa lakini na hawa tuwaangalie wanavyeti hawa.

Kwa hivyo, kama wanavyeti basi mimi naomba na hawa waajiriwe na halafu wapewe *training* ndani ya ile kazi yake kama mnavyoeleza, mimi nakubaliana nayo hiyo na wala tusiwaweke magogoni leo na elimu yao wanahangaika.

Mhe. Naibu Spika, kama Mhe. Waziri atalifanya hili basi nakubaliana naye, kwa sababu wako wengi huko ambao wenye vyeti na hawana kazi na wanakuja kwetu sisi tuwasaidie, sisi tunawambia kwamba tunasema na tutaendelea kusema na wala hatutochoka. Kwa kweli hatutoweza kuzuia fungu kwa sababu tukizuia itakuwa tutazuia ule utendaji, lakini fungu lile tutalikasimu kwa sababu hatuwezi kuweka fungu kubwa kwa madhumuni ya jambo fulani na hatimaye ikawa lile jambo lisikamilike. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, suala hili alikalie kidete sana kwani hawa nao wanayo haki na wametumia jasho lao katika walipakodi, basi na wao wapewe kazi, ili waweze kujisikia kwamba wameweza kusomeshwa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema leo sitokuwa na hoja nyingi nilitaka nimalizie hapo.

Vile vile hivi karibuni tulipiga sana kelele kuhusu suala la mambo ya Elimu ya Juu huko na kuweza kupewa mikopo wanafunzi wetu kwa wakati. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri anieleze kuwa zile fedha ambazo zilizokuwa tupewe na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na zilikuwa zinatajwa sana hapa.

Kwanza aniambie ni sababu zipi zilizofanya hasa tusiweze kupewa? Pili tulipotamkiwa kupewa kulikuwa na *agreement* fulani, yaani tulikuwa na mkataba au tuliambiwa kwa mdomo na kama tuliambiwa kwa mdomo, basi tumepigwa changa la macho, tumedanganywa na tumekubali kudanganyika, lakini kama kutakuwa na mkataba fulani ulikuwepo, sasa nani aliyezubaa kwenda kuchukua zile fedha, kwa sababu kaka yangu hapa Mhe. Omar Yussuf Mzee alieleza vizuri sana, kwa mantiki ya lugha yake iliyokuwa ni nzuri.

Lakini nilikuwa na huzuni kubwa sana, kwa sababu yeye ameeleza kwa huzuni kuweza kuzikosa fedha zile na kuingia kwenye bajeti yake na

alisikitika sana, sasa kama yeye Mhe. Waziri amesikitika sisi *backbenchers* tufanye nini? Tulie machozi.

Suala hili siku zote tunalisema jamani, mnapokwenda kwenye vikao vyenu msitegemee hizi mambo ya *minutes* za kikao, kwa sababu *minutes* za vikao zinaweza kufanyiwa *vice versa* na zikafutwa na ikawa mchezo umekwisha. Mhe. Naibu Spika, mara nyingi sana sisi tunapokwenda kwenye vikao vile basi tumeshaamua jambo hili Wazanzibari Mawaziri wanafunga *briefcase* zao na kurudi mbio na masuala yamekwisha wanasubiri waje huku na kufanya utekelezaji hapana.

Kutokana na hali hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba sikubali jambo hilo, isipokuwa mnakubaliana basi kaa pale na kama matanga unakaa pale, yaani kama unavyokwenda kulala matanga mitaani, basi na pale unakaa na kusubiri mpaka kile ulichokikusudia unarudi nacho na hivyo ndio *system* ambayo tunaitaka.

Kwa hivyo, ndio maana tukasema kwamba tubadilishe mfumo, kwa ajili ya kuwaokoa Wazanzibari, ili tupate elimu kwa sababu Wazanzibari kielimu tuko nyuma kabisa na tuseme ukweli, kwani hatuipati Elimu ya Juu kutokana na nini? Msingi wa fedha zenyewe hatuzipati za kutosha.

Mhe. Naibu Spika, hili nitakuwa mkali sana na tumeshachoka Mhe. Waziri. Sasa mambo kama haya Mhe. Naibu Spika, tukiwatetea wako huko nje wanakwenda kusema vyengine, jamani tutafika wapi na tunachotetea ni maslahi ya Wazanzibari na tupewe haki zetu.

Kwa mfano, ukitizama *average* yetu sisi ya Elimu ya Juu hapa Zanzibar na wenzetu kule *Mainland* ni tofauti, wenzetu wako juu zaidi kuliko sisi, kwa sababu fedha zenyewe zimelala kule na hapa hazilali, mnahangaika na *briefcase* kila siku jua na mvua na kurudi hapa kutuletea jibu *nothing*, hamna kitu. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana hali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Makamu wa pili tumsaidie kazi, ili kuweza kuondoa hili zogo la kila siku, tumeshachoka Mhe. Naibu Spika, kila siku bodi inakaa na Waziri mwengine wa Elimu, pia atakaa mwengine atakuja na Mhe. Mshimba pengine azikose.
Lakini jambo la msingi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kama hivi sasa mtakwenda kukaa kitako kwenye Vikao vya SMT na SMZ *mabaunsa* tupo hebu tuiteni na sisi tufike Mhe. Naibu Spika, kwa ajili ya kudai haki zetu na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wala usipate tabu jamani tumekuja na watu wa *bachbenchers* wakiongozwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe.

Hamza Hassan Juma, Mhe. Ismail Jussa Ladhu wako nje wanasubiri haki yao na wametuambia hatutoki humu ndani kama hatukutoka na haki yao. *(Makofi)*

Maana yake mule ndani mutoke na *cheque* au *agreement* ya uhakika ambayo imesainiwa na tunaiamini, vyengine vyovyote hamtoki na nyinyi tutakufungieni mlango na sisi tupo, uone kama haki haikuja Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, hebu jaribu uone suala hili, tena nakwambia *believe me* na niko *serious* na wala sio kama ni *joke* tumeshachoka, kwa sababu fedha zetu hatuzipati kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Wizara hii mambo mengi sana imetufanyia kwenye majimbo yetu, basi sikuwa na hoja nyingi sana. Kwa kweli wamejaribu kutumia ile Mifuko ya Wafadhili kwa kujenga au kufanya ukarabati maskuli yetu na tumeyaona, hapa sina tatizo.

Lakini tatizo au haki yangu kutoka *Mainland* kuletwa hapa na mimi ndipo ninapokuwa mgomvi na ndipo nitageuzwa kila jina na niambiwe kila jina na wala sitosikia mimi, kwa sababu haki ya mwananchi wangu wa Zanzibar lazima nitaitetea kwa mujibu wa Katiba, kwa kuwa kitu kimo ndani ya Katiba, kwa nini nisikitetee na mimi nitakuwa msaliti naipinga Katiba yangu. Kwa hivyo, nitatetea kitu ambacho kimo ndani ya Katiba kuendeleza na kuhakikisha Wazanzibari wanapata Elimu ya Juu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante na sasa nafasi tunampa Mhe. Rashid Seif Suleiman, ajiandae Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak na baadaye Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru, pia namshukuru *Allah* kwa kutupa uhai, uzima na taufiki ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Vile vile na kushukuru wewe tena kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo kuchangia machache kuhusiana na Bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. *(Makofi)*

Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na muda mrefu aliochukua, lakini tulimaliza kwa wakati na baada ya kutoka pale ndio Mwenyezi Mungu akatuletea mitihani.

Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ziwani natoa mkono wa pole kwa wote wafiwa, ambao kwa taarifa nilizopewa baadhi ya wananchi wa Jimbo la Ziwani wamo. Kwa hiyo, wote

Zanzibar, Tanzania na kwengineko kote natoa mkono wa pole na tuchukue ile ya uvumilivu, kwa sababu tutaletewa mitihani mbali mbali na wanaozingatia wazingatie.

Mhe. Naibu Spika, jengine baada ya hayo, naomba Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema waliotangulia mbele ya haki na wale wafiwa awape subra na hivi ndivyo maisha yalivyopangwa.

Sasa tukija kwenye bajeti, nilikuwa nikijiuliza mimi wakati nilipokuwa *Form V* na *VI* ilikuwa mwaka gani? Nikajiambia kwamba ilikuwa ni mwaka 1974 na 1975. Kwa hiyo, nikafanya hesabu hapa mpaka hivi leo nikaona ni miaka kama 37 tokea kumaliza *Form VI*. Mhe. Naibu Spika, wakati ule ilikuwa *Form V* na *VI* iko Lumumba tu na wala sio sehemu nyengine, ndipo tulipopata na haikuwa ajabu tulikuwa tukisomeshwa na walimu wa ndani ya nchi na baadhi yao walimu walitoka nje na *mostly* walikuwa ni kutoka India. *(Makofi)*

Lakini leo nimepata masikitiko makubwa sana, kwamba baada ya miaka 37 sio kuwa tuagize walimu wa Chuo Kikuu, tunaagiza walimu wa Sekondari kutoka nje. Kwa kweli hii lazima tujiulize tumejikwaa wapi? Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa tumeanzisha Vyuo Vikuu, basi hiyo ingelieleweka kuagiza walimu wa Vyuo Vikuu, kwa sababu walimu wa Vyuo Vikuu wanatakiwa wawe na viwango vikubwa vya elimu pamoja na uzoefu. Kwa hivyo, si rahisi kupatikana kirahisi katika nchi yetu, lakini kuagiza walimu tena wa *Science* na *Maths* hapa Zanzibar. *(Makofi)*

Jambo la kushangaza ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kumbe ina fahari, kwa sababu wametia picha kwenye kitabu chao, mimi nilifikiri watakuja hapa kwa masikitiko makubwa kwamba hatukuwa na la kufanya isipokuwa ni kugaiwa walimu kutoka Nigeria, lakini kumbe wameona ni jambo la maendeleo makubwa, yaani wametia mpaka kwenye kitabu chao, huu ni msiba. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi sikusoma Kiingereza, lakini hawa Waheshimiwa Wa-Nigeria wakizungumza mimi *pronunciations* zao sizifahamu vizuri. Sasa nafikiri wakifika kwanza wapelekwe Taasisi yetu ya Lugha, ili wakabadilishe zile *pronunciations* kwanza, ili angalau waweze kuwafahamu wanafunzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi nilipokuwa nikichangia kuhusu Bajeti za Wizara ya Elimu, nilisema kwamba tathmini ya bajeti katika ngazi mbali mbali za elimu zinatakiwa zichambuliwe, ili tuweze kujua tunatumia kiasi gani katika Skuli za Maandalizi, Skuli za Msingi, Skuli za Sekondari na hata katika elimu ya Chuo Kikuu.

Kwa kweli hii inasaidia wakati yanapotoka matokeo ya mitihani ya ngazi tofauti, tunaweza tukarudi na kusema kwa nini matokeo haya ya mitihani yanatokea hivi, ni pahala gani ambapo tumepapunja au hatukuwapa fedha za kutosha, lakini hii bajeti mchanganyiko haiwezekani kutathmini hata siku moja. *(Makofi)*

Kwa mfano, tunaweza kuwa tunawanyima Skuli za Msingi bajeti yao na kuipeleka Skuli za Sekondari na Chuo Kikuu ni watu wanaongojea kibendera waje wapokee na *cream* yote inatokea pale Skuli ya Msingi na ndipo panapo andaliwa. *(Makofi)*

Sasa lazima hizi bajeti zetu tuzipange na sio kwamba kila bajeti ya kila Wizara iwe inalingana na Wizara nyengine, kwa sababu hii Wizara ya Elimu ina bajeti yake na wenzetu wameshaanza kupanga hivi na tayari wamepata maendeleo, tena bajeti yote kikamilifu ya uendeshaji, *administration*, *current expenditure* pamoja na mishahara na kila kitu kinapangwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunajua *exactly* mwanafunzi wetu akitoka darasa la saba ameshatumia kiasi fulani, mwanafunzi wetu akitoka *Form IV*, yaani kuanzia *Form I* mpaka *IV* ameshatumia kiasi fulani na kwa hivyo ikiwa nchi yetu itapata ongezeko la bajeti basi tunajua wapi pa kuingiza na wala sio kama tunababaisha tu na hivyo ndivyo inavyopangwa bajeti. *(Makofi)*

Lakini kila siku tunaletewa bajeti ambayo ya mchanganyiko na wala huwezi kujua chochote na hata kusema hapa *Primary* tunavunja, pale *Secondary* hivi, kwa kweli tunadanganyana au Kiswahili kizuri tunavungana ama tunababaishana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri, hivi sisi hatusomi kutoka kwa wenzetu. Kwa mfano, hapa tunapitisha safari za nje na huko nje tunakwenda kufanya nini na siku hizi kuna mitandao tele na wala hakuna haja ya kwenda huko nje, yaani ukifungua tu mtandao unakwambia. Kwa kweli nashukuru Wizara ya Elimu hivi sasa inataka kusambaza mpaka *Primary* na sikwambii wao wenyewe. Kwa hivyo, tunataka kujua kwa nini bajeti inachanganywa namna hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hata hiyo ya kuchanganya kitabu cha mara hii kina matatizo, kwa sababu sisi tulitegemea kwamba kila Idara itamaliziwa mambo yake na vitengo vyake, lakini inamalizwa Idara na baadaye vitengo na wala hakijulikani hichi kiko huku au wapi, yaani vitengo tu, sasa hivi vitengo viko peke yake na wala haviko chini ya Kurugenzi fulani. Kwa utaratibu wa

kibajeti kila kitengo unakiweka chini ya Kurugenzi yake na mwisho inatajwa ile na wewe msomaji unajua. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu bajeti ya Chuo Kikuu cha *SUZA*. Katika kitabu hichi imeandikwa tu, kwamba wamepewa au wametengewa ruzuku ya bilioni 4,200,000,000/= kwa matumizi ya kawaida. Mhe. Naibu Spika, nauliza sisi Chuo chetu Kikuu kiko katika *development stage*, yaani kiwango cha kuendelea cha maendeleo, bado hatujafikia pahala na tukasema sisi Chuo Kikuu chetu tayari ni *established*.

Kwa hivyo, mbona hamna pahala inapoeleza bajeti ya maendeleo ya Chuo Kikuu hichi cha *SUZA* iko wapi. Kwa mfano, nimekwenda kwenye Bajeti ya Wizara ya Elimu mwisho kule wanasema Bajeti ya Maendeleo ni shilingi bilioni 33,000,000,000/= je, nauliza katika hizi ngapi za *SUZA*, hazikutajwa zimesahauliwa au hamna hata kitu kimoja cha maendeleo kwa ajili ya *SUZA*? *(Makofi)*
Mhe. Naibu Spika, nije kwenye samani. Mhe. Waziri wa Fedha hapa alituambia mara hii mbali ya fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya samani za skuli, lakini kuna shilingi bilioni 2,000,000,000/=.

Sasa nawauliza Wizara ya Elimu, mbona haijajitokeza mahala na hizi shilingi bilioni 2 hawatarajii kupewa au Wizara ya Fedha wenyewe ndio watakaotumia ama vipi, kwa sababu nimetizama kwenye kifungu cha samani nimeona mwisho kwa Idara ya Mipango na Sera labda ndipo zilizo samani za skuli ni shilingi milioni 9 na kidogo tu.

Katika Sera ya Elimu Mhe. Naibu Spika, wanasema kwamba tutatoa nafasi au fursa sawa kwa wanafunzi wote. Mimi napiga kelele kila siku hapa kwamba lazima tufikie lengo la kuona kwamba mwaka fulani tunamaliza kabisa tatizo la wanafunzi kukaa chini, kwa nini hatuwezi, sasa maana ya Wizara au Serikali maana yake nini? Ikiwa jambo kama hilo moja, hatuwezi kwenda hivi hivi mpaka lini na lazima tuwe na lengo.

Sasa ikiwa lengo lile halikufikiwa ndio wale Mawaziri au waendeshaji wa Serikali watajiuliza kwa nini halikufikiwa, lakini Mawaziri hawataki kuji-*commit* kwenye lengo. Kwa mfano, mimi nilimwambia Mhe. Waziri wa Elimu aliyekuwepo katika bajeti ya mwaka jana na nilimwambia kwamba tunazo Sherehe zetu za Mapinduzi za Miaka 50, mwaka 2014.

Kwa hivyo, ni vyema tukate hizi sherehe kwanza na tu-*supply* wanafunzi na kila mwanafunzi akae juu ya kiti na meza yake na halafu miaka 50 na sisi tutachangia sherehe hizo, kwa sababu wanafunzi wote watakuja kukaa kwenye viti, lakini hatuwezi kufanya maamuzi. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, Mhe. Waziri tupe uhakika kwamba ni lini Zanzibar kila mwanafunzi atakaa juu ya kiti na meza badala ya kupinda mgongo. Kwa mfano, tungelikuwa tunagawa hizi nafasi sawa, kwamba wanafunzi wote wa darasa la kwanza wanakaa chini, lakini kuna skuli wanakaa kwenye viti wote na skuli nyengine hawana au nusu ya skuli haina, sasa huo usawa katika skuli uko wapi. Kwa hiyo, lazima tufike pahala tuweze kutoa maamuzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, siku moja niliuliza hapa tulikuwa na mfadhili aitwae *OPEC* aliwahi kutuchangia na alitutoka vipi, je wafadhili hawatutoki kwa njia hizi hizi tu za kubabaishana? *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nije kwenye maslahi ya walimu Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli walimu ni watu ambao wanafanyakazi saa 24, na wala kazi ya mwalimu haimaliziki, ukitoka skuli unakwenda nyumbani lakini kuna kazi yake unaitayarisha. Sasa maslahi yao ni lazima yatizamwe uzuri. Tunashukuru Serikali kwa jumla lakini je, hicho kiwango tulichofikia hapo tulipo sisi wenyewe huko Serikalini tulijitizama ndicho kiwango tunachokiweza au ndicho kiwango tulichokifikiria tu kuwapa. Kwa sababu walimu na wao ni binaadam na wengine wengi ni wazalendo sana. Lakini sisi wenyewe tujiamini kwamba hichi kweli ndicho kiwango tulichofikiria kuwapa na ndio uwezo wetu.

Kuna baadhi ya mambo huwa tunakubaliana ndani ya nchi kuyafanya, wakati mwengine ni kinyume na Matakwa ya Kimataifa au viwango vya Kimataifa, lakini kwa dharura huwa tunayafanya. Tuna Wizara ya Afya hapa tuliiuliza maswali ikawa inajikinga kweli kweli, vijana wetu wanafundishwa udaktari hapa hapa nchini hapana chuo, hapana chochote. Lakini tumekubaliana kwamba hawa watafundishwa hapa halafu baada ya miaka mengine watakwenda nje kujifundisha na Wa-Cuba.

Kwa hivyo, kuna baadhi ya walimu tuliwapa sisi wenyewe viwango kwamba hawa wanaweza wakasomesha Sekondari. Kwa nini ghafla uje huu mtikisiko huu wa huyu kafika hapa, kafika hapa, bila ya Wizara ya Elimu kusimama wakasema hawa tunawaweka hapa na hawa tunawaweka hapa na waka-*defend* kwenye utumishi. Kwa sababu kazi yao Utumishi ni kutizama vile viwango halisi vya *certificate* lakini Wizara ya Elimu inayo uwezo wa kusema walimu hawa sisi tumewa *qualify* kwa kiwango hichi, kwa hivyo tunawalipa kiasi hichi, Inao uwezo huo Wizara ya Elimu.

La kusikitisha zaidi mimi nililifuatilia hili suala lililotokezea juzi, kwa nini walimu hawakupelekewa hata barua walipokatwa mishahara yao. Na niliwambia siku ile Mhe. Waziri wa Utumishi na Utawala Bora mzigo

mshawatupia Wizara ya Elimu huu. Akasema wao wameandika barua lakini Wizara ya Elimu yenyewe haikuwaandikia walimu wao. Naomba Mhe. Waziri uje ututhibitishie hapa kwamba kweli nyie mlipelekewa barua na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora kwamba walimu hawa watakatwa pesa zao, lakini nyinyi hamkuwaandikia barua wakenda wakaona ndani ya mishahara yao tu, uje ututhibitishie hapa leo ili Waziri nani aliyesema kweli atakuja kujulikana hapa hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kama ingelikuwa ipo elimu sasa hivi ingepewa thamani kwa Zanzibar na muelekeo wake ni elimu ya ufundi. Lakini kama ipo elimu iliyotupwa na kudharauliwa basi ni hii elimu ya ufundi. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aje atueleze hasa wana malengo gani ya elimu ya ufundi basi siye. Maana Tanzania Bara kuna vyuo vinaitwa *Institutes of sciences and Technology* kama hiyo yetu iliyokuwepo Mbweni. Lakini je, unaweza kwenda kuichukua ukaioanisha na ile. Sitaki Chuo Kikuu hiyo hiyo *Institutes of sciences and Technology* ichukue ukaioanishe na Arusha, ichukue ukaioanishe na Mbeya *Institute of Sciences and Technology* ambazo zipo huko mikoani na sisi ni Zenji hapa.

Mhe. Waziri tupo Zenji hapa na *Institute* yetu ndiyo ile pale. Hebu njoo utupe muelekeo wa Waizara ya Elimu na Elimu ya Ufundi. Maana yake hata zile Skuli za Vyuo vya Amali vilivyokuwepo Vitongoji na Mkokotoni vilivyoanzishwa juzi havina vitu, ndio vile vile walivyoombewa ndio vile vile. Sasa hivi wataazimana vijiko, msumeno mmoja utatoka Vitongoji utakwenda Mkokotoni na Mkokotoni watatoa patasi watapeleka Vitongoji, hakuna kitu kinachoingizwa. Hebu tupeni msimamo hasa Elimu ya Ufundi mnaiweka wapi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakuja kwenye matokeo sasa. Waheshimiwa matokeo ya mitihani nawashukuru sana katika kitabu cha Wizara ya Elimu kwamba wametupa jaduweli nzuri yenye matokeo ya kuanzia mwaka 2007 mapaka 2011. Lakini Mhe. Naibu Spika, wataalamu wote wanasema kwamba kuandika *data* sio muhimu sana, muhimu sana ni kuzifanyia uchambuzi zile data. Kuziandika tu ukawa nazo ni sehemu moja lakini sehemu muhimu ni kuzifanyia uchambuzi.

Mhe. Naibu Spika, katika miaka yote hiyo *division IV* na *division 0* kwa *form IV* ni asilimia 85.1, tukuchukulie kiwango cha kupasi ni *division I, II* na *III* lakini ukiwachanganya wale kwa miaka yote hiyo *division IV* na *division 0* ambao bahati mbaya basi Wizara ya Elimu wamenyamaza kimya kama haipo hii *division*, wameweka I, *II, III, IV* ile 0 wameinyamazia kimya. Sawa lakini *percentage* mwisho ni 100 hakuna zaidi ya mia *percentage*. Sasa na sisi tukifanya tunatizama mbona 100 haijatimia, tunasema ndio ile ziro.

Mhe. Naibu Spika, tunaridhika na matokeo haya ya asilimia 85 katika kipindi chote hicho asilimia 85.1 ya wanafunzi wamefeli. Hebu tupeni msimamo wa Wizara ya Elimu uko vipi katika marekebisho yenu. Kwa sababu moja katika masharti ya kuandika Sera ni kuitathimini pengine Sera yetu tuliyoiandika haitufai. Tutathmini kwa nini wanafunzi wanafeli hivi.

Mhe. Naibu Spika, *form VI division IV* na *division 0* ni asilimia 45 ambao angalia hawa ni wale waliopasi form IV wakawa na *qualification* za kuingia *form V* na *VI*, lakini kufeli yao ni asilimia 45, tuko wapi.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, tupeni Msimamo wa Wizara ya Elimu kuhusu Dakhalia. Pamoja na matatizo yote tuliyonayo juzi tumesikia hapa mabadiliko ya vikosi, sasa watakula kwenye kambi zao. Je, wanafunzi watakula wapi na wao wakajiunge na vikosi wapate kula. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarouk: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nami nichukue fursa hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza leo kufika katika Baraza hili tukufu na kutekeleza shughuli zetu. Pili nirejeshe shukurani kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwako kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mawazo yangu katika Bajeti hii ya Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa ya kutoa mkono wa pole kwa janga ambalo limetokea ni msiba wetu sote kwa hivyo Mwenyezi Mungu atupe moyo ya subra juu ya msiba huu na Waislamu wote tuelekee katika *taqwa* ya Mwenyezi Mungu kwamba jambo lolote analolitaka litokee basi litakuwa, hakuna yeyote atakayeweza kuzuia, Mwenyezi Mungu akilipanga liwe litakuwa. Tuone kwamba matukio yake Mwenyezi Mungu haleti nakama ila kwa vitendo vyenu mnavyovifanya.

Kwa hivyo haya ni mapigo ambayo anatupiga Mwenyezi Mungu, tunatakiwa turudi sote kwa Mwenyezi Mungu. Haleti nakama Mwenyezi Mungu ila tunakosea Allah (SW). Mambo mengi yametokea wenzetu jinsi gani walivyokuwa wakigharikishwa. Kwa hivyo na sisi tusome na tukae viongozi na Mashekhe tuone kwamba tuna makosa makubwa.

Leo namwambia Mhe. Waziri wa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, hawa vijana ambao wanafanya ulawiti asiwapelekee kondom hawa. Leo mtu mmoja ambaye atafanya ulawiti katika nchi mmoja tu basi *Arshi* ya Mwenyezi Mungu inatikisika. Leo wako wangapi, wanaofanya matendo kama haya. Basi tuone tunafanya jinsi gani na Mwenyezi Mungu anatutia adabu kiasi gani. Kwa hivyo turudi kwa Mwenyezi Mungu.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, nianze katika ukurasa wa 33 ya Bajeti ya Mhe. Waziri wa Elimu. Katika Elimu Mbadala, katika kitabu hiki kimeelezwa kwamba kuna skuli za msingi 37 ambazo zimeanzisha madarasa ya elimu ya maandalizi. Ukifungua kitabu hiki katika ukurasa wa 35 unakuta kwamba kuna upungufu wa madarasa, huku unakuta kwamba skuli hizi za msingi zinafungua madarasa ya maandalizi. Mimi naomba Mhe. Waziri hebu tuangalie upungufu huu wa madarasa tuliokuwa nao katika skuli zetu za msingi na jopo la wanafunzi tulilonalo katika madarasa. Hatuoni kama kutenganisha hizi skuli za maandalizi kuziweka mbali na hizi skuli zetu za msingi zikawa mbali ili kupata unafuu wa kupunguza na kupata madarasa tukayatumia kwa vizuri kwa wanafunzi wetu waliokuwepo pale.

Naomba Mhe. Waziri hebu tulifikirie hili, unakuta darasa moja lina wanafunzi 120, mwalimu anasomesha vipi. Halafu na leo tukaweke na mle mle skuli za maandalizi. Naomba hili Wizara liliangalie kwa makini lakini ifikirie kuona hatua kama hii kuweza kuzitenganisha hizi skuli zetu.

Halafu chini huku anasema kwamba Wawakilishi kuwashajihisha wananchi kuendelea kuchangia maendeleo ya elimu. Mimi nasema tuwapongeze wazee kwa hili wanachangia vya kutosha. Mzazi yoyote basi atafanya juhudi aende japo kwa Mwakilishi au Mbunge wake lakini mwanawe achangie skuli. Lakini cha kuwashajihisha mno pia tuwashajihishe walipe madarasa. Vyuoni watoto walipe, kwa sababu tayari mwanafunzi huyu hupo radhi aweke rahani kitu chake akalipe skuli. Kwa hili wananchi wanajitahidi sana kwa kuchangia skuli, lakini madrasa hawazichangii wale wazee. Nadhani nazo tutilie mkazo pia madrasa wazee washajihishwe wawasaidie walimu. Kwa sababu hata madrasa tunapiga kelele sana walimu wasaidiwe hakuna chochote. Kwa hivyo mchango wao mara nyingi unatoka kwa wazee. Kwa hivyo pia washajihishwe wazee wachangie madrasa kwa sababu nguvu zote wanaziisha katika skuli. Mimi nadhani hili cha msingi tuwapongeze wazee kwa juhudi wanayoifanya pia tuwashajihishe wachangie madrasa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika ukurasa wa 79 kuna suala zima la kesi za ujauzito na ndoa za wanafunzi. Hili ni suala zito ni suala ambalo kila siku linazidi. Nakumbuka katika Baraza la Saba kuna Mwakilishi mmoja Mhe. Harouna alitakiwa ajenge mabweni ya kulelea watoto. Na mimi leo namuuliza Mhe. Waziri je, keshayatarisha haya mabweni ya kulelea watoto. Kwa sababu sheria zetu wenyewe tulizozipitisha hizi ndizo zitakazotufunga. Leo mtoto wangu akipita kiwango akiolewa tayari anambiwa asende skuli. Huyu anayebeba mimba mwanafunzi tayari huyu sheria inamtaka kwanza azae akisha arejee skuli akishakutimiza masharti. Kwa hivyo tayari watoto wanajua

mimi nikishachukua mimba nazaa mtoto namuweka halafu narudi skuli, kwa hiyo tutayarishe haya mabweni ya kulelea watoto, kutokana na hali hii.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala zima la wakaguzi. Nimeona hapa katika ripoti kuna wakaguzi wanane wapya na wakaguzi wawili walihudhuria katika mafunzo ya matumizi ya *computer*. Mimi nataka nimuulize tu Mheshimiwa kwamba wakaguzi hawa ambao uliowaainisha hapa ni kutoka sehemu gani, ni wote wa Pemba, au na Waunguja na katika wakaguzi hawa wamo ambao watashughulikia masomo ya kiingereza. Naomba hilo uje unisaidie.

Mhe. Naibu Spika, jengine nije katika suala la maslahi ya walimu ambalo Mhe. Rashid Seif keshalichangia lakini na mimi kama sijalizungumza nitakuwa mkosefu wa fadhila kwa sababu naijua thamani ya walimu. Bado maslahi ya walimu hayakidhi haja na kila nikisimama katika Wizara hii mimi nitasema na nina msemo wangu siku zote huwa nasema "*Inna-l mu allima wa twabiba kilaa huma laa yanswihani idh lam yukram*" Hakika ya mwalimu na daktari wawili hawa huwezi ukanasihika kama hukuwatukuza na kuwatukuza kwao ni kuwafanyia katika maslahi mazuri".

Kwa hivyo mimi nadhani mtu afike atakapofika lakini ana anzia kupata elimu na mwalimu ndiye anayemfanyia kazi hii, hata akiwa jaji, akiwa nani lakini ananza kwa mwalimu ndiye anayemfundisha na akampa heshima hii. Kwa hivyo huwezi ukapata heshima ukawa wewe Rais, ukawa Waziri, ukawa nani kama hukuanzia hapa, mwalimu hakukupa wewe taaluma, nadhani hili tulione.

Mhe. Waziri kuna matatizo baadhi ya walimu hawapewi maposho yao ya likizo. Kwa hivyo kwa nini walimu hawa hawapati maposho yao ya likizo. Jamani tuwatizameni walimu vizuri, na hili naomba Mhe. Waziri uje unijibu.
Mhe. Naibu Spika, jengine kuna malalamiko ambayo yametokea katika skuli ya Potoa naomba uje unijibu vizuri. Skuli hii ina walimu mahiri, walimu wazaliwa, walimu ambao wanapasisha vizuri kutoka michipuo, wanatoka watoto 10, 9. Ni skuli ambayo walimu wake ni wazalendo. Lakini kuna tatizo kuna walimu watatu pale wamesimamishwa kazi. Ni sababu zipi zilizopelekea walimu hawa kusimamishwa kazi. Naomba uje unieleze kama kuna sababu yoyote au Wizara tu ilikurupuka ikapelekewa fitna na ikachukua suala la kuwasimamisha. Kwa hivyo uje unieleze ni sababu zipi zilizowafanya walimu hawa mwalimu mmoja wa msingi, mwalimu wa Sekondari walikuwa wawili. Kwa hivyo uje unieleze ni sababu zipi zilizosababisha kwamba walimu hawa wasimamishwe kazi kwa ghafla.

Jengine tuje katika suala la *tuition*, mimi nazipiga vita *tuition*. Mheshimiwa *tuition* hazitusaidii, *tuition* zinatuletea madhara, zinatuletea matatizo.

Nakumbuka kipindi cha nyuma wazee walipiga kelele na sisi tulipiga kelele jamani *tuition*, tusingoje mpaka tusemwe kwa maneno maovu huko nje. Mhe. Harouna alizisimamisha *tuition* kilichotokea nini. Tulikuwa tunasemwa kwa mambo mabaya huko nje, bila shaka labda kuna mtoto wa kiongozi kafanywa mambo mabaya ndio zikastopishwa *tuition*, lakini *tuition* haitusaidiii.

Kuna mwalimu mmoja juzi ananambia anamkuta mtoto wa *tuition* anasomeshwa kwa vitendo viovu. Katika kupapatua akaipata simu ya mtoto mwanafunzi mwanamke, akaichukua akampigia simu mama ake. Unamjua mwenye namba hii, akasema namjua akaulizwa nani, akasema mwanangu. Akaambiwa njoo sasa hivi huyo mwanao basi hayupo *tuition*. Jamani hizi mimba zilizotajwa zinapatikana huko *tuition*. Tunaomba Mhe. Waziri *tuition* hazitusaidii na walimu mimi nadhani kama ingelikuwa si hizi *tuition* wangelikuwa wakisomesha vizuri. Lakini yote yanakuja mwalimu yule yule anasomesha pale anajua namtaka mwanafunzi huyu aje *tuition* aje anipatie Sh. 200/-

Tulioneni hili, mtoto saa 4 bado yupo majiani mtoto mwari, *tuition* hazitusaidii. Mimi mwenyewe nnao watoto wangu wawili wari wako Chuoni hakuna hata mmoja aliyekwenda *tuition*. Mungu akitaka kukupa anakupa tu, hakuletei barua mmoja yupo Chuoni Mbweni anasoma hapo, nilipiga vita sitaki *tuition* na hata mmoja hakwenda *tuition*. Hili suala tuliangalieni, kusoma mtu kunataka idili yake mtu mwenyewe. Mzazi mtoto atakuaga nakwenda *tuition*, wewe utamwambia nenda mwanangu. Japo wanatoka ndani watoto wetu na maninja mazuri tu wanakwenda *tuition* akifa hapo anavua ninja anavua na baibui.

Naomba Mhe. Waziri hili tulione. Jengine Mhe. Waziri suala zima la elimu ya mjumuisho bado miye inanipa wasi wasi hii elimu ya mjumuisho. Wasi wasi wangu nahisi hawa watoto tunawakosesha elimu. Haiwezekani kama nilivyosema darasa lina watoto 120, mwalimu yule keshachoka akashughulikie watoto wale wawili waliokuwemo mmle. Bado nalo tulione hili, tunawanyima elimu hawa watoto. Haiwezekani hata siku moja mwalimu binaadamu na yeye, tunampa mzigo mchanganyiko ule uliokuwemo. Hili mimi naona bado linanipa wasi wasi labda Waziri atakuja kunipa majibu mazuri mpaka na mimi kichwa changu kifunuke nione kweli hawa watoto wanafaidika na hii elimu.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuna suala zima la mitaala yetu. Mhe. Waziri mfumo mzuri wa kufundisha watoto ni lazima uwe na muungozo wa kufundishia. Mheshimiwa uliwahi kusema hapa kwamba suala hili limo katika mchakato. Kwa hivyo nakuomba Mhe. Waziri uje unieleze je, mchakato huo au muungozo huu maalum umefikia wapi mapaka sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, katika skuli zetu kuna kitengo cha ushauri nasaha. Mimi naomba uje unieleze kwamba kitengo hichi hizi ripoti zake wanazipeleka wapi juu ya huu ushauri nasaha unaotolewa humo maskuli. Kwa sababu maskuli yetu kuna mambo ambayo mengine mazito. Hebu nenda skuli ya Nyerere katembelee pale. Ndio maana naona hivi vitengo vya ushauri nasaha vinapelekwa wapi au ushauri nasaha wanao ukimwi tu, hakuna mengine.

Kuna watoto wetu wa kiume maskuli wanaharibiwa, nenda Skuli ya Nyerere, katafute ushahidi utaupata, kuna watoto wadogo wa darasa la sita na darasa la tano, wameshabadilisha sauti watoto wa kiume. Nenda Kiembesamaki, wapo walimu wanatusikitikia, watoto wa Nyerere wapo, kuna mtoto pale tumekwanda akahojiwa akaulizwa je, ukiitwa kwenye vyombo vya habari unaeleza kama hivi unavyoeleza. Akasema nitaeleza, aliyekuchukua akakufanya hivi utasema, akasema nitasema. Na katwambia huyo mtu kasema kwa Serikali hii ukenda popote sisi hatufungwi.

Tuione hii hali wanafunzi wetu ambao tunawategemea kesho waje kuwa Maspika, kesho waje kuwa Mawaziri, waje kuongoza Serikali hii, mtu keshakuwa anapunga mkono atakuja kuweza kuiongoza Serikali. Tuone Mhe. Waziri hivi vitengo kama vinafanya kazi vifanye kazi vizuri na ripoti iletwe. Itapoletwa ripoti Waziri ni lazima wanafunzi wetu anayehusika na hayo tujue anachukuliwa hatua gani.

Nina imani nimetaja skuli mbili tu hizo kwa hali iliyokuwepo si skuli mbili, inaonesha zipo skuli nyingi kwa sababu ikiingia balaa haiingii pahala pamoja balaa linaingia kila pahala. Tuone hii hali kwamba wanafunzi wetu wanachukuliwa hivi sasa wanaharibiwa mtoto mdogo anapewa simu si kiasi chake. Mtoto unamuhadaa kwa kitu kidogo tu, kwa hivyo naomba uje unieleze kitengo hiki cha ushauri nasaha ripoti zake zilizokuwepo tujue zinapelekwa wapi.

Mhe. Naibu Spika, pia katika Maskuli kuna Kamati za Maskuli, naomba Kamati hizi nazo uzifatilie kuna Kamati zinafanya uzuri katika Maskuli na zinaleta maendeleo katika zile skuli. Naipongeza sana Kamati yangu ya Skuli ya Ndijani, tarifa mimi mwenyewe wananipa barua, nakwenda pale kupanga, kujua skuli zao zipo vipi, nashukuru wametoa barua kwa kila aliyesoma pale achangie skuli ile apitie kwenye benki kwenye *account*.Wanafanya kazi nzuri, zamani tu kulikuwa kuna mambo ya kisiasa ilivyokuwa hatujakaa vizuri. Miye baadahi ya Kamati walikuwa wakisema kwamba nisiletewe barua lakini sasa hivi nashukuru naletewa barua. Kwa hivyo kuna baadhi ya skuli kamati hizi hazisaidii kitu, kile cha skuli wanakitaka wao. Kwa hivyo hizi nazo naomba zifanyiwe kazi.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, natoa tena mkono wa pole nawaomba wananchi wa Zanzibar tuwe na subra kwa haya. Turudi kwa Mwenyezi Mungu tulipomkosea, turudi, tuleteni toba. Baada ya hayo nitaunga mkono Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja kunijibu kwa vizuri na kwa ufasaha katika hoja zangu nilizozitoa. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Naomba niwajulishe kwamba tumepata ugeni katika Baraza letu. Ujumbe wa Waheshimiwa Wabunge wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania jumla yao ni 40, wamekuja kuungana na sisi katika kuomboleza msiba tulioupata jana wa kuzama meli. Kwa hivyo tunawashukuru kwa niaba yenu na wanaongozwa na Mhe. Mahmoud Chombo yeye ni Katibu wa Bunge wa Zanzibar. Naomba wasimame muwatambue. Ahsante sana naomba tukae.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magomeni nitoe mkono wa pole kwa familia za marehemu waliofariki katika ajali ya meli iliyotokea hivi karibuni kwa kweli tulipatwa na huzuni kubwa juu ya tukio hilo ambalo limetokea. Tunawaomba familia za marehemu wawe na moyo wa subira katika kipindi hiki cha msiba.

Mhe. Naibu Spika, hili ni tukio la pili katika muda mfupi, limeweza kutokea katika visiwa vyetu hivi vya Zanzibar. Pamoja na kwamba ni Rehma ya Mwenyezi Mungu lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, itabeba dhamana juu ya tukio hili. Pamoja na kwamba ni Rehma ya Mwenyezi Mungu lakini na uzembe nao unachangia. Serikali pamoja na Wizara ya Mawasiliano au Wizara ya Miundombinu watawajibika katika kitendo kile.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo mafupi juu ya msiba sasa nije kwenye ripoti hii au hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoisoma, tumemsikia na tunaunga mkono hotuba hii.

Katika hotuba ya Mhe. Waziri amezungumzia mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2011/2012. Katika maeneo ambayo ameyaeleza Mhe. Waziri ya mafanikio amezungumzia juu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, kwamba kimetimiza miaka kumi tokea kuanzishwa kwake mwaka 2002. Mhe. Waziri ametueleza kuwa Mkuu wa Chuo cha Zanzibar ambaye pia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu.

> "Ameunda Kamati ambayo itachunguza uwezekano wa taasisi nyengine za elimu ya juu zilizokuwepo Zanzibar kuweza kuunganishwa na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Kamati hiyo imeshawasilisha ripoti yake kwa Mkuu wa Chuo ambaye ni Mhe. Rais na hivi sasa inaandaa utaratibu wa taasisi nyengine za elimu ya juu zilizokuwepo Zanzibar kuweza kuunganishwa na kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, hatua kwa hatua."

Mhe. Naibu Spika, maelezo ni mazuri, lakini katika jambo hili la kuunganisha vyuo linatakiwa lifanywe kwa tahadhari kubwa. Nimuombe sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi jambo hili halitaki haraka. Kwa sababu Chuo Kikuu hichi cha Taifa (SUZA) tukiangalie uwezo wake, maendeleo yake, tukishakukihisi kwamba sasa kinaweza kuunganishwa na vyuo vyengine basi tunaweza tukafanya hivyo. Kwa sababu bado shuo hiki hakijaweza kutoa maendeleo makubwa.

Kuna taasisi nyengine hapa Zanzibar sasa hivi kwa mfano Chuo cha Usimamizi wa Fedha Chwaka kimepiga hatua kubwa, kinakwenda vizuri. Lakini kuzifanya taasisi hizi kuziunganisha pamoja ni kuziuwa zile taasisi nyengine. Jambo hili Mhe. Spika, linahitaji kuangaliwa kwa makini sana.

Mfano mdogo Mhe. Naibu Spika, wenzetu hawa wa SUZA wapo katika jumuia ya TCU *(Tanzania Commission for Universities*) wamo lakini sasa hivi wanashindwa wanafunzi wao wakuomba maombi ya Chuo kupitia TCU kwa nini tujiulize, sababu gani. Mpaka wakafika pahala wao wanatoa fomu za wanafunzi kujiunga moja kwa moja kwenye SUZA lazima hapa kutakuwa na kasoro.

Mimi kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wazo la Mhe. Rais ni zuri lakini linahitaji kuangaliwa kwa umakini wa hali ya juu. Vyenginevyo tunaweza tukaviuwa na vyuo vyengine ambavyo tayari sasa hivi vimeshapiga hatua na vipo katika hatua kubwa. Hilo moja Mhe. Naibu Spika.

La pili ni suala la Bodi ya Mfuko wa Elimu ya Juu tunaipongeza kwa shughuli zake wanazozifanya na tunaipongeza serikali kwa kuongeza kiwango cha Fedha katika bodi hii kutoka shilingi bilioni 4 katika mwaka uliopita na kuwa bilioni 8 kwa mwaka huu wa fedha wa 2012/2013. Hapa wametueleza kwamba bodi inatarajia kupeleka masomoni wanafunzi wapya 800 kwa kiwango cha Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili, katika vyuo vya ndani ya nchi, wakatwambia wananchi watakaoteuliwa watateuliwa kwa mujibu wa fani zilizopewa kipa umbele kulingana na mahitaji ya soko.

Mhe. Naibu Spika, hapa panahitaji umakini na kwa sababu kuna taarifa ambazo zilizotolewa kwamba wanafunzi watakaopewa mikopo mwaka huu ni wale waliofaulu sayansi peke yake. Nataka Mhe. Waziri aje alithibitishie Baraza hili juu ya kauli hiyo, kwamba ni wanafunzi waliofaulu sayansi tu peke yake ndio watakaopewa mikopo. Kama hivyo ndivyo atueleze sababu.

Mhe. Naibu Spika, kitendo cha kuwapa kipaumbele wanafunzi wa sayansi tu kupewa mikopo ni kuwavunja moyo wanafunzi wanaosoma zile kada nyengine. Ambazo kada zile nazo pia ni muhimu. Pia tuangalie hivi tunavyotoa kipaumbele kwa wanafunzi wa sayansi kupewa mikopo, tuiangalie Wizara ya Elimu ni kwa kiasi gani imeweza kuwawezesha watoto wetu kusoma sayansi. Hadi leo ifike pahala kwamba tuwape kipaumbele wanafunzi wa sayansi. Kila wakati tunakuwa na kilio hapa cha sayansi, mimi katika chule yangu Sekondari ya Nyerere kuna mwalimu mmoja tu wa sayansi. Halafu leo unasema tunawapa kipaumbele mkopo kwa wanafunzi waliofaulu sayansi na kuwapa wale wengine.

Mhe. Naibu Spika, hili mimi sikubaliani nalo hata siku moja. Nakubali kwamba watoto wa sayansi wapewe kipa umbele, lakini na wanafunzi wanaosoma masomo mengine na wao wapewe kipa umbele na wapewe mikopo kama inavyostahiki. Wale wenye sifa ya sayansi wapewe mikopo na wale wenye sifa kwa masomo mengine wao wapewe kipa umbele, vile vile. Kwa hivyo hili linahitaji ufafanuzi wa kina Mhe. Waziri.

Jengine Mhe. Naibu Spika, kuna eneo hapa limeandikwa Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu. Mimi Baraza hili silielewi na jana nilimwambia Mhe. Naibu Waziri hapa, mimi ninavyokumbuka Sheria iliyopitishwa hapa ilikataa jina hili la Baraza la Upimaji na Tathmini leo tunashangaa kwamba jina hili limejitokeza tena katika kitabu chake hiki. Sasa hatuelewi kwamba amekosea, wamefanya kwa makusudi, wamesahau. Mimi nasemka kwamba sheria imepitishwa na Mhe. Waziri aliyepita likubali juu ya mabadiliko ya jina hili. Leo tunashangaa kwamba bado limejitokeza jina lile lile, Mhe. Waziri hebu uje utupe ufafanuzi. Kamka litakuwa limebakia jina hili hili nadhani Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tutakuwa wagumu kupitisha fungu hili. Kwa sababu chombo hiki hakipo kwa mujibu wa sheria.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, ametwambia hapa Mhe. Waziri kwamba Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu, Bara hili linamajukumu la kusimamia shughuli zote zinazohusu masuala ya mitihani ya SMZ ikiwemo utungaji, uchapishaji, usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba, kidato cha pili na mafunzo ya uwalimu yaani Astashahada ya msingi na mambo mengine. Nilikuwa najiuliza bodi hii mbali ya shughuli hii, hii mitihani ya taifa inashughulikiwa na chombo gani.

Huku mbele kuna maelezo yametolewa, lakini yameni comfuse, kwa sababu huku imeelezwa shughuli hiyo. Lakini hapa kwenye ukurasa wa 67, kifungu cha 145 kinasema kwa upande wa Mitihani ya Taifa ya kidatu cha nne ambapo imeeleza kati ya wanafunzi kadhaa wa kadhaa mpaka *form Six*. Sasa sijui kama chombo hichi kinasimamia yote au kinasimamia haya maelezo ambayo yametueleza hii ya huku ni *statement* tu, hiyo hatuelewi.

Mhe. Naibu Spika, jengine tunataka jutue hapa tulikuwa tuna kizaazaa juu ya wanafunzi waliofutiwa mitahani. Wazara ikasema kwamba pamoja na adhabu waliyokuwa wamepewa watoto ya kufutiwa matokeo lakini serikali au Wizara inafanya uchunguzi juu ya tuhuma za wale waliohusika na jambo hili. Sasa tunataka atwambie mpaka leo ni watu gani waliohusika na hatua gani za dharura zilizochukuliwa na hatua gani za baadae ambazo tunategemea kuchukuliwa kwa sababu muda umeshakuwa mrefu.

Lakini tunaipongeza serikali kwa hatua hii iliyochukua ya kuzungumza na wenzao wa Baraza la Mitihani la Taifa la kupunguziwa adhabu watoto hawa. Tunaipongeza na tunaishukuru sana. Lakini tunataka kujua ni adhabu gani iliyotolewa juu ya wote walioyohusika katika kadhia hii. Kwa sababu adhabu hii sio kwa wanafunzi tu na wale waliohusika. Tuhakikishe kwamba hawatorudia tena kufanya jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, jengine nizungumzie kitengo cha Uhasibu. Kitengo cha Uhasibu ametueleza hapa kinasimamia ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi wote wa Wizara pamoja na mahitaji mengine ya Wizara. Kumekuwa na malalamiko ya walimu, walimu wamekuwa wakilalamika kwamba wamekuwa wakikatwa mishahara yao ovyo. Mishahara yao imekuwa haina utulivu, leo wanalipwa huu kesho wanalipwa hivi, kesho wanalipwa hivi ni kwa nini. Kwa nini walimu hawa tumekuwa tukiwasumbua sumbua.

Kwa nini imekuwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hawajui mishahara yao, mwezi huu analipwa hiki mwezi unaokuja hiki, akienda anababaisha hivi, tunataka Mhe. Waziri uje utwambie hapa kwa nini walimu mishahara yao imekuwa haina utulivu, wanakatwa fedha zao ovyo, hili jambo la kusikitisha sana Mhe. Naibu Spika, hasa kwa wakati huu wa sayansi na teknolojia.

Kwamba tunatakiwa tuende katika utaratibu lakini tumekuwa tukiyumba yumba huyu kakatwa 28,000 huyu kakatwa hiki. Hao walimu wako wengi na wana malalamiko mengi juu ya mishahara yao. Halafu kumekuwa na visababu mbali mbali visivyokuwa na msingi. Sisi tunataka kuona kwamba walimu wetu wanalipwa mishahara inayostahiki tena mishahara mizuri inayostahiki na kada yao.

Jengine katika hapo Mhe. Naibu Spika, juu ya posho la walimu wakuu. Inasikitisha kwamba mwalimu Mkuu analipwa posho la sh. 15,000 kwa mwezi, *is it right*, kweli Mwalimu Mkuu na dhamana aliyokuwa nayo katika Skuli ya kusimamia Skuli nzima unamlipa posho la sh. 15,000/- kwa mwezi halafu umtegemee mwalimu mkuu yule afanye nini. Hii si kudharau shughuli za wenzetu, wakati dereva anayemuendesha kiongozi, Mkurugenzi au Katibu Mkuu au karani analipwa shilingi laki moja kwa mwezi.

Leo unamlipa mwalimu mkuu eti posho la uwalimu mkuu sh. 15,000/-, hiyo ni halali kweli. Hapa hatukubaliani na jambo hili, lazima walimu wakuu ambao tumewapa dhamana ambao wanasimamia walimu wote wanasimamia wanafunzi kuhakikisha kwamba wanasoma vizuri, wanafanya vizuri, walipwe vizuri maposho yao ya uwalimu, hili sio jambo zuri, hii tena ni dharau 15,000/- unampa mwalimu mkuu eti kwa dhama ya kusimamia skuli, halafu wewe utegemee kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho ili nisiutumie muda wako sana, hili nahitaji kupata ufafanuzi kwa Mhe. Waziri. Hili nadhani linahusu Baraza la Upimaji wa tathmini ya elimu. Sasa hivi utaratibu uliopo kwamba wanafunzi wa skuli *Candidate* ambao wanataka kufanya mitihani ya hii ya 'A' Level ambao umri wao sina uhakika wewe ndio utakuja kunipa uhakika. Umri wao wakitimia miaka 25 hawaruhusiwi kufanya mitihani yao kama skuli *Candidate*. Hili tunahitaji maelezo.

Wanafunzi ni wadogo, wanasoma bado wapo skuli, kwa sababu ya umri wao tunawabadilishia eneo kwamba wewe umeshatimia umri wa miaka 25 maana yake sasa ukafanye mtihani ya *Private* unamtoa kwenye skuli ya *Candidate* kwa nini iwe hivyo na yule bado ni mwanafunzi. Lakini kibaya zaidi Mhe. Naibu Spika, mwanafunzi yule anakujakuambiwa dakika za mwisho, mtihani upo pale anaambiwa majina haya hawa watafanya mtihani wa *private candidate* wakati huku ameshalipa, keshajitayarisha kwa kufanya mtihani wa *school candidate* dakika za mwisho wanabadilishwa wanaambiwa mtakwenda kufanya mtihani wa *private*.

Kwa nini tusiwaeleze mwanzo kama kuna utaratibu huo. Hatuoni kama tunawapotezea muelekeo, halafu tunakuja kusema kwamba wanafunzi wanafeli, wakati jama hili nyinyi mnalielewa. Wizara ya elimu inafahamu kama kuna utaratibu huu ambao ni mbovu. Huu utaratibu ni mbovu, *in fact* kama utaratibu upo lakini ni mbovu uhaufai. Lakini kama upo mbovu kwa nini wasiambiwe wanafunzi mapema, kwa nini imakuwa mtoto keshajitayarisha na wazazi wake wameshajitayarisha kwa ajili ya kufanya mtihani wa Skuli anaambiwa sasa akalipe fedha kwa ajili ya mtihani wa skuli

ya *private candidate.* Kwa nini na huyu ni mwanafunzi wa shule. Hili Mhe. Waziri aje atueleze vizuri, atuelimishe vizuri tuelewe, kwa sababu sisi ndio tunaowasimamia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sina zaidi mimi mchango wangu ni huo niunge mkono hoja ya Mhe. Waziri pale ambapo atakapojibu hoja zangu. Kwa kweli mafungu yake ni makubwa mno katika kitabu, nisengependa kuchambua moja baada ya moja lakini kwa kweli ana mafungu mazito. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe safari hii tutabadilisha *system*, hapa tunachokitengo cha Utafiti cha Baraza la Wawakilishi, kinajukumu la kufanya utafiti tuliokuwa hatukielewi na hatukitumii.

Tutawataka sasa watufanyie utafiti katika vitabu hivi juu ya matumizi haya ya fedha za walipa kodi. Mafungu yamekuwa mazito, matumizi yamekuwa mazito. Wafanye utafiti ili tujiridhishe juu ya mafungu haya yaliyorundikwa katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Elimu na wewe pia katika Wizara yako kuna mafungu ambavyo yamerundikwa yanahitaji kwa kweli tupate majibu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara yangu ambayo nimetokea kule nikaingia hapa, nakushukuru sana. Pia nimshukuru Waziri kwa kusoma bajeti yake mbele yetu.

Kabla ya hapo na mimi nitoe mkono wa rambi rambi kwa wole wote waliopatwa na msiba ambao niseme kwamba msiba huu umetugusa sote. Nasema kwamba jambo lolote likishakuandikwa basi Mwenyezi Mungu akikuandikia litakukuta. Kama mwenzangu alivyotoa aya hapa na mimi niseme vile vile *"Innamaa amruhu idha arada shay-an an-yaqula lahu kun fayakun fasubhana ladhii biyadihii malakutu kulli shay-in wailayhi turjauun"*.Kwa hivyo linalotaka kukufika Mwenyezimungu anasema *"kun fayakun".*

Niseme tu kama serikali itakuwa ina jukumu bado na ina mzigo mzito ili mambo haya ya matatizo ya vyombo vyetu hivi vya usafiri viweze kutafutiwa ufumbuzi wa haraka haraka ili tusipoteze, watoto wetu, ndugu zetu na jamaa zetu. Ni lazima serikali sasa hivi ichukulie nguvu zaidi pamoja na taasisi zote husika zitusaidie kuhusu jambo hili na hasa Mamlaka ya hali ya hewa. Kwa sababu kuna mambo mengine haya ni lazima kama Mamlaka nayo iwe inasaidia kwa hili.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende na ukurasa Nam. 34 ya hotuba hii ya Mhe. Waziri inayosema kuhusu madrasa na vyuo. Mhe. Waziri napenda kumuuliza atakapokuja hapa atwambie vyuo hivi ni vingapi na vimepata usajili na atuorodheshee pamoja na majiya yao. Hapa ametaja tu ni madrasa 2251 lakini hatuzijui Pemba ziko ngapi na Unguja ziko ngapi. Imesema kwa kipindi hichi idara haikuweza kuendesha mafunzo ya walimu.

Kwa hivyo ni matumaini yangu kwamba hapo baadaye atajiandaa vizuri ili tuwasaidie walimu wa hizi Madrasa kwasababu ni muhimu kwa jamii zetu hasa tukiwa waumini wa dini ya Kiislamu katika nchi yetu hii. Kwa hivyo ni lazima elimu hii tuipe kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, nikienda na ukurasa Nam. 37 Idara ya Elimu ya Sekondari. Mhe. Waziri ametwambia hapa kuna skuli 271 hizo skuli 220 ni za serikali na 51 za watu binafsi. Sasa sijui hizi skuli za watu binafsi kwa sababu wanajiendesha zaidi kibiashara sijui inazifatilia vipi kuhusu ufanisi wao wa kazi.

Hili vile vile nilikuwa naliomba Mhe. Waziri atwambie wanazifatilia vipi skuli hizi ili tunaona kwamba kuna uchakachuaji wa mambo ya mitihani na kwa sababu yanakwenda kibiashara inaweza ikawa ndio wale katika takwimu tunazozisikia kwamba watoto wanafika darasa la tisa lakini hawajui kusoma wala kuandika, wala kuhesabu. Hili pia kama serikali sijui inazifatilia vipi skuli hizi za watu binafsi.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa Nam. 55 kuhusu Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, kwanza niulize elimu hii ya amali, kwa sababu inawachukua vijana wetu, inawasaidia lakini baada ya kuwasaidia wanatoka pale baada ya kupata vyeti. Lakini bado kama serikali ilikuwa inajukumu la kuwasaidia hawa vijana, kuzingatia kwamba tumeshatumia nguvu kubwa na baadaye ikawa hakuna mafanikio. Watakuwa wanazurura zurura na baadaye kuingia katika mambo mbali mbali ya hatari ambayo wanaangukia tena kwenye madawa ya kulevya. Serikali ingewaweka pamoja hata kutafuta pengine kama wale seremalla wakawaweka kwenye vituo maalum ambavyo wataendeleza ile kazi yao.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa nambari 46 inasema Idara ya Elimu Mbadala kwenye fungu la 93 ambalo wanatumia vyombo hivi vya habari, tukizingatia kwamba jambo lolote au haki yoyote katika nchi yetu hii inamuhusu kila Mzanzibari. Nikizingatia kuna maeneo ya mbali kama vijijini mawasiliano yanakuwa hayafiki na kwa vile kila tunachokipata basi tugawane kwa sote. Ni tathmini gani iliyofanyika kuonesha kwamba ni watu wangapi wamefaidika kutokana na mpango huu.

Mhe. Naibu Spika, nende ukurasa Nam 55 wa bajeti hii ambayo Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Je, kwenye mafunzo haya pia nimuulize Mhe. Waziri kama nilivyotangulia kueleza kwamba kila kitu kinatuhusu iwe elimu au jambo jengine lolote linatuhusu sote tufaidike. Je, kwenye suala hili la walemavu kawasaidia vipi Mhe. Waziri. Kwa sababu hapa katika idadi hii ya jumla ya pamoja ni 730 kati ya 175 ni wanawake na 555 ni wanaume.

Sijui hapa katika mafungu haya maalum kama walemavu ni wangapi na wanawake ni wangapi na wangapi wanaume. Kwa sababu sasa hivi kama tunaridhia ile mikataba ya kimataifa ni kwamba kusiwe na mapungufu yoyote baina ya wanawake na wanaume kwa sababu tunakwenda katika *gender balance*. Kwa hivyo, ni lazima tujue wanawake wangapi na wanaume wangapi kuweko na *gender balance.* Sasa Mhe. Waziri atapokuja anieleze.

Nikiendelea nije kwenye suala la Chuo Kikuu cha Taifa ambacho kiko katika hii Taasisi ya TAKILUKI. Taasisi hii ni muhimu na kwa sababu inasomesha lugha, lakini hapa Mhe. Waziri ametuelezea tu jumla ya wageni 126 wanaume 30 na wanawake 96. Vile vile Chuo hiki nafikiri kinasomesha na hata watu wetu ndani ya nchi yetu, sasa hakutwambia hapa ni lugha ngapi ambazo zinasomeshwa au watu wetu wangapi ambao wanasoma katika chuo hiki au Taasisi hii ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa wa 73, kwanza nianze na ukurasa wa 71 ambako kuna kitengo hiki cha uhasibu. Kitengo cha uhasibu ni muhimu na kwa sababu na mimi ni fani yangu, hivyo napenda kusema kwamba kitengo hiki kinakuwa na kazi kubwa na pesa zote ambazo tunazipitisha hapa kwa usimamizi wa mwenyewe Katibu Mkuu na wao hapa napenda wamsaidie sana Katibu Mkuu kwa kufuata zile kanuni na sheria za matumizi ya fedha za umma. Pia zile *documents* zote ziwe zimekamilika na vile vile kuwe na *registers* zile. Nashukuru sana kwamba leo hapa nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya *PAC* na leo mjumbe mwenzangu mzito yupo hapa Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, kwa hivyo niseme kwamba tunatilia mkazo sana kuhusu utumiaji wa fedha za umma.

Pia nikipongeze sana Kitengo cha *PMU* na mimi nilikuwepo pale na nimeshuhudia namna kinavyofanya kazi na niwapongeze sana, ni lazima vitengo hivi viwili viwe vinafanya kazi sambamba.

Kitengo hiki kimesema kwamba kimetumia pesa hizo zilizotajwa kwa ujenzi wa Skuli za Ghorofa ikiwemo Skuli ya Kwamtipura. Kwanza hapa niseme kamba hii skuli sasa mimi na jirani yangu tutavutana sana, kwa sababu anasema hii skuli ni yake, lakini skuli hii ni yangu mimi na nasema nataka

kubadilisha jina sasa. Hii skuli inaitwa Skuli ya Kwamtipura lakini iko Jimbo la Amani. Kwa hivyo, nasema kwamba hii skuli Mhe. Naibu Spika, nataka kukwambia kwamba sasa nitaibadilisha jina.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo niseme kwamba, kwa niaba ya wananchi wangu walionichagua kwa kura nyingi wa Jimbo la Amani naunga mkono hoja.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa asubuhi hii ya kuchangia hotuba ambayo ni nuru ya dunia yetu. Leo hii sote hapa tuko siku ya pili ya maombolezo. Dini yetu ya Uislamu imeshapanga utaratibu katika suala hili na nafikiri wengi tunajua kwamba Mwenyezi Mungu katwambia kuwa '*Idhaa aswabat hum-muswibat*', basi huwa tunasema, '*qaalu, innalillahi wainna ilayhi raajiun*'.

Pia huko mbele akatwambia tena kwamba, '*lan yuswibana illa maakataba llahu lanaa*'. Kwa hiyo hayatotufika isipokuwa yale Mwenyezi Mungu ametupangia. Lakini mwisho akasema tuwe na subira kwa sababu subira ndio msingi wa kuingia peponi. Mwenyezi Mungu tumuombe atupe subira hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitokuwa na mengi sana leo isipokuwa nitasema kidogo tu. Mhe. Ali Mzee Ali juzi alipokuwa anachangia Hotuba ya Wizara ya Katiba na Sheria aliturejesha nyuma sana, na alitupangia historia kiasi kwamba ilituvutia sana, na kila alichokisema kwa kupitia ile njia ya historia kilitushawishi pakubwa sana. Sasa nikaona labda leo na mimi nikipata fursa niseme kidogo na niulize.

Kwa sababu ninachohisi kwamba somo la historia katika nchi yetu limesahaulika, na ninavyohisi tunaingia katika jumuia tofauti hivi sasa, tunaingia katika Jumuia za Afrika Mashariki, Jumuia za Afrika Mashariki na Kusini, jambo ambalo tunahitajika tuelewe hawa tunaotaka kuungana nao wakoje na sisi wenyewe tukoje, bila ya kujua unakotoka huwezi kujenga msingi mzuri wa unakokwenda. Sasa je, niulize labda hili somo la historia hivi sasa limesahaulika moja kwa moja halimo katika skuli au limo lakini limo katika ngazi ya juu.

Mhe. Naibu Spika, niondoke hapo nije katika suala la vyeti. Hivi sasa tuna utaratibu katika nchi yetu kwamba somo la ngazi ya cheti hasa kwa walimu hatuna tumeliondosha moja kwa moja, tumeanza na ngazi ya *diploma* tukienda na mbele. Sasa sijui niulize tena hapa je, tumeshafikia hali ya kuwa hatuna umuhimu tena wa kuwa na wale walimu ambao watakuwa na ngazi za cheti.

Lakini jengine sijui kwa sababu mara nyingi katika nchi zetu hizi huwa sisi tuna-*imitate* au tunaiga kutoka nchi ambazo zinaendelea, na wao wanakuja na *policy* zao na kutuingizia katika mitaala yetu. Sasa sijui tumeiga nchi gani utaratibu huu kwamba wao hawana vyeti na sisi ikabidi tuige au tumeshafikia hatua ya kwamba labda wanafunzi walioko chumba cha saba baada ya miaka miwili ijayo pengine tutakuwa na walimu wa *diploma* na wengineo. Sasa labda ningepata maelekezo kama hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumbukumbu zangu katika miaka ya 1980 kuanzia 1977 tulianzisha vyuo, kwa maoni yangu mimi ni kwamba hizi zilikuwa ni *centre of excellences*, kwamba wanafunzi waliokuwa wanapelekwa pale walikuwa wako katika kiwango na wanafunzi waliokuwa wanatoka pale pia walikuwa wako katika kiwango. Tulikuwa tuna vyuo vyetu vya Nkrumah, Fidel Castro, Lumumba pamoja na Karume. Leo nathubutu kusema kwamba mainjinia wengi tulionao walianzia aidha pale wakenda masomoni baadae, watu walioko katika mambo ya uvuvi wengi wamepitia chuo cha Lumumba, na sisi wengine wa Fidel Castro tukapata elimu ya kilimo.

Lakini leo vyuo vile Mhe. Naibu Spika, nahisi kama sio vyuo tena ni skuli tu za kawaida, mtu anakwenda Lumumba au Karume ni kama anakwenda skuli tu, hakuna ile *quality* ya kwamba hapa labda tunampeleka kijana akitoka ataweza kujitegemea. Sasa sijui Wizara imeliona hilo na labda katika miaka tunayokwenda itavipa kipaumbele gani ili kuondokana na wale wataalamu wa mambo ya uvuvi na ma-*engineer* katika meli zetu ambazo kila siku zinazima *engine* njiani.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kidogo katika suala la Baraza la Upimaji na Tathmini. Imekuwa hivi sasa ni kawaida Mhe. Naibu Spika, kwamba tuna mitihani tofauti tofauti, kuna wakati ambapo baada ya kufanya mitihani hii huwa tunateua wanafunzi, na wanafunzi hawa tunawaita wana vipaji maalum. Sasa mimi Mhe. Waziri ningependa anisaidie jambo moja kwamba, mfano unaisikia skuli moja ya Utaani au ya Bopwe inatoa wanafunzi karibu mia moja au kuanzia thamanini kwenda mia moja, wote hawa unaambiwa wana vipaji maalum, na wanakwenda katika skuli moja, mkoa mzima pengine wa Kusini Pemba umetoa wanafunzi 15 au 20, sasa sijui ule uwezo wao wa ufahamu unapimwa kwa njia gani. Je, ule mtihani tunaoufanya kwa ajili ya kutoa wanafunzi wale ni kweli unatosheleza kumpima mwanafunzi kwamba yule kweli ana uwezo, kiasi kwamba skuli moja itoe wanafunzi wengi kuliko Mkoa mzima ambao pengine utakuwa una wanafunzi zaidi ya 500 au 600 waliofanya mtihani kama ule.

Labda hapa Mhe. Waziri angelinisaidia suala kama hili nikapata kujua je ile mitihani ina uwezo wa kumpima mtu uwezo wake au ni mitihani imefanywa

kwa bahati katika kipindi kile mwanafunzi amebahatika kusomeshwa somo lile na ameshinda kwenye mtihani.

Lakini katika hili Mhe. Naibu Spika, hivi sasa nikiangalia kiwango cha elimu katika nchi yetu ukilinganisha na nchi nyengine kiko chini, katika kufuatilia nimegundua kwamba jirani zetu wa Kenya wamo katika mpango wa kuangalia na kutathmini elimu yao ilivyo. Hata nchi ya Uingereza vile vile wako na hoja mbele ya Baraza kuangalia je, jinsi gani watakavyoboresha mfumo wao wa elimu. Sasa kila nikiangalia nahisi kwamba nchi hizi tukilinganisha na sisi basi wao kiwango chao kiko juu, sisi kiwango chetu kiko chini. Sasa sijui kwa miaka kumi ya mfumo huu au zaidi tunaokwenda nao, je tumetosheka na mfumo uliopo kwamba huu unatuwekea *quality* fulani au una mwelekeo labda baadae baada ya kufanya *evaluation* tukaona kwamba na sisi hivi sasa tuna umuhimu wa kubadilisha mfumo wetu angalau kidogo uweze kwenda na hawa wenzetu tulio jirani nao. Kwa sababu pengine tunataka kuingia katika hiyo Jumuia ya Afrika Mashariki na baadae pengine Jumuia kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kidogo katika Afisa Elimu Mkoa, Afisa Elimu Wilaya. Mimi napata matatizo kidogo kwa sababu kiutaratibu *pyramid* ya Wizara ya Elimu kuna Ofisi ya Elimu Wilaya na Ofisi ya Elimu Mkoa, lakini nashangaa kwamba mpaka hivi sasa watu hawa hawajielewi, nasikia kuna Ofisa wa Elimu Mkoa lakini hana madukhuli au hana senti yoyote ya uendeshaji wa ile ofisi, na Ofisa Elimu Wilaya nae pia hana fungu lolote linalomuwezesha yeye kuendesha ile Idara, akienda Wizara ya Elimu anaambiwa aa, wewe uko Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, akienda Ofisi ya Mkuu wa Mkoa anaambiwa nyinyi ni watu wa elimu, sasa hawa ndio wanaoratibu shughuli zote za elimu za mikoa na wilaya, lakini hawana fungu lolote linalooneshwa zaidi ya ule mshahara. Sasa ikiwa kwamba wao ndio wanaoratibu shughuli hizi, je hizo shughuli za elimu zitafanyika kama wao hawana fungu lolote.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa wamewekwa katika mfumo kama huo kwamba wao hawana utaratibu wowote ule, kuna haja labda yoyote ile ya kuwa sisi hivi sasa tukawa tuna Ofisi ya Elimu Wilaya au Mkoa, labda tusingekuwa na Ofisi ya Elimu Wilaya na Mkoa nao tukausamehe ili tukarahisisha kwa sababu ule umuhimu wenyewe hasa haupo.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende kidogo katika suala la *tuition*. Wengi hapa wamezungumza *tuition*, lakini wao wamekwenda katika suala la upatikanaji wa ujauzito na mengineyo. Mimi Mhe. Naibu Spika, nataka nilizungumzie katika upande mwengine, hivi sasa ukiangalia kila kona katika mji wetu utasikia kuna mwalimu ameweka *tuition*, kuna mtu anasomesha *tuition*, sasa

kinachonisumbua ni kwamba mara nyengine unakuta yule mwalimu ambaye anasomesha somo la Kiingereza skuli ndiye mwalimu yuke yule ambaye amewaita wale wanafunzi kwenda jioni kuwasaidia katika lile somo fulani hivi. Sasa najiuliza ni kwamba wale walimu wamewaona wanafunzi wao kwamba muda ni mchache kuwa hautoshi katika vipindi walivyowekewa au wale wanafunzi hawaelewi ufahamu wao ni mdogo.

Hili ningependa Wizara waliangalie kwamba ikiwa kuna *tuition* je, hizi *tuition* wanaziratibu, kwamba yule mwalimu ambaye anasomesha ile *tuition* ana kiwango kinachofikiwa. Kwa sababu wakati mwengine unakwenda unakuta mwalimu ambaye anamsomesha mwanafunzi anayetaka kujiandaa kwa mtihani wa *Form VI* yeye hajafikia hata ile *Form VI* yenyewe, lakini kwa sababu anatembeza watalii huko nje ana ile fursa ya kuzungumza kile Kiingereza sasa yule unamkuta ndiye anayewasomesha somo la Kiingereza. Kwa maana hiyo unakuta sasa ule ufahamu wake kwa vile na yeye hakupitia somo la ualimu kwa sababu kuna *method* na mengineyo ambayo anatakiwa ayajue, unakuta sasa aa wanafunzi wetu wameonewa katika mitihani yao na mengineyo.

Sasa mimi ningependa Wizara ikawa na utaratibu maalum, wale ambao wanaweka *tuition* basi wakajulikana huyu ni mwalimu, na yeye kama ni mwalimu kweli kasomea na ana sifa kama hizi. Kuna wengine huko unakuta anasomesha *biology* lakini yeye ni mwalimu ambaye anasomesha *art* akiweko darasani, lakini sasa kwa vile tumekiweka kitengo hiki kama ni *business* basi anaweka tu, anasema na mimi nasomesha *tuition* nina wanafunzi, *lahaula wala kuwatta*, hawana wanachokijua wakisikia mwalimu fulani anasomesha *tuition* basi wanakwenda, matokeo yake mzazi sasa unakuta kalipia mwanawe kusoma *tuition*, matokeo yakija aa tumefutiwa matokeo kwa sababu fulani fulani. Sasa mimi nahisi Wizara hivi sasa ishafika wakati wale ambao wanaandaa *tuition* na wao wakawafanyia *evaluation* wakawatafuta wakajua ni nani na kwa nini anafanya somo fulani.

Lakini nijiulize tena katika hilo, kama ni muda ambao hautoshelezi au ni uelewa wa wanafunzi darasani hata tufike hadi kwamba kila kona hivi sasa kuna *tuition* ambazo zinatupeleka katika hayo ambayo wengine wameyasema.

Mhe. Naibu Spika, labda mwisho nimalizie kwamba, nimesikitishwa sana na kitendo cha mwalimu mmoja kama miaka miwili iliyopita, huyu alikuweko katika Skuli ya Tumbe. Mwalimu huyu alimpa ujauzito mwanafunzi wake wa kike akakimbia, lakini alipokimbia hivi karibuni karejea sijui kama alikimbia au alijificha katika mazingira ambayo alikuwa haonekani, lakini bado kapewa uajiri tena na lililofanyika ni kwamba kaondoshwa katika sehemu ile kapelekwa skuli nyengine yamemalizika. Sasa sijui huo ndio utaratibu uliopo

katika serikali yetu na wizara zetu kwa jumla au kuna utaratibu maalum wa walimu ambao wanafika kufanya matendo kama hayo.

Mhe. Naibu Spika, naona muda wako nisiuchukue sana naunga mkono hoja.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nichukue nafasi hii kutoa pole kwa wale wote ambao wamefiwa na wale ambao wamefikwa na majanga ambayo yametutokezea hivi juzi. Namuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira.

Lakini pia nichukue nafasi hii niipongeze sana Wizara hii ya Elimu kwa sababu ndio wizara mama miongoni mwetu, kwa kweli ni wizara ambayo ndiyo iliyotufanyia kila kitu na tukaweza kuingia katika Baraza lako hili tukufu japo elimu yenyewe ya chini ya miembe.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwa kweli nimuombee dua Marehemu Abeid Amani Karume ambaye baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 alitoa baadhi ya mambo bure bila ya malipo, moja wapo ikiwemo elimu. Lakini kutokana na mambo ya kutoka nyuma na hivi sasa kwa sababu sasa tumezidi ki-*population* haiwezekani wazee lazima watusaidie baadhi ya mambo na si kosa.

Lakini mimi nasikitishwa sana Mhe. Naibu Spika, na hili nilisema nilitafutie pahala na pahala pake ni hapa, leo tunathubutu kumtukana mjane wa marehemu Karume ambaye ni miongoni mwa mmoja wapo aliyetusaidia kwa namna moja au nyengine, haidhuru ni mikutano ya huko lakini sisi wengine inatuuma, sheria na huruma Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli mimi sikufurahishwa na mkutano uliofanywa akachambuliwa mke wa Marehemu Karume, ni makosa makubwa sana kwa sababu Mwenyezi Mungu kamchukua mumewe lakini yeye tunae kwa jambo ambalo ni demokrasi, nilisema hapa ndio pahala pa kusema. Jambo ambalo mtu yoyote ni demokrasi kwake aidha atake Muungano wasitake muachie aseme nafasi ambayo anaihisi yeye Mhe. Naibu Spika, sio umuingilie halafu matusi yenyewe si matusi ya kisiasa ni matusi mabayamabaya. Si jambo la busara wakati yeye ndiye aliyetuletea uhuru hapa tukaweza kujitawala, kwa hivyo lazima staha iwepo. Nilisema hilo nilizungumze na nalizungumza kwa uchungu sana Mhe. Naibu Spika.

Nikija katika wizara hii na mimi niungane mkono na wenzangu kwamba *tuition* kwa kweli zinatuharibia. Tuwe makini wizara watoto wetu sasa hivi pamoja na utandawazi ulioko hiyo ndiyo inayoleta sababu ya kutuharibia watoto wetu. Lakini si hilo tu Mhe. Naibu Spika, mimi nilipokuwa Wizara ya Wanawake na Watoto katika kuchangia kwangu nilisema hivyo kuna sababu

ipi ambayo kama hatukurejesha mambo mazuri ya nyuma, kwa nini watoto wetu waonekane saa mbili za usiku mpaka saa nne au tano wao wanaranda tu ovyo, lazima kuwe na utaratibu na tutunge sheria kwa sababu watoto wetu wameanza kuharibika mtoto wa miaka sita, saba, nane anakuwa mvuta bangi na unga, watoto wa kike na wa kiume Mhe. Naibu Spika.

Kwa sababu sasa hivi tukitaka tusitake wazee tunachangia, tunachangia watoto wetu kufanya yote ambayo ni kinyume na utaratibu wa kitoto. Na sisi Mhe. Naibu Spika, tulikuwa watoto kazi yetu ilikuwa nage, kifuu na mchanga, mengine yalikuwa hayakuwepo, lakini leo watoto wa miaka mitano na sita mambo wanayoyafanya Mhe. Naibu Spika, ameyazungumza Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak hapa ni aibu kusema katika kikao hiki. Watoto wa miaka sita na saba ambao wako darasa la kwanza na la pili jamani wizara hii iwe makini na vijana wetu, leo sisi hatuna vijana ambao tutasema tunaringia Mhe. Naibu Spika, watoto wamejiingiza katika mambo ambayo kwa kweli ni kinyume na utaratibu na silka na mila zetu Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, kama hatukuwa makini basi taifa hili litapoteza mawaziri wazuri, marais wazuri, madaktari wazuri, litapoteza aina mbali mbali ya fani. Mhe. Naibu Spika, na sisi tunachangia wakati mwengine, kwa sababu tunasema kwa nini wizara haiandai kila mtu na kipaji chake akajulikanwa, uwezo huo upo na wenzetu ndivyo wanavyofanya tubadilike. Unamhisi mtoto huyu kipaji chake kinampa atakuwa *artist* mzuri basi watafute na ma *artist* wenyewe umpe kipaji chake kile, lakini leo tunamangamanga wanafunzi wetu sayansi hawapasi vizuri kwa nini? Ni kwa sababu hatutoi kipaumbele na walimu wa sayansi hatuna wengi namna hiyo.

Mhe. Naibu Spika, naiomba sana Wizara ikae itafakari baadhi ya mambo itizame upya katika wizara hii, ili kuhakikisha kusonga mbele sio tubakie hapa hapa tu na hii ni wizara mama kama nilivyosema mwanzo, ni wizara ambayo ikikubali inawezekana kwa sababu ndio wizara inayotoa mawaziri, marais, inatoa kila fani. Sasa mimi sielewi kwa nini hawawezi kujipanga na wataalamu wanasomesha wao na wao wenyewe ni wataalamu. Naiomba sana wizara kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, ikae itafakari, ipange mipango yake ambayo itaweza kusukuma.

Lakini nije kwa baadhi ya mambo. Mhe. Naibu Spika, tunajua kwamba wizara hii ni wizara ngumu, ni wizara ambayo kwa kweli haimithiliki katika wizara nyengine kwa sababu hizo wizara nyengine zisingezaliwa kama si wizara hii kutokana na wasomi ambao wanasomeshwa na wizara hii. Lakini la kushangaza Mheshimiwa kwamba kuna vyeti feki vya watoto wetu wanapomaliza masomo. Hayo siyasemi kwa kubahatisha, mwenzangu Mhe. Salmin Awadh Salmin amezungumza sasa hivi kusema kuna Kamati ya

Utafiti ya Baraza la Wawakilishi kitengo cha kamati hiyo. Na mimi nasema kwa utafiti nilioufanya kwamba iwe makini Wizara ya Elimu vyeti feki vipo, cha *Form IV, Form VI, Form II, Form I,* yanatokea tokeaje haya, wajiulize yanatokeaje haya. Naomba iwe makini sana katika mambo hayo.

Kwa sababu unayempenda Mhe. Naibu Spika unataka afanikiwe, usimfanyie magubegube kwa sababu ni jamaa yako, ndugu yako, mpenzi wako ukampa cheti cha kughushi ni makosa makubwa sana na wala humsaidii, unakwenda baadae unamuadhirisha.

Mhe. Naibu Spika, nije katika walimu. Huko nyuma nilipokuwa nikisoma mimi ilikuwa tunawatetemekea walimu, kuku akizaa kwenu unaficha mayai unampelekea mwalimu, ukiona kitu kizuri unakificha unampelekea mwalimu, jamani katika nchi mwalimu ni mtu muhimu sana, ni mtu ambaye anatakiwa apewe hali na mali ili kuhakikisha akili yake ina-*concentrate* na anaowafundisha. Sio dakika kumi anasomesha pale anaandika juu ya ubao dakika 15 anatoka anakwenda kutafuta kula. Hapo bado hujamsaidia mwalimu na mimi natilia mkazo kuhusu habari ya walimu.

Mhe. Naibu Spika, naiomba sana wizara kama nyuma huko tulikuwa tunawa-*push* lakini naona hapa katikati tumejisahau, na wizara hii inapata fedha nyingi sana zisipotee tu katika mambo ya mipango na maendeleo huko na katika utawala zifanye kazi yake walimu wapewe hadhi yao na lile posho la shilingi 15,000 si shilingi 15,000 kuna wengine wanapata shilingi 7,000, wengine 5,000. Mimi nashangaa wakati huu unampa mwalimu posho la shilingi 5,000.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba sana mimi sitaki nizungumze sana kwa sababu ni wizara ambayo imenipa taaluma mpaka nikafika humu, lakini akupendae anakwambia na mimi nilisema nizungumze hayo kwa sababu ni wizara yangu, ni wizara mama naipenda, mimi baada ya kumaliza masomo tu nilifanya kazi Wizara ya Elimu na nikapata mafunzo mengi sana, Marehemu Juma Jongo ndiye aliyenisomesha mambo ya *administration,* kwa hivyo ninawataka wenzangu tukae tuwasaidie mawaziri wetu ili kuhakikisha wizara hii haituhumiwi kwa mambo mengine.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii, maana isingekuwa vyema kama sikutoa niliyonayo katika wizara hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumepata wachangiaji kumi asubuhi, lakini wamebakia kumi na tatu, kwa hivyo naomba wale wote ambao hatukuwaita asubuhi waje mapema jioni tunachelewa sana, tuje mapema ili

tuweze kuchangia wale waliosalia. Baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao chetu hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi alau niweze kuchangia mawili matatu yatokanayo na bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kabla sijafanya hivyo, basi naomba nianze kwa kutoa mkono wa pole kwa wale waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki katika msiba huu uliolikumba taifa tangu juzi. Kwa hivyo kwa niaba yangu binafsi na wananchi katika Jimbo la Chake-Chake naomba nitoe mkono wa pole kwa wote waliopoteza wapendwa wao, na tumuombe Mwenyezi Mungu roho zao aziweke mahali pema peponi, na wale ambao wamepoteza basi Mwenyezi Mungu awajalie subra na wale waliokuwa majeruhi Mwenyezi Mungu awape nafuu ili wapone haraka.

Katika hilo Mhe. Mwenyekiti, turudie lugha na kauli yetu ya kila siku kwamba mambo haya sasa yanaonekana ni mambo ya kawaida, na kama ni Wawakilishi wa wananchi tuendelee kutoa wito kwamba wote wale waliowajibika, maana yake sisi kazi yetu kubwa ni kusema tu na tutaendelea kusema, maadam yanaendelea kutokea na wanaoathirika ni wananchi waliokuwa hawana hatia, kwa hivyo tutaendelea kulizungumza hili hadi pale siku moja ambapo Mwenyezi Mungu akawatia *taufiq* hawa viongozi wetu na kulifanyia kazi suala hili. Kwa hivyo ninatoa wito kwa serikali kuwachukulia hatua wale wote waliohusika katika hili na wa pande zote mbili, ama iwe wa upande wa Dar es Salaam au upande wa Zanzibar. Lakini hatuwezi tukaziona roho changa, roho mbichi zikiteketea pasi na hatia yoyote ile, ya Mwenyezi Mungu tumuachie Mwenyezi Mungu lakini yale yaliyoekewa mkono wa binadamu ni lazima yachukuliwe hatua Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Katika hilo naomba nieleze tena kwamba kwa kuwa yanaonekana majanga yanatokea na yanawakumba wananchi wetu kila siku, na kwa kuwa sasa tunajadili bajeti ya Wizara ya Elimu, naomba hili somo la uokozi, suala linalohusiana na uokozi sasa litiwe katika mitaala ya elimu ili vijana tangu wakiwa wadogo wajue namna ya kujiokoa kwa sababu suala la usafiri baina ya visiwa; usafiri baina ya Pemba na Unguja, baina ya visiwa viliomo ndani ya visiwa viliomo baina ya Pemba na Ungaja, baina ya Zanzibar na Tanzania

Bara ndio maisha yetu ya kila siku. Kwa kuwa inaonekana sasa suala hili linakuwa ni zito kupatiwa ufumbuzi, naomba kuandaliwe mtaala maalum kwa wanafunzi kuanzia darasa la kwanza wajue namna ya kujiokoa Mhe. Mwenyekiti, pindi itakapotokea majanga kama haya kwa mara nyengine. (*Makofi*).

Sasa baada ya kuelezea haya yatokanayo na msiba uliotukumba, naomba moja kwa moja niende kwenye bajeti husika. Naomba nigusie kwamba bajeti ya Wizara ya Elimu, fedha hizi tunazozitenga kwa ajili ya shughuli za Wizara hii kwa mwaka huu 2012/13, ni muhimu zigawike katika maeneo makuu mawili kama haya yafuatayo.

Bajeti lazima iangalie mfumo wa elimu, lakini bajeti ni lazima iende kwenye maendeleo ya elimu. Tunaposema Mhe. Mwenyekiti, mfumo wa elimu tunamaanisha mwanafunzi pamoja na mwalimu wake, elimu inaanza hapo kwenye mwanafunzi pamoja na mwalimu wake. Bajeti lazima imguse mwanafunzi na mwalimu wake, lakini bajeti lazima igusie kwenye ujenzi wa madarasa pamoja na ujenzi wa vyumba vya maabara.

Bajeti halikadhalika igusie kulenga kwenye vifaa vya kusomeshea pamoja na kujifunzia, pamoja na huduma zinazotokana na elimu. Bajeti ni lazima izungumzie kwenye masuala ya mitihani kwa sababu kipimo cha elimu ni mitihani kwa kila ngazi, kwa hivyo lazima bajeti iguse kwenye mitihani. Lakini bajeti lazima iguse kwenye shughuli za utawala.

Sasa tunapoziangalia hizi fedha zinazoombwa ambazo ni bilioni sabini na moja kwa kazi za kawaida. Ni lazima tuzione bilioni sabini na moja zikichawanyika katika maeneo haya. Kuanzia suala la mwanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, kila mwaka wanafunzi wanajiunga katika skuli, na kila mwaka wanafunzi wanamaliza skuli. Tunashukuru kwamba *enrollment* katika skuli zetu zote ni asilimia 100, hilo tunalishukuru kwamba tumefika katika kiwango hicho cha kuwapokea watoto kila mwaka. Hilo ingawa lina changamoto zake lakini kwa hilo tunasema tunashukuru.

Lakini bajeti vile vile ni lazima ilenge namna ya kuwahudumia walimu, kwa maana ya mishahara, maslahi pamoja na mafunzo. Tumeendelea kuona kwamba maslahi ya walimu bado yanakuwa ni duni. Kitu ambacho kwa namna yoyote ile kinapunguza morali ya walimu wetu kusomesha, kwa sababu mbali ya mshahara wao wanaoupata lakini walimu hao hao kuna michango isiyopungua mitano walimu kila kipindi hutozwa. Sijui kuna mchango wa siku ya walimu duniani, kuna michango mingi ambayo mshahara

ule ule ambao mwalimu anautegemea. Kwa hivyo maslahi ya walimu yanaendelea kuwa ni duni.

Lakini vile vile mwalimu ili awe mwalimu lazima apate mafunzo ya mara kwa mara ya ndani ya nchi na nje ya nchi. Lazima apate vijikozi ambavyo vinaweza kumuendeleza katika fani yake mara kwa mara. Kitu ambacho kwa kweli hivi sasa hata ukiona *training* zinafanywa basi ni tabaka fulani tu katika ngazi ya Wizara ya Elimu, lakini mwalimu hasa yule aliyepo kijijini anayekamata chaki, yule utamuuliza mwaka mzima hajafika hata hapa Unguja kupata angalau *training* angalau na yeye akapata kijisoda.

Lakini jengine tumeshuhudia kwamba madarasa na maabara, hili asilimia kubwa sana linachukuliwa na wananchi, wananchi ndio wenye dhima wanaolishughulikia suala hili. Vifaa vya kusomeshea, kujifunzia na huduma za wanafunzi Mhe. Mwenyekiti, hili linabebwa na wazazi wenyewe.

Halikadhalika suala la mitihani, sisi Wawakilishi wako ni mashahidi kwamba ukiacha mbali mitihani ya juu, lakini hii mitihani inayowadahili wanafunzi katika ngazi za chini takriban wadau kama vile Wabunge, Wawakilishi pamoja na wengine ndio wanaolishughulikia suala hili la mitihani.

Sasa tunapata kuona kwamba asilimia kubwa ya bilioni sabini na moja zinamalizia kwenye shughuli za utawala tu, hazifiki kule ambako zimekusudiwa katika suala zima la kuimarisha elimu. Katika hili Mhe. Mwenyekiti, naomba kuna utafiti mdogo ambao nimeufanya hapa.

Mathalani fungu 0401 linalohusiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Vifaa vya uchapaji, sikulichukua fungu lote kwa maana ya *items* zote, kuna *items* kama sita nimezichukua na naomba nizirudie kama zinavyofuata.

Vifaa vya uchapaji vimetoka kwenye shilingi milioni nane hadi kwenye milioni arobaini na moja. Mwaka jana walituletea shilingi milioni nane ambapo mwaka huu wameomba milioni arobaini na moja kwa vifaa vya uchapaji.

Sasa sijui kama ni vifaa vya uchapaji vya aina gani. Hapa Mhe. Waziri atakapokuja naomba anieleze kwa sababu mwaka jana, hizi shilingi milioni nane kwa Idara moja tu, hii milioni nane ya mwaka jana ilitolewa au haikutolewa, lakini kama ilitolewa kwa nini mara hii waombe shilingi milioni arobaini na moja, kuna kitu gani.

Kuna vyakula, vinywaji na viburudishaji vimetoka milioni mbili hadi ishirini na tano. Maana yake mara hii wanataka kuburudika na kunywa sana. Safari za

ndani milioni tatu hadi kumi na tatu, safari za nje milioni tatu hadi ishirini na nne. Ununuzi wa samani ni milioni thamanini hadi mia tisa na thamanini na saba. Mwaka jana ni milioni thamanini mpaka milioni mia tisa na thamanini na saba.

Lakini kuna suala la ushauri nasaha kwa wanafunzi, wametoka shilingi milioni sitini na tano hadi milioni mia mbili na ishirini. Mwaka jana kwa ujumla katika vifungu hivi vinatembea *around figure* tisini na tano milioni, lakini imekuja mwaka huu bilioni moja, sitini na saba milioni. Hapo pana ongezeko la asilimia tisa.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi hii sikubali kwa sababu kuweza kuyachanganua haya na ukaelezea sababu hasa ya kupanda mpaka maana yake mahitaji yakawa ni halisi, zikaongezeka katika kiwango hiki, kwa kweli hii haikubaliki. Mimi ninadhani kwa fedha hizi zilizoongezeka basi zipelekwe tu katika mafungu mengine ambayo yanakuwa na umuhimu zaidi. Hatuwezi tukaidhinisha fedha katika kiwango hiki, maana yake leo tunapoambiwa ununuzi wa samani, Mhe. Waziri atakapokuja atwambie hizi ni samani gani, ni samani za ile Idara yenyewe au ni samani zile zinazozungumzwa na Waziri wa Fedha kuchukua madeski tukenda tukayapeleka kwa wanafunzi. Maana yake ikiwa ni samani za skuli basi hilo tayari serikali imeandaa mpango wake wa namna gani skuli zetu zitapata madeski, hilo tumeliandalia utaratibu.

Lakini ikiwa samani zinazohusiana na Idara, yaani vikalio. Sisi kwa kadri tunavyoijua kama Wizara ya Elimu hivi sasa ina vikalio vya kutosha, na hata kama kuna upungufu si upungufu wa kutosha kwenye shilingi milioni thamanini mpaka kwenye milioni mia tisa na thamanini na saba. Hii haikubaliki.

Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja ninadhani aje atueleze hili ili vyengine basi mimi nitashauri wenzangu bajeti ile ile ya bajeti ya mwaka jana tuweze kuipitisha bajeti ile ile ya mwaka jana, ni thamanini tu zinatosha kwa sababu kuna matatizo makubwa zaidi ambayo yanahitaji fedha katika Wizara ya Elimu kuliko hata hayo mambo mengine kwa kweli. Kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja naomba hili aje anielezee kutokana na fungu hili la 0401.

Lakini vile vile mbali ya Idara moja moja, nilifanya utafiti mdogo unaohusiana na ongezeko la baadhi ya vifungu na nilikwenda kwenye chakula na vinywaji, lakini vile vile nikaingia kwenye safari za ndani na safari za nje. Kwenye chakula, vinywaji na viburudishaji Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa mwaka jana *round figure* ilikuwa kama tisini na nne milioni kwa chakula na vinywaji.

Lakini mara hii ni zaidi ya milioni mia mbili na ishirini na moja, ikiwa ni ongezeko la hamsini na tisa. Sasa mimi ninashauri wakubwa kama hamli nyumbani murudi tena kula nyumbani, lakini hatuwezi tukaorodhesha tena pesa kama hizi.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti zinazokuja zinazidi kutupa uchungu kwa sababu kila pahala ambapo panazidi fedha hizi ambazo hazina maelezo kwa kweli sisi tutazikataa. Tunahitaji tupate meli na vifaa vya kuokolea. Hatutoruhusu tena kutumia fedha ambazo kwa kweli hazina maelezo.

Kwa hivyo wazee katika maofisi kama ikiwa kamati zikija kule ni lazima muzipe chakula na nini, maji ya kunywa yanatosha, kila mtu aende akila kwake. Lakini pesa hizi tisini na nne na milioni za mwaka jana tutaendelea na mwaka huu, tutaendelea kuwapa tisini na nne milioni. Hizi nyengine peleka sehemu nyengine ambako kuna mahitaji muhimu zaidi.

Safari za ndani ni tisini na tisa milioni mwaka jana lakini mara hii ni mia mbili na hamsini na tisa milioni. Munakwenda pahala gani? Hii kwenda kila pahala Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi tu kutumia pesa namna hii kwamba kila siku watu wafikirie namna ya kutembea tu. Hebu watu mutulie maofisini mufanye kazi. Wenzangu asubuhi aliwaambia siku hizi dunia ya sasa ni dunia ya mtandao, ukifungua mtandao unaweza uka-*apply* chochote na unaweza ukaona chochote duniani unachokihitaji. Kwenda kule ni kwa mambo ya lazima tu, sijui kwenda kutiliana saini na vitu vyengine. Lakini tunasema kwamba watendaji tunataka mubakie maofisini ili wapunguze safari hizi, na ili mutulie maofisini maana yake lazima sasa mubakie mutufanyie kazi zetu hizi.

Jengine ukiachia mbali hilo ambalo naomba Mhe. Waziri atakapokuja atupe maelezo ya fedha hizi zilizoongezeka, lakini kama ikiwa hatukuridhika kwa kweli tutamuidhinishia zile zile za mwaka jana, abakie na zile zile ili fedha hizi ili tuzilenge kwenye sehemu ambazo zinahitajika. Wazazi wetu hivi sasa wanapata taabu sana, maana yake mzazi anampeleka mtoto skuli akachukia yule mtoto, kila siku kuna mchango huu, kuna mchango wa fagio. Sasa tunasema *enough is enough.*

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, kuna taasisi ambazo zinapokea ruzuku lakini bahati mbaya kwamba taasisi hizi zinazopokea ruzuku, hakuna uchanganuzi wake. Tunahitaji vile vile uchanganuzi wa hizi taasisi ambazo zinapokea ruzuku.

Mathalani Chuo cha Kiislamu ni thalathini milioni Pemba na Unguja ni milioni thalathini. Taasisi ya Karume walitoka kwenye milioni mia moja hadi

milioni mia tatu na hamsini na tano. Chuo cha Benjamin Mkapa milioni thalathini, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali milioni mia tatu mpaka milioni mia nane hamsini na tatu, sisi hatuna ugomvi wa kuidhinisha fedha hizi lakini haja yetu ni kupata uchanganuzi. Kwa sababu mbali ya fedha lakini tunahitaji fedha hizi zinakwenda pahala, kwa sababu lazima baadae iwe ni rahisi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuweza kuzifuatilia fedha kama hizi.

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu bilioni nne hadi bilioni nane, na hapa kidogo tutakuwa na mashaka, kwa sababu kuna fedha zile ambazo serikali zimekopeshwa na leo katika bajeti hii tutahitaji tupate jawabu kamili. Tutahitaji wapi bilioni nane za mwaka jana zile fedha tulizozidai tunahitaji tuzipate ili tuweze kuziidhinisha, muweze kujenga hoja ili tuweze tuziidhinisha hizi nyengine.

Baraza la Upimaji na Tathmini elfu moja mia tatu na thamanini na tatu milioni hadi elfu moja mia tano, Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu thamanini hadi tisini, na Taasisi ya Elimu ni hamsini na nne hadi sabini na mbili. Kwa hivyo hoja hapa ninakuomba Mhe. Waziri utakapokuja haja yetu pamoja na kupata mafungu ya jumla kwamba ni ruzuku, lakini tunachohitaji sasa ni ufafanuzi wa ruzuku hizi tunazokwenda nazo.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba niingie kwenye suala zima la uvujaji wa mitihani. Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo hili la uvujaji wa mitihani kitu ambacho ninasema sasa kwamba wakati umefika tuweze kuzifanyia kazi hoja hizi na serikali iwe na majibu. Kwa sababu suala la uvujaji wa mitihani lina athari kubwa sana katika jamii yetu.

Mimi siamini tu kwamba ni mambo ya kawaida, ninaamini kuwa kutakuwa na mikono ya watu, ama mifumo hii tunayoitumia siyo au kutakuwa na namna yoyote ile ambayo inapelekea mitihani yetu hii iweze kuvuja, na hivyo kwa kweli kupoteza kiwango cha elimu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kiwango chetu cha elimu ni kibovu. Siku zote tunazungumzia elimu yetu Zanzibar na Tanzania kwa jumla haijawa, bado ni mbovu ipo chini sana. Hatuwezi kujinasibu kwa hilo. Mimi hivi karibuni kuna kijana nilimpeleka Kenya kule, ni kijana wa darasa la sita basi katika kujiunga akaambiwa bwana wee! Ikiwa unataka kusoma hapa lazima urudi darasa la tatu kutokana na kiwango chako cha elimu. Kijana akalia baada ya kulia nikamwabia ikiwa unataka kusoma ndio huko huko, ukitaka utaanza darasa la tatu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nisisitize tena kwamba lazima wizara iandae mikakati itakayopelekea, maana yake kama kuna wizara ambayo

inahitaji hasa ifumuliwe, maana yake iundwe tena upya, ijapo mawaziri ni nyinyi simwambii Mhe. Ali Juma Shamuhuna aondoke aah! Maana yake usije kusema mbona anaanza kuniandama tena, ukae wewe na naibu wake ndiye huyo huyo lakini pafumuliwe kiasi cha kuhakikisha elimu tunayokuja nayo ni nzuri. Elimu ilingane na nchi nyengine zilizotuzunguka katika Afrika ya Mashariki na Kati.

Mimi ninadhani hilo linawezekana, lakini katika hali hii tunayokwenda nayo hii, walimu njaa, walimu hawana maslahi, kila siku unasikia mitihani imeshaibiwa. Hii haiwezi kutupa elimu ambayo ni nzuri. Kwa hivyo ninaiomba wizara na mimi ninaamini Mhe. Waziri kazi hiyo unaiweza vizuri tuweze kufikia katika kiwango hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba zaidi katika bajeti hii mimi nitahitaji ufafanuzi kwa sababu sasa hatuwezi tukawa tunakwenda kupitisha mafungu bila ya kujua Baraza hili fedha hizi zinakwenda katika mafungu gani. Naiomba wizara zaidi ijikite katika maeneo mawili muhimu.

Eneo la kwanza elimu ambapo tunaweza tukaitengeneza na ikawa ni elimu, ni elimu ya msingi au elimu ya maandalizi na msingi. Mimi ninakubali kabisa hapa ndio pahala hasa pa kupafanyia kazi. *Kambare mkunje angali mbichi*…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika 5 za kumalizia.

Mhe. Omar Ali Shehe: Haya.

Kambare mkunje angali mbichi. Tatizo la elimu linalotukumba sisi ni kwamba hichi chanzo cha elimu ya maandalizi na msingi, hapa ndipo penye matatizo. Kama kuna pahala mbapo serikali inapaswa kuekeza fedha nyingi sana ni katika elimu ya maandalizi na elimu ya msingi. Lakini vile vile sehemu ya pili serikali inaweza ikaekeza sana ni katika elimu ya vyuo vya juu.

Maeneo haya mawili ni maeneo muhimu sana na ni maeneo nyeti sana. Lakini sisi kwa kweli haijulikani hata tunapoelekeza tunakwenda tu. Kwa hivyo baada ya hayo machache kwa sababu leo nina msiba sana Mhe. Mwenyekiti, kusema kwangu kutakuwa ni kudogo sana, tena mpaka nitakapopata maelezo nitaiunga hii mkono.

Lakini ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kwa umakini sana anijibu hoja zangu hizi, vyenginevyo basi msimamo wangu ni pale pale kwamba fedha hizi zilizoongezeka kwa Wizara ya Elimu na wizara nyengine zitakazokuja,

fedha zote tunazikata hizi zinapelekwa kwenye ununuzi wa meli pamoja na vifaa vya kuokolea.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii na mimi kwa kuwa mchangiaji wa pili jioni hii ikiwa ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii. Kwa nafasi yangu Mhe. Mwenyekiti, ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii.

Sasa kwa kadri ya ufahamu wangu naomba nichangie mawazo yangu kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi naomba nitoe pole kwa Wazanzibari na Watanzania kwa jumla kutokana na msiba uliojitokeza juzi wa meli ambayo imetokezea katika bahari yetu, ambapo tulishuhudia majeruhi na maiti mbali mbali kama Wazanzibari na Watanzania.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wananchi wa jimbo langu tunawapa pole wale wote waliofiliwa na wale ambao wameokoka Mwenyezi Mungu awape subra waendelee kuvumilia na kwamba kazi ya Mwenyezi Mungu haina makosa.

Mhe. Mwenyekiti, kama mwenzangu alivyosema sisi kama Wawakilishi tutaendelea kusema na kusisitiza kwamba Katiba zetu zote mbili zinahimiza ulinzi wa raia na mali zao. Kwa hivyo kama ni Mwakilishi Mhe. Mwenyekiti, tutaendelea kusisitiza hilo na ninaona kama hatutochoka kusema hilo kwa sababu Wazanzibari wanahitaji kulindwa kwa mujibu wa Katiba wao binafsi na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nianze mchango wangu moja kwa moja kwenye Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo ninasisitiza ni kwamba ninahitaji majibu ya kina ya fungu la mishahara lililoingizwa tangu 2010 ambalo halikuwafikia walengwa kwa maana wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiwa Mjumbe wa kamati na pia ni Mwakilishi nimekuwa nikifuatilia kwa karibu mno maslahi ya walimu na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, kwa nini fedha zao zilizoingizwa kama sehemu ya mishahara yao zilitumika kwa matumizi ya kawaida, jambo ambalo limewanyima haki wafanyakazi wetu, na vile vile limedumaza utendaji na ufanisi mzima wa mafunzo ya amali kama nyenzo iliyokusudiwa kujenga maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, fungu hili kutumika katika matumizi ya kawaida ni kinyume na sheria ya fedha. Fungu hili lilikusudiwa mishahara na kadri ya ufutiliaji kama kamati, majibu ambayo Mamlaka wametupa bado hayajaridhisha. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba …

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wa Mhe. Hija msaidieni muondoleeni simu yake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwamba lazima mafunzo ya amali yapatiwe fedha kama ilivyokusudiwa, na kamwe kusiwe na ubabaifu na matumizi yasiyokuwa ya kisheria. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakuomba sana unipatie sababu za msingi kwa nini fungu la mishahara la wafanyakazi wa Mafunzo ya Amali lilitumika kama fedha za kawaida kama za OC. Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni hoja ya kwanza.

Hoja ya pili Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki kuna jina la Baraza la Upimaji la Tathmini ya Elimu ya Juu. Mhe. Mwenyekiti, kadri ya ufahamu wangu Baraza hili halikupitisha jina hili. Baraza hili lilipitisha Baraza la Mitihani la Zanzibar na wala sio Baraza la Upimaji na Tathmini ya Elimu ya Juu. Kama hii ndio sheria ambayo Mhe. Rais ameitia saini, hii ni sheria mpya ambayo sisi hatukuipitisha.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba sana Mhe. Waziri na Mhe. Mwanasheria Mkuu atwambie kwa nini hadi hii leo sheria iliyopitishwa sio hii na wizara yake imetuletea jina hili ambalo si jina ambalo Baraza hili tulivyolipitisha kama ni sheria.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ninalotaka kusema ni suala zima la Chuo cha SUZA. Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi ni miongoni mwa Wajumbe ambao hawaridhiki na fungu ambalo linatengwa kwa ajili ya kuendeleza Chuo cha SUZA. Mahitajio ya chuo kikuu chetu, walihitaji bilioni ishirini na tatu kwa ajili ya kuendesha kazi za kawaida kama chuo, ikiwa ni sehemu ya kupata walimu, kuboresha miundombinu ya ndani pamoja na kuboresha taaluma nzima ya fani mbali mbali ya Chuo Kikuu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya serikali imewapatia bilioni 4 kama mishahara na milioni 200 kama matumizi mbali mbali ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, dunia nzima chuo cha taifa ni chuo muhimu sana. Sasa kutoka bilioni 23 ambazo wamezihitaji wenzetu wa SUZA kuwapatia bilioni 4.2 kwa kweli ni mzaha na zaidi ni kwamba serikali haijakusudia kuekeza kwenye taaluma hii ya kielimu. Mimi binafsi Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kuona kwamba serikali inazungumza mdomoni kwamba inahitaji kuendeleza elimu, lakini kumbe ni nadharia tu sio kwa moyo wa dhati kabisa.

Kwa hivyo, mimi ninavyoona kuwapatia fedha ndogo chuo cha SUZA ni kudumaza elimu na kama yale malengo ambayo serikali imekusudia ikiwa ni pamoja na kuongeza vyuo vyengine yaani kuviunganisha nadhani ni ndoto ambayo haitafikiwa kwa zaidi ya miaka 10.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na Mhe. Salmin Awadh kwamba tusije tukafanya mchezo tukaamua kuichukua Chwaka, Kizimbani na Mbweni ikawa sehemu ya Chuo Kikuu. Tumeshindwa kushughulikia mkono mmoja wa shati, itakuwaje tushughulikie mikono minne ya shati.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasaha zangu ni kwamba SUZA iwachiwe SUZA isiunganishwe na matawi mengine, kwa sababu hatuna ujasiri wa kuwapa fedha kwa ajili ya kufanya shughuli zao. Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye suala zima la bodi ya mikopo ya elimu ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefanya utafiti na nimeomba tupatiwe orodha ya watu waliopewa mikopo ile. nashukuru nimefanikiwa kupata ule orodha na bodi ya mikopo wamekiri kwamba waliomba bilioni 8.4 na serikali ikawapatia bilioni 7.8 kwa miaka hiyo minne mfululizo. Lakini matumizi ambayo wametumia, kwa mujibu wa maelezo yao wenyewe ni shilingi bilioni 4.02. Hoja ni kwamba wawakilishi wanahitaji kujua, bilioni 7 zimekwenda wapi. Nimebahatika kuona kitabu cha majina ya wanafunzi, nimejumlisha mmoja mmoja na hesabu yake ni bilioni 4. Mhe. Waziri utuambie sasa zikowapi bilioni 3.3.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani kuwa wizara hii ya wataalamu ikose kuwapata watu iliyowakopesha. Mwenye duka anauza sukari kilo kumi za kufunga, maarufu mtumba anamjua kila mtu aliyemkopesha seuze serikali. Ndio serikali inatuambia inawatafuta watu iliyowakopesha ni aibu. Mimi kama mwakilishi niliwahi kuwa mwalimu sielewi suala hili, ni lazima watuambie walimpa nani. Shutuma ni kwamba fedha hizi zilitumika kwa maslahi binafsi, hapa ndio inakuja orodha ambayo mmetupa wanafunzi Wazanzibari kimewatafuta na gharama yake ni bilioni 4.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri sasa atuambie ziko wapi bilioni 3.7 fedha za walalahoji, Wazanzibari wanyonge. Mhe. Mwenyekiti, suala hili kama sijapata maelezo, basi nitawasilisha sheria zangu, wasiwe tayari kuidhinisha fedha mpya ya bilioni 8 kuwapa watu ambao hawamjui nani wanayemkopesha. Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani na nimesema hivi kwa sababu ninayo majina na wamekuja watu juzi mbele ya wenzangu wote wapo. Walituambia huu mkopo mpya, wameambiwa kwamba kila mtu ambaye anataka mkopo atowe shilingi laki tatu. Nimeambiwa mbele ya wenzangu zaidi ya 20, walikuja vijana ambao wameomba mkopo, wakaambiwa kama

mnataka mkopo toweni shilingi laki tatu. Kumbe fedha ya serikali ni biashara ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, majina tunayo ya watu duniani wote waliokuja na tuko tayari kuja hapa kuthibitisha. Kama mtu ana uwezo wa shilingi laki tatu basi asingekopa. Mzanzibari mwenye uwezo wa shilingi laki tatu za kuhonga rushwa, basi asingekuwa tayari kukopa fedha kwa ajili ya masomo. Kwanza Mhe. Waziri tupatie bilioni 3.5, halafu tuambie kwa nini fedha ya serikali ni kitega uchumi cha watu fulani. Mhe. Mwenyekiti, hayo tumeambiwa kama wanakamati, tena tumeambiwa kwa ushahidi kwamba vijana wetu sasa wanaambiwa watowe fedha kwa ajili ya kupatiwa mkopo. Mhe. Mwenyekiti, kama huu ndio mtaji wa bodi hii nadhani hatuna haja ya kuwapatia fedha kwa sababu kumbe ni kitega uchumi cha watu fulani.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye sakata zima la vyeti feki. Mhe. Mwenyekiti, nimefanya utafiti kidogo. Nimekwenda Chuo cha Kiislamu pale Mazizini, wanafunzi wa diploma ya msingi waliomaliza mwaka 2010 walikuwa ni 775, kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 246 walipasi moja kwa moja na wanafunzi 124 walikuwa wanasafu na walisapua, jumla yao ni wanafunzi 370 kwenye wanafunzi 775. Ni dhahiri wanafunzi 405 walipata ziro.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni la kusikitisha sana. Kumbe kuna wanafunzi ambao wana vyeti ambavyo sio halali na hao ndio waziri wa utumishi alioamua kuwaajiri kama walimu wa sayansi. Mhe. Mwenyekiti, mimi niliwahi kuwa mwalimu, taaluma ya ualimu haiendi hivyo, unampa mtu cheti feki maana yake nini, maana yake unamuhalalisha aajiriwe, baada ya miaka miwili unamuhalalisha aende akachukuwe digrii, ameshindwa diploma ya msingi Mazizini aje amudu digrii. Mhe. Mwenyekiti, hilo pia wamekuja hapa Barazani, wametuita na wako tayari kuthibitisha kwamba maafisa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio waliotoa vyeti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninayo aina moja ya cheti, naomba nikuonyeshe kwamba haiwezekani. Cheti hiki Mhe. Mwenyekiti, kina muhuri wa Msaidizi Mkuu wa Chuo, kina muhuri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, saini unaweza ukaghushi. Saini yako mimi naweza nikaghushi.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri aniambie, kwa nini mtu aghushi cheti na baadae apate muhuri *original* wa wizara. Walituambia, ilikuwa siku ya Ijumaa kuna mvua, unatoa shilingi laki tatu mkono wa kulia unapewa cheti, ni dhambi kubwa. Walituambia vinatolewa vyeti zaidi ya 200, maana yake nini 200 mara laki tatu ni milioni 600. Mtu anakaa kwenye kompyuta anatafuta mtaji ni hatari kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa Chuo cha Kiislamu kinafanya haya, je makafiri watafanya nini wao. Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huu ajira ambazo zimeajiriwa utumishi wa umma kwa kisingizio cha walimu wa diploma ya sayansi sio halali. Sio halali maana yake mmepotosha serikali. Mhe. Mwenyekiti, katika hili nimeomba kupatiwa majina ya walimu na shule zao, naomba nizitaje.

Mhe. Mwenyekiti, shule ambazo walimu hao wapo, naomba nisitaje majina. Mwalimu mmoja ameajiriwa Nungwi, mwalimu mmoja yuko Kiboje, mmoja yuko Kidimni, mmoja yuko Wilaya ya Kati, mmoja yuko Kinyasini na kadhalika. Unamchukua mwalimu mwenye ziro ya diploma ya msingi unamwambia akafundishe *form four* ya Kiboje, halafu unategemea kupata divisheni *one* au *two*, maisha hatupasi. Kumbe walimu wetu ndio wale wenye maziro ndio ambao wanawafundisha watoto wetu kwa ajili ya kusubiri matokeo ya *form four*, kwa nini tusikopie, kumbe wanafunzi waliokopia mwaka jana ni halali yao hawana walimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini tuwape fedha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Waheshimiwa Wajumbe, kwa nini tuwape fedha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ikiwa wao ndio wanaoandaa walimu feki kwa ajili ya kuwasomesha wanafunzi wetu feki. Mhe. Mwenyekiti, eti Zanzibar tunataka kujiunga na Afrika ya Mashariki kwenye ushindani wa soko la ajira, kwa mfumo huu.

Mhe. Mwenyekiti, naungana na Mhe. Omar Ali Shehe kwamba kuna haja ya Mhe Rais kama dhamana wa nchi hii kuliangalia suala hii kwa upana sana na wala msiseme kwamba wanafunzi hawa walighushi vyeti. Wanafunzi hawa walipewa vyeti na maafisa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa ushahidi na wanajulikana ni lazima washughulikiwe kwa kutiwa adabu, kwa kusababisha wananchi wetu kupata vyeti feki.

Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe umebakiza dakika tano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, CCM wanatuambia kwamba eti mmekosa walimu wa sayansi Zanzibar, tuwapatie fedha mkachukuwe walimu Nigeria. Mhe. Mwenyekiti hilo mimi siungi mkono, kwa sababu kama kweli mnahaja ya walimu wa sayansi basi mngewaondosha wale wote ambao wanawapotosha vijana wetu katika masomo ya sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, leo Zanzibari feki. Mzanzibari ndiye anayesifiwa kwa uaminifu. Mnigeria mnawajua historia yao, ni magube tu. Kwa hivyo, tuwapatie fedha walimu wa Nigeria ili waje hapa wawasomeshe wanafunzi wa Lumumba na Fidel Castro. Mhe. Mwenyekiti, mimi siungi mkono. Mimi wazo langu ni kwamba muwatafute wataalamu wa Zanzibar wa ndani hata wale ambao wamestaafu tuwakusanye halafu tuwapatie fedha wawasomeshe watoto wetu, wapo lakini mmewaacha wameondoka leo mnahangaika. Maana yake huku nyuma kuna Mnigeria hapa na Mhe. Waziri anabadilishana hati. Mhe. Mwenyekiti, sio kila aliyevaa kanzu na kofia ni mtu muhimu, mtahadhari sana. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe niwaombe sana msimpe Mhe. Ali Juma Shamuhuna jukumu la kutupatia walimu kutoka Nigeria, halafu baadae mtamlaumu na akae na wataalamu wake, awatafute Wazanzibari walioko Pemba, Unguja na Bara waje hapa wawasomeshe watoto wetu. Hata kwa mzunguko, wiki moja Pemba, wiki, Makunduchi, wiki Makunduchi, wiki Mkoani lakini Wazanzibari tuwapatie fedha kwa ajili ya kusomesha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba hoja yangu ya vyeti nipate majibu, ndio tiketi ya bajeti hii ni asilimia 50 hiyo na mikopo ni asilimia 50 vyenginevyo bajeti hii sitoipitisha. Niwaombe wawakilishi kwamba msitegemee wanafunzi wenu watapasi kwa mfumo huu wa vyeti feki na hivi havijaandaliwa na mtu wa kompyuta Vikokotoni ni maafisa wenyewe ndani ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio waliotoa vyeti hivi. Wanafunzi wapo, wameacha namba za simu kama tukiwahitaji tuwaite na wako tayari kuwataja wale waliofanya mambo haya

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba majibu na siungi mkono hoja mpaka nipate majibu hayo. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kutoa mawazo yangu katika mchango wangu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah, aliyenijaalia jioni hii kuwa katika hali ya uzima na afya njemaa.

Vile vile kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kojani, naomba kutoa pole kwa wafiwa wote katika meli iliyopata maafa na ikazama kutoka Dar es Salaam kuja Zanzibar. Nawatakia wenzetu waliotangulia Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi, amin.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu nianze moja kwa moja kwenye elimu ya msingi. Katika ukurasa wa 11 kifungu cha 23, kimeeleza kuimarisha elimu ya msingi. Mhe. Mwenyekiti, hapa mimi naipongeza serikali kwa kulijua hili,

kwa sababu watoto wetu wanaanza kufeli katika elimu ya msingi. Mtu anafika darasa la saba, wengine ni tatizo kujua kusoma na kuandika. Mhe. Mwenyekiti, kama tutajiandaa vizuri kama tulivyokusudia basi tutafika malengo.

Mhe. Mwenyekiti, unapotaka kuimarisha ni lazima ujiandae na katika kumuandaa mtoto kwenye masomo uwe na skuli za maandalizi, lakini skuli za maandalizi kwa kule kwetu shamba hamna kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema ni aibu kabisa. Natoa mfano katika Jimbo langu la Kojani, mwaka jana skuli ya Kojani Kisiwani haikutoa hata mtoto mmoja aliyefaulu na skuli ya Chwale haikutoa hata mtoto mmoja aliyefaulu darasa la saba. Mhe. Mwenyekiti, hii inavunja moyo sana. Hapa tunataka tuelezwe sasa hivi serikali imejipanga vipi ili kukabiliana na mambo haya. Hilo moja.

Nikitoka hapo moja kwa moja niende katika elimu ya juu, katika kifungu cha 124 mpaka kifungu cha 139 kwenye ukurasa wa 58 mpaka ukurasa wa 64 imeelezea elimu ya juu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nieleze maana halisi ya elimu ya juu kwa sababu ya utata uliopo. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, la elimu ya juu ni la Muungano, kama ni suala la Muungano kuna utata uliopo kiutendaji na kiuwezeshaji. Mhe. Mwenyekiti, kwa maana kwenye utendaji wanatusimamia wenzetu hawa. Mitaala ni yao, *syllabus* ni yao na Baraza la Mitihani yote wanasimamia wao, isipokuwa mishahara tu tunawalipa walimu wetu sisi je, hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, wengine wametumikia taasisi za Muungano, wanalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Kwa mfano, polisi, jeshi, uhamiaji, anga na kadhalika. Kwa nini sisi hawa walimu wanaosomesha elimu ya juu wasilipwe na Jamhuri ya Muungano. Mhe. Waziri utakapokuja hapa utueleze kwa kina jambo hili na sisi tulifahamu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze ni kiasi gani serikali imesaidia vyuo vya elimu ya juu binafsi ambavyo vimetoa mchango mkubwa hapa kwetu. Kwa mfano, Chuo cha Tunguu na Chukwani, vinatoa fani mbali mbali, wakiwemo wataalamu wa sheria, uchumi, utawala, bishara na kadhalika.

Vile vile nataka kujua ni kiasi gani serikali ya Muungano inachangia bajeti ya masuala ya elimu ya juu visiwani. Mhe. Waziri utakapokuja hapa utupe maelezo ya kina na sisi tupate kufahamu kwa sababu suala hili la elimu ya juu

ni suala la Muungano. Pia Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapofika hapa Baraza la Mitihani lina watumishi wangapi na kati ya hao Wazanzibari ni wangapi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba unielimishe na kujua, kwa nini Baraza la Mitihani ambalo ni chombo cha Muungano hakianzishi ofisi ndogo visiwani Zanzibar, kama zinavyofanya taasisi nyengine za Muungano. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mitihani nalo lingeanzisha ofisi ndogo kama taasisi nyengine tukaweza kupata hata ajira. Lakini kumekuwa na kitu hata kama itaanzishwa ofisi hiyo ndogo hapa, basi na wafanyakazi wanawatoa kule Tanzania Bara, sisi hatufaidiki. Mhe. Waziri utakapokuja hapa utueleze kwa kina. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Mitihani kama litaanzisha ofisi ndogo ndogo hapa kwetu visiwani basi nadhani tutafaidika vya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 41, kuna Idara ya Technolojia ya Habari na Mawasiliano, ambayo inatekeleza mradi mkubwa wa kutumia kompyuta kama chombo cha kujifunza na kufundishia kwa skuli 248 zitafaidika. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sisi watu wa majimbo ya shamba na skuli za shamba tuna hofu kubwa sana na mambo hayo sana hufikia mjini. Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri atakapokuja hapa basi anifahamishe ndani ya jimbo langu ni skuli ngapi zitafaidika na mradi huo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la walimu ambao ni kidogo sana maskulini, lakini kuna walimu wanaojitolea kuanzia mwezi wa April mpaka hapa ninapozungumza hawajaajiriwa, wakiwemo walimu wa sayansi. Mhe. Mwenyekiti, ukitaka kujua suala hili kwa kule kisiwani Pemba wapo walimu wanaotoka Mtambwe kwenda kufundisha Fundo, wapo walimu wanaotoka Gando kwenda kufundisha Fundo, wako walimu wanaotoka Mchangamdogo wanakwenda kufundisha Fundo. Mhe. Mwenyekiti, wanapiga kambi wiki nzima na maslahi yao wanayopata ni kidogo sana na wana familia.

Kwa hivyo, mimi napenda kusema kwamba walimu tuwaangalie kwa jicho la huruma, bila ya kuwawezesha walimu wakapata mahitajio yao, basi hatutopata watoto wenye elimu, kwa sababu walimu wenyewe hawako walimu kwa hivyo hatokuwa na uwezo wa kufundisha kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, imezungumzwa hapa *tuition*. Mimi niungane na wenzangu kwamba hizi *tuition* nyengine zinatuletea matatizo kwa watoto wetu. Mtoto anakwenda *tuition* mpaka saa nne za usiku mtoto mwari. Atakuletea *tuition* ya kweli, maana yake akija atakuja na ujauzito.

Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwa tukisoma sisi mwanafunzi ilikuwa ikifika saa 2:00 za usiku hasubutu kutembea tena. Lakini yote ni mila, silka na

utamaduni wetu umeondoka, tumewapa uhuru mkubwa watoto wetu wanafanya wanavyopenda. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kama kweli inataka kutupa elimu ya kutosha basi lazima kuwe na mikakati endelevu, kwa sababu mtu unapompa uhuru mpaka ukapindukia unakuwa sio uhuru ni matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak alizungumza hapa asubuhi kwamba wazee na sisi tunachangia, uhuru umekuwa mkubwa kwa watoto wetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, siungi mkono hoja mpaka nitakapopata maelezo ya kutosha ya Mhe. Waziri, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai tukiwa wazima na tunaendelea na mjadala wa bajeti kwa wizara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Leo tukiwa tunajadili bajeti ya wizara hii muhimu ya elimu na mafunzo ya amali.

Vile vile nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa maoni yangu katika bajeti hii. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuingia katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe ninaowawakilisha hapa, naomba niungane na wenzangu wote kutoa mkono wa pole kwa Wazanzibari wote, lakini hususan ndugu, jamaa na marafiki wa wale ambao wamepoteza maisha yao, katika ajali ya meli ya Mv Skagit ambayo ilitokea majuzi.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kwamba Wazanzibari hawawezi kuendelea tena kila siku kushuhudia wakipoteza maisha yao, kutokana na sababu ambazo zingeweza kuepukwa. Mhe. Mwenyekiti, ni wazi kwamba juzi kulikuwa kuna dhoruba baharini, lakini maswali mengi yanaulizwa na wananchi kuhusu meli hizi na hasa za kampuni hii, na jinsi zinavyoruhusiwa na mamlaka zinazohusika kuendelea kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Yako maswali mengi Mhe. Mwenyekiti, leo sio mahala pake, lakini nilitaka kusema kwamba inasikitisha na Wazanzibari wanatuhoji sisi kama wawakilishi wao, kwamba je na hili mtanyamaza kimya kama mlivyonyamaza kimya. Sasa mara nyengine tukisema hapa, huwa tunalaumiwa kwamba labda tunakusudia kumlenga mtu na wala sisi hatumlengi mtu Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Sambamba na hilo kwa sababu sitaki nipoteze muda wangu niseme, kule kukosekana kwa umakini kwa serikali katika suala hili Mhe. Mwenyekiti, hata huduma za uokozi mara hii zilikuwa si za kuridhisha hata kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jana siku nzima nimeshinda bandarini pale hakuna huduma yoyote, boti za uokozi zimekwenda asubuhi na kwenda *trip* ya pili mafuta hakuna pale, basi tunajiuliza hapa kweli kuna maandalizi ya uokozi Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kwa hivyo, haya tutapata nafasi yake na tuyajadili kwa kina wakati ukifika. Lakini hapa niruhusu nitoe joto langu kwamba kusema kweli hatuonekani kwamba tunasonga mbele isipokuwa tunarudi nyuma kila siku Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika hili nasema wazi kwamba wale wote ambao waliokuwa na dhamana na wakashindwa kutekeleza dhamana zao, Wawakilishi wa wananchi tunadai wawajibike Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba wakati wake utafika tukijaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawaombea wote ambao wamefariki Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi, na sisi atupe subira na pia atupe nguvu ya kusimamia uwajibikaji katika serikali yetu, ili mambo yanayoweza kuepukwa basi tuone yanaepukwa katika nchi yetu kuliko kusababisha vifo vilivyokuwa havina sababu. *(Makofi)*

Vile vile nitumie fursa hii Mhe. Mwenyekiti kwa kusema nalaani vikali kitendo cha Spika wa Bunge kukataa kuakhirisha Bunge baada ya Wazanzibari walioko ndani kutoa hoja, ili kutoa nafasi kwenda kuungana na wenzao kuonesha kuguswa na hisia za vifo vilivyotokea Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kitendo kile kimewafadhaisha wazanzibari wengi sana na haidhuru baadae palichukuliwa jitihada za kujaribu kusawazisha hali, lakini tayari athari imeshaonekana. *(Makofi)*

Sasa mambo kama haya Mhe. Mwenyekiti, ndiyo yanayowafanya wazanzibari wahoji kwamba kweli kuna nia ya dhati ya udugu unaozungumzwa kila siku katika hili. Kwa mfano, ajali ile ingewakumba wengine wasiokuwa Wazanzibari Bunge lingekataa kuakhirishwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haya ndiyo mambo wazanzibari wanayahoji na mimi nasema nalaani kabisa hatua ile iliyokuwa imefanyika pale ya Spika yule, ambaye hakuonekana kabisa kujali hisia za wananchi wa Zanzibar katika mkasa ule. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nirudi katika Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Mwenyekiti, elimu ndio roho ya maendeleo katika nchi yoyote, wakati fulani nilipokuwa nikichangia hapa katika mjadala wa Kamati na katika mswada mmoja wa Wizara ya Elimu, niliwahi kunukuu makala hii inayoitwa *Pass the Books. Hold the Oil*, iliyoandika na mwandishi mmoja maarufu, ambaye ni msomi mkubwa anayeitwa **Thomas Friedman**.

Mhe. Mwenyekiti, hii inaonesha kwamba kuwa na utajiri wa rasilimali sio maana ya kuendelea kiuchumi kwa nchi, wamefanya utafiti kuonesha kwamba kuna nchi ambazo zimeekeza katika kusomesha watu wao, ndizo zilizopiga hatua kubwa za kiuchumi. *(Makofi)*

Lakini leo sina muda wa kunukuu, nataka niseme kwamba zimetajwa nchi kama vile Taiwan, kwamba wao wameekeza kunyanyua vipaji vya watu wao, nchi ambayo hata mchanga wa kujengea inauagiza kutoka China, lakini leo ni katika nchi ambazo wastani wa pato la mwananchi ni miongoni mwa nchi zinazoongoza duniani kabisa. *(Makofi)*

Vile vile kuna nchi ambazo zina mafuta humu hayo tunayoyapigania sisi tuyachimbe hapa, lakini zimeshindwa kuendelea kwa sababu hazikuekeza fedha zile za mafuta na rasilimali nyengine katika kusomesha watu wao.

Mhe. Mwenyekiti, hii nitampa baadaye na kila wakati ninapenda kuwapa na kila Mhe. Waziri wa Elimu anayekuja aisome, ili apate kujifunza. Lakini nalisema hili Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mwaka huu bajeti ya Wizara ya Elimu imeongezwa si haba, ukitizama *trend* bajeti ya shughuli za kawaida kuanzia 2009/2010 ilikuwa shilingi bilioni 27,875,995,644/=, mwaka 2010/2011 ilikuwa shilingi bilioni 42,861,309,345/=, mwaka 2011/2012 ikawa shilingi bilioni 45,308,000,000/=, lakini mwaka huu ni shilingi bilioni 71,050,000,000/=. Kwa kweli hilo ni ongezeko la zaidi ya nusu kuliko bajeti ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuuliza *trend* hii inasaidia kunyanyua elimu yetu, jawabu Mhe. Mwenyekiti hapana. Mimi mara hii kwa sababu nimejikita kuyatizama mafungu ya bajeti nimejua kwa nini hatuendelei kielimu, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Bajeti za Wizara ya Elimu zimegeuka badala ya kuekeza katika kusomesha watoto wetu, imekuwa ni fungu la kujinufaisha watawala katika Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwape nasaha ndogo tu watendaji wa wizara, naona siku hizi umekuwa ni mtindo na nilisema hapa, kwamba kila mtu akija

hapa anarekebisha na tunapewa upya hesabu za bajeti za wizara. Kwa hivyo, nataka niwaambie kwamba mkifanya hivi ndio mnajianika.

Mhe. Mwenyekiti, nilipopewa hii nimeilinganisha na ile ya awali iliomo katika hili buku. Katika jambo la kustaajabisha kwamba kuna mafungu makubwa yamewekwa unaona yamepunguzwa ghafla, lakini kwa sababu fedha hizi zinataka kwenda kutafunwa pahala fulani, basi zimebandikwa katika idara zile zile, isipokuwa zimehamishwa hapa na kupelekwa kule, yaani kama Mchezo wa Sarakasi Mhe. Mwenyekiti.

Kutokana na hali hiyo, watafute watu wa kuwadanganya sio Wawakilishi wa Baraza hili, kwani tunayo macho na darubini kali tena tunaona. Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano tena naomba uniridhie nisilisome lote, kwa sababu nikilisoma lote nitamaliza muda wangu wote kulijadili hili tu kwa ukubwa wake, lakini nitatoa mfano na baadae nitakuja kusimama kwenye vifungu vya kila idara kwa sababu mifano ndio ile ile. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano kwa idara moja tu Idara ya Mipango, Sera na Utafiti buku la awali mwanzo Fungu la Mishahara Fedha Taslim katika eneo la *vote* 211107 Malipo baada ya Saa za Kazi palikuwa na shilingi milioni 116,599,000/= katika hili buku, baada ya kuona kuna hoja imepunguzwa ile shilingi milioni 100 imepungua na kubakia zile shilingi milioni 16,599,000/=, lakini ile shilingi milioni 100 itapelekwa katika kusomesha watu, hapana isipokuwa imegaiwa.

Kwa hivyo, katika zile shilingi milioni 30,000,000/= zikaingizwa katika vote 220105 kwenye Gharama za Vifaa vya Uchapaji na ilikuwa ni shilingi milioni 11,009,000/= na ikafanywa shilingi milioni 41,009,000/=. Halafu zikachukuliwa nyengine shilingi milioni 20,000,000/= zikaingizwa katika Gharama za Safari za Nje na palikuwa na shilingi milioni 4,000,000/= na pakafanywa shilingi milioni 24,000,000/= katika idara hiyo hiyo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, hazijatimia ziko shilingi milini 30,000,000/= zitapelekwa wapi kwenye Gharama za Mafunzo Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilikuwa hana fedha za mafunzo palikuwa na zero zero kama ilivyokuwa mwaka jana na pakawekwa pale shilingi milioni 30,000,000/=. Kwa hivyo, zile shilingi milioni 100,000,000/= zikafanyiwa hesabu yake na kutimia pale, Mwakilishi asishtuke kama fungu hili limevimba basi litawanywe huku na kule Mhe. Mwenyekiti.

Kwa kweli namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akayatizame hayo yako katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pia yako katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji, yako katika Idara ya Elimu ya

Maandalizi, Msingi na Kati, Idara ya Sekondari, yaani yako katika kila pahala. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, Mhe. Mwenyekiti, situmii muda wangu adhimu hapa ninayo mambo mengi ya kuchangia nikayachambua moja moja. Lakini ninachosema kwamba yote nitayahoji wakati wa vifungu, naomba hilo liwe *noted*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, unaona matumizi mabaya ya mafungu. Kwa mfano, kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Fungu la Misaada ya Kijamii 272100 Ushauri Nasaha kwa Wanafunzi, mwaka jana lilikuwa shilingi milioni 65,000,000/= na mwaka huu ni shilingi milioni 220,000,000/=. Hivi ni ushauri gani nasaha huo unaotolewa wa kuchukua shilingi milioni 220,000,000/=. *(Makofi)*

Kwa kweli haya yapo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba mafungu yaliyoongezeka ni kwenye safari, viburudishaji vimeongezeka mara kumi kwenye mafungu mengine katika kila idara Mhe. Mwenyekiti, unashangaa kwamba na kujiuliza watu hawa wako *serious*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nasema ningetegemea fedha hizi zingekwenda katika huduma za walimu, ili kuongezeka kwa bajeti hii kusaidie walimu na elimu. Lakini limekuwa ni limbikizo la watawala wanaojikusanya pale katika Makao Makuu ya Wizara ya Elimu kwenda kutafuna fedha za walipa kodi, hatukubali Mhe. Mwenyekiti. Nasikitika sana tena wengine ni walimu wangu, lakini hapa nimetumwa na wananchi kwa ajili ya kuja kutetea na kufanya kazi yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba hili naliacha, kwa sababu hili nikilichambua tutamaliza muda wote. Kwa hivyo, ninachosema ni kwamba yote haya wakati nikija kwenye vifungu nitayahoji moja moja.

Vile vile nataka kukubaliana na Mhe. Omar Ali Shehe, kwamba Mhe. Mwenyekiti katika wizara ambayo tutaikatia mafungu yake tuyapunguze yaende kwengine tutaanza kuonesha mfano katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa kweli tulipunguza katika wizara ya mwanzo Ofisi ya Rais shilingi milioni 40 za TV ambazo hazina maelezo. *(Makofi)*

Hali hii inaonesha kwamba watu si wakweli katika mafungu haya, kwa sababu kama kweli zilikuwa zimekusudiwa vile, huwezi kuzitawanya namna hii na kutueleza kwamba Wizara ya Fedha imekosea na wala si kweli Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa hizi zimewekwa watu kutega kuna mambo yao humo. *(Makofi)*

Kwa hiyo tutayakata Mhe. Mwenyekiti tena nina hakika kwamba tukipunguza humu na zitakwenda kwenye mambo yanayohusu elimu, huduma za skuli, huduma za vitabu na kuna mambo mengi ambayo ni muhimu yanayohitajika tena katika Wizara hii ya Elimu na wala sio nyengine. Kwa hivyo, kama nilivyosema naomba Mhe. Mwenyekiti, niishie hapo kuhusiana na suala hili kwa sababu sitaki kuchukua muda mwingi. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu na nilisema kwamba tunategemea kuongezeka kwa bajeti kwa wizara hii katika vipindi tofauti kuonekane katika kuimarika kwa hali ya elimu Zanzibar, lakini hali haiko hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, asubuhi Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema hapa, kwamba mafanikio ya sera yoyote yangeonekana katika tija matokeo yake, pia niliwahi kusema katika bajeti zilizopita hapa, kwamba tatizo *input* inayoongezeka, lakini *output* inazidi kuanguka, yaani *input* ni hizi fedha ambazo tunazowaongezea kila wakati, lakini *output* ni matokeo hatuyaoni.

Vile vile Mhe. Rashid Seif Suleiman alisema kwamba ukiangalia matokeo yale ya *Form IV* ukichanganya *Division IV* na *Zero* ni asilimia 85.1 kuanzia mwaka 2007 mpaka 2011. Lakini ukienda kwenye *Form VI*, ambao ungetegemea hao kama wangepasi vizuri wanao uwezo basi huku wangeonekana wanapasi vizuri, lakini nako bado *Division IV* na Zero ni asilimia 45 Mhe. Mwenyekiti. Sasa hii tunasema mafanikio ya Sera ya Elimu imeleta mabadiliko katika nchi au inazidi kutuangusha.

Kutokana na hali hii, hatuwezi tukajenga taifa linaloendelea, tukichukua ile mifano niliyoisema mwanzo ya mwandishi ***Thomas Friedman*** kwa kuwa na matokeo ya namna kama hii hatutajenga nchi maisha Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli hawa baadae na Wazungu wanasema '*ukiingiza taka utatoa taka'* na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ananisaidia hapa anasema Waswahili wanasema '*utavuna ulichokipanda'*.

Sasa leo tunapanda uoza huu tunategemea tutakuwa na watendaji wa maana kwa ajili ya kujenga nchi hii Mhe. Mwenyekiti, hatufiki. Mhe. Mwenyekiti, hili nataka kulitolea mfano mmoja mzuri sana. Katika skuli ambayo ni *symbol* katika Zanzibar hii ni Skuli ya Lumumba, ambapo hata mimi nimesoma Mhe. Mwenyekiti, tena viongozi wengi wameshiriki ilipokuwa inatimiza miaka nadhani 50 walishiriki kwenda kufanya Matembezi ya Mshikamano na kuchangia kwa hiari.

Leo Skuli ya Lumumba pekee imeweka *record* mara hii *division zero* 128 katika wanafunzi 300. Mhe. Mwenyekiti, katika hali kama hii tunategemea

kweli kujenga jamii ya watu walioelimika, ili waje watusaidie kuimarisha utendaji katika nchi, hata siku moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba suala hili tupewe maelezo wakati atakapokuja Mhe. Waziri, kwa nini tumuidhinishie Mhe. Waziri na wizara fungu hili la shilingi bilioni 71/= ikiwa matokeo ndio haya, wanafanya tathmini kiasi gani ya Sera hii mpya ya Elimu. Mhe. Mwenyekiti, naomba melezo katika hili. *(Makofi)*

Sasa niende kwenye suala jengine kama nilivyosema kwamba ninayo mambo mengi na muda leo mchache. Eneo jengine ambalo nataka litizamwe na Wizara ya Elimu na kama nilivyosema, kwamba kila wakati *focus* iko katika vipi watu watapata ulaji.

Mhe. Mwenyekiti, wapo waandishi wa vitabu wa Kizanzibari hapa, tena wazuri tu wengine na wameandika vitabu vizuri ambavyo vinatumika vyengine katika masuala ya lugha. Kwa mfano, Kenya, Tanzania Bara, lakini sisi Zanzibar tunawaporomosha na wala haviorodheshwi katika vitabu vya kusomeshea maskulini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunao waandishi hapa kama vile Bwana Ali Shaaban, Mzee Haji Gora, Dkt. Said Ahmed wapo waandishi wengi tu ambao wameandika, lakini hatuviorodheshi Mhe. Mwenyekiti, suala hili nililisema mwaka jana na narejea kusema mwaka huu, badala yake tunang'ang'ania waandishi na wachapishaji wa nje, kwa sababu ya majina tu.

Kwa mfano, *Oxford*, Macmillan na juzi tumeshuhudia *World Bank* imepiga marufuku kuchukua *tender* za *Oxford* na Macmillan kwa sababu ya rushwa iliyokuwemo tena Tanzania hii. Kwa hivyo, tusitizame jina tu, kwa sababu inaitwa *Oxford* au Macmillan, isipokuwa tutizame *quality of work*, ubora wa viwango wa kazi inayotoka pale.

Sasa kwa nini tunawaangusha waandishi wa Kizanzibari kama vitabu vyao vimefika kukubaliwa katika nchi au Afrika ya Mashariki hii, mfumo wao wa elimu ni mzuri zaidi kuliko wetu sisi, yaani wanapasisha wanafunzi vizuri zaidi kuliko sisi, kwa nini vitabu vile kwao vikubalike na sisi hapa tunaviangusha Mhe. Mwenyekiti na kwa nini tunawavunja moyo hawa.

Kwa kweli kama hatujengi vipaji vya Wazanzibari, hivi nani atavinyanyua vibaji hivi Mhe. Mwenyekiti, hili halikubaliki naomba maelezo Mhe. Waziri atakapokuja, mwaka jana nililiuliza na bado ninaendelea na mara hii nataka niambiwe kwa nini tunaendelea kuwavunja moyo waandishi wa Kizanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba sina muda wa kufafanua kwa kina natoa mifano michache.

Nikiondoka hapo, sasa naomba niende katika Chuo cha Kiislamu. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atakapokuja aje kuniambia Wizara ya Elimu imeamua kuua Elimu ya Dini ya Kiislamu Zanzibar na kukifunga hichi chuo. *(Makofi)*

Katika kitabu hichi wametuambia kwamba wanao mpango wa kukiendeleza kufika kuwa Chuo Kikuu cha Elimu ya Kiislamu Zanzibar nafurahi, lakini mbona hali halisi haioneshi hivyo Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli ndio yale malengo yanayoishia vitabuni, lakini katika hali halisi haijioneshi hivyo na hayo ndio mafanikio ya Sera yetu ya Elimu hayo, katika kufikia kuorodhesha wanafunzi tunasema tumefika asilimia 100 na tunajisifu kila pahala, lakini Mhe. Mwenyekiti, mafanikio hayapimwi kwa *quantity*, yanapimwa kwa *quality*. Mhe. Mwenyekiti, hili naomba maelezo.

Kwa nini nasema hali halisi haioneshi hivyo. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Elimu imeondosha mafunzo ya Shahada ya Ualimu, ambapo ilikuwa ni msingi wa ualimu bora, kwa nini waje watueleze. Lakini suala la idadi ya uchukuaji wanafunzi wa Chuo cha Kiislamu Mhe. Mwenyekiti, imeshuka kutoka 1500 hadi kufika wanafunzi 225 na katika hao wanafunzi 15 tu ndio wanaosoma Masomo ya Kiislamu pale. Sasa wizara ina lengo gani Mhe. Mwenyekiti, ndio lengo la kuanzishwa chuo kile. *(Makofi)*

Vile vile hata kwa mwaka huu Mhe. Mwenyekiti, katika wanafunzi walioomba ambao wanakaribia 230 kati yao 122 tu ndio walioomba Kitivo cha Masomo ya Dini, na kuna taarifa kwamba pengine hata hao hawatochukuliwa, sasa kuna lengo la kukiua chuo hicho Mhe. Mwenyekiti. Chuo hichi kilipoanzishwa kilikuwa na eneo la ekari 80 na leo tunaambiwa limebakiwa na ekari 40 tu na ardhi ile kapewa nani au ameichukua nani na inafanyiwa kazi gani? *(Makofi)*

Sasa pala kama ekari zote hizo zipo ndio pangekuwa na eneo la kuongezwa na kuwa hicho Chuo Kikuu cha Kiislamu tunachokitaka katika Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba hivi ndio kumuenzi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Kwa hivyo, naomba maelezo katika hili Mhe. Mwenyekiti, kwa nini niidhinishe fedha ambazo najua zinakwenda kumaliza mambo kuliko kutengeneza mambo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kidogo kama nilivyosema kwamba ninayo mambo mengi tena ya msingi, nadhani itaisaidia wizara. Sasa nije katika suala zima la walimu, kwa kweli huwezi Mhe. Mwenyekiti, kuimarisha elimu ikiwa huwathamini walimu, na sote sisi humu tuna jeuri yetu na tunajua kuchambua mambo humu kwa sababu tulisomeshwa na walimu. *(Makofi)*

Kwa mfano, ukienda kwa madaktari, mainjinia, wanasheria, wakaguzi pamoja na wengine, yaani wote wameanzia kwa mwalimu. Jambo linalonisikitisha ni moja, kwamba Wizara ya Elimu watendaji wake wengi walitoka huko kwenye walimu hawa wa ngazi ya juu, sasa mbona wanawasahau wenzao walikotoka kule. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati fulani liliwahi kuulizwa swali hapa na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alisema kuhusu michango, kwamba michango ile ni hiari, lakini walimu wanatuthibitishia kwamba mpaka leo wanaagizwa na Maafisa wa Elimu wawakate walimu kwa lazima, na imetajwa hapa michango mitano ya shilingi 1,000/= kila mmoja na kwa sababu ya muda sina haja ya kuiorodhesha na imetajwa na watu wengi hapa. Kwa hivyo, naomba maelezo kwa nini tunawalazimisha walimu kuchangia. *(Makofi)*

Lakini walimu mafao yao ya likizo hawapati, yaani mpaka baada ya miaka mitatu. Vile vile hata wanapopewa hawapewi kama wenzao zinakopwa mara walipwe shilingi 50,000/= tu, kuna nini hapa wakati mafungu ndio haya tunaidhinisha hapa sisi kila mwaka Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna hivi Vituo vinavyoitwa *Teacher's Centres* (*TC*), walimu wanatuambia kwamba wizara haishughuliki navyo hivi, isipokuwa vinakuja kuviombea fedha tu na mwaka huu fedha zimeongezeka hapa, lakini hawashughuliki navyo na badala yake wanavingoja vinapoongeza mapato, pengine vikipata misaada kutoka nje, basi Wizara ya Elimu inakwenda kuvisimamia, ili ipate mapato kutoka kwenye Vituo vya Walimu, badala ya kuvisaidia visomeshe walimu, ili viwaongezee mafunzo bado inataka kuvikamua. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo katika hili.

Vile vile naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti, kwamba walimu na alilizungumza hapa Mhe. Rashid Seif Suleiman wakati wa asubuhi, Walimu Wakuu posho yao wanayopewa ni shilingi 10,000/= na wengine wanaobahatika ni shilingi 15,000/=. Sasa yule Mwalimu Mkuu anapewa nusu yake ni shilingi 75, 00/= na Msaidizi Mwalimu Mkuu anapewa shilingi 5,000/=, hivi ndivyo tunavyothamini walimu Mhe. Mwenyekiti.

Kweli tunategemea walimu hawa watakuwa na ari na moyo wa kujituma kwa ajili ya kutujengea msingi wa elimu katika nchi yetu tukapata maendeleo, hata siku moja Mhe. Mwenyekiti.

Sambamba na hilo Walimu Wakuu hawa wametupiwa jukumu na wala sio hilo la kuwaongoza walimu wenzao, hata jukumu la kutafuta vyanzo vya mapato vya skuli kupitia kuziongoza na kuzisaidia Kamati za Wazee za Skuli. *(Makofi)*

Lakini kuna *incidence* Mhe. Mwenyekiti, kwamba Walimu Mkuu anahangaika na anapata msaada, sasa akeshakuupata basi Wizara ya Elimu inauchukua na kuupeleka kwengine. Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa mfano katika skuli ambayo iko katika jimbo langu Skuli ya Kajificheni, walifanya mpango wa kupata Mradi wa Maktaba.

Kwa hiyo, kuna bibi kutoka Uingereza alipita na kutaka kuwasaidia, mradi ule Wakuu wa Wizara ya Elimu waliona haufai kukaa Kajificheni wakauhamisha na kuupeleka Kisiwandui, yaani walimu walifanya kazi yote ile ya kuandika *project* na kila kitu hawakusaidiwa, kuna nini Mhe. Mwenyekiti, tunaomba tuambiwe na hivyo ndivyo tunavyowathamini walimu.

Mhe. Mwenyekiti, si hayo tu kuna tatizo la uhamisho wa ovyo wa walimu na huku nako pia ni kuwavunja moyo. Kwa mfano, katika Skuli ya Haile-Sellassie hivi karibuni kumehamishwa walimu 28 wanaambiwa pale wako wengi, lakini unaondosha walimu 28 kwa mpigo, unategemea utakuza elimu katika hali kama hiyo Mhe. Mwenyekiti.

Vile vile katika Skuli ya Michepuo ya Biashara pale kuna watu ambao wamesomea *degree* ya Uchumi walimu na wanasomesha masuala ya Mchepuo wa Biashara kuhusiana na uchumi.

Sasa leo kwa sababu tu kuna mambo hawaridhiki watendaji wa Wizara ya Elimu, basi wamewahamisha na wengine wamepelekwa Chukwani na Jang'ombe, mtu ana-*degree* ya Uchumi kwa ajili kusomesha Mchepuo wa Biashara Mombasa anachukuliwa na kupelekwa Jang'ombe akasomeshe *Biology*, hivi sisi tuko *serious* Mhe. Mwenyekiti, hatuwathamini walimu.

Mhe. Mwenyekiti, hata wanapokwenda wizarani kufuata huduma wanavyokuwa *treated*, haioneshi hadhi ya kuheshimu walimu na wanasikitika kwamba wanaowafanyia hivyo wengine ni walimu ambao walitoka nao huku chini, yaani kila wakati wanaulizwa umekuja kufanya nini huku kwa nini usikae skuli huko ah! Mhe. Mwenyekiti, kama amekwenda Wizara ya Elimu kuna huduma anaifuata pale.

Lakini hata katika kuwathamini kwenye ile mishahara yao, unaweza kumkuta mwalimu amesomesha kwa miaka 40 ana *diploma*, mshahara wake anavyompita mwenzake ambaye ameanza *diploma* mwaka huu ni shilingi 1,000/=, yaani kinatizamwa kiwango cha elimu tu hapa na wala siku ile miaka aliyosomesha yote. Kwa kweli haya ni mambo ambayo Mhe. Mwenyekiti, nataka yazungumzwe.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ya *Nursery*. Katika pahala ambapo tunapoanza kuwaandaa wanafunzi ni *Nursery School*. Lakini leo Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha *Teacher's Centre*, Kituo cha Walimu cha *Nursery* ambacho kipo pale Saateni walimu wanakaa chini ndio wanafunzwa hao, mimi nilidhani wanafunzi tu ndio wanaokaa chini tu, kumbe mpaka walimu wenyewe wanakaa chini, hivi tunanyanyua kiwango gani cha elimu Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Lakini hawa Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba wametupwa, Mwalimu Mkuu posho yake yote kwa skuli yote, ambaye huyu ana kazi kubwa zaidi, kwa sababu kule vile vichekechea ni kazi kubwa zaidi kuliko sisi wanafunzi wakubwa analipwa shilingi 5,000/= kwa mwezi Mhe. Mwenyekiti, kweli tuko *serious*.

Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba Wizara ya Elimu watendaji wake wamekuwa hawataki ushauri katika ile Sera yao mpya ya Elimu na haya matokeo yaliyotoka ya kufeli namna kama hii, walimu wamewaita na kuwapa mawazo mengi mazuri na yote yamepuuzwa. Sasa unapimaje tathmini ya mafanikio ya sera hii Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo katika suala hilo.

Suala la ukubwa wa madarasa limezungumzwa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niache hapo.

Jambo la mwisho kuhusiana na skuli ni kwamba skuli kufungiwa *Commercial Metres*, yaani hizi mita za umeme, skuli zimefungiwa mita za biashara na hivi skuli zinafanya biashara gain, na wala haikufungwa mita kulingana na mahitaji kama ya nyumbani, skuli inatoa huduma (*services*) na wala haifanyi biashara pale.

Matokeo yake leo kuna skuli ambazo zinatakiwa zilipe shilingi 60,000/= kwa mwezi, fedha zenyewe zinatoka wapi Mhe. Mwenyekiti na wazee wenyewe ndio hao wanaoambiwa wachangie kila kitu. Mhe. Mwenyekiti, haya nahitaji majibu ya kina la sivyo nitakuwa mgumu kweli kuipitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hilo la walimu na ninaomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anijibu katika suala la Skuli ya Bububu. Walimu Wakuu nimewatetea, lakini kuna baadhi ya Walimu Wakuu kwa sababu ya kuachiwa madaraka, basi wanafanya wanavyotaka Mhe. Mwenyekiti.

Mwalimu Mkuu wa Skuli ya Bububu kila kitu amefanya kama ni chake, amejenga mabati yaliyobakia amechukua kwake, miti anakata anauza na kuchukua yeye, panahitajika maelezo ya msingi na walimu wanapohoji wanahamishwa, wakimripotia Mwalimu Mkuu, basi Maafisa wa Elimu wa Wilaya, hahojiwi yule mwalimu kuitwa na kusikilizwa upande wa pili na kuchukuliwa na kuhamishwa tu. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kuhusu Mwalimu Mkuu huyu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa na wala halichukui muda, kwa sababu hili sina haja ya kulisoma. Naomba kuiuliza Wizara ya Elimu, hivi Wizara ya Elimu watendaji wake wako juu ya sheria na hawafungiki na sheria za nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mwalimu Ameir Makame Ameir wa Uzi Ng'ambwa, huyu alisimamishwa kazi kwa kuambiwa kwamba amemfanya vibaya mwanafunzi wake, lakini kesi imepelekwa Mahakamani, hatimaye kesi ikaamuliwa tarehe 08/09/2011 kwamba huyu mtu hana kosa na ameachiwa huru, lakini Wizara ya Elimu mpaka leo haitaki kumrejesha skuli na kulipwa nusu mshahara.

Matokeo yake *pay slip* ninayo hapa Mhe. Mwenyekiti, anakatwa zile kodi zikeshakumalizwa kukatwa mapato yake yote ni shilingi 151,000/= ndio *gross salary*, lakini akimaliza hayo makato yake yote anakatwa shilingi 15318/= anachobakia kuchukua nyumbani ni shilingi 1,000/=. Huyu Mahakama imeamua kwamba hana hatia na pahala pa mwisho kama mtu anahatia ni Mahakamani, kwa nini Wizara ya Elimu inaendelea kumnyanyasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo ya kina, na kama nilivyosema yale ya vifungu kama nilivyosema ningeyataja moja moja kama unavyoona Mhe. Mwenyekiti nimeshauchukua muda mkubwa nadhani ningefika mpaka saa 2 sijamaliza hapa, lakini nimetoa mifano ninayotaka, kama vile haya yanayohusu sera, hadhi ya walimu na maslahi yao. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama haya Mhe. Mwenyekiti, hatukupewa maelezo ya kina basi bajeti hii itakwenda kulalia paani. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na siungi mkono hoja hii mpaka nipate maelezo ya kina katika vifungu nilivyovitaja. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa anafuata Mhe. Saleh Nassor Juma na baadaye Mhe. Rufai Said Rufai.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusu hoja iliopo mbele yetu. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na kutupa uwezo wa kuondoka majumbani kwetu mpaka hapa katika chombo hichi, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote hatuna budi kumshukuru.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia nafasi.

Kwa hivyo, nianze kwanza kabisa sijaingia kwenye hoja, kwa masikitiko makubwa niungane na wenzangu kutoa pole, kwa wale wote ambao wamepoteza familia zao kutokana na ajali ya meli ya MV. Kalama, ambayo imezama juzi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi natoa mkono wa pole kwa wale wote waliopoteza ndugu zao. Aidha wale wote ambao wameokoka, basi tunawaomba wavute subra na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niwaambie wananchi wa nchi hii ya Zanzibar, kwamba sisi Wawakilishi ni masikini sana, utajiri wetu sisi ni maneno na *Wallahi Laadhimu* ingelikuwa maneno yananunua meli, basi meli ingelikuwa imeshafika hapa tena si moja ni nyingi tu zingelikuwa zimeshafika hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, laiti kama meli inapatikana kwa kutoka roho ya Mwakilishi, kwamba Mwakilishi afe ndio ipatikane meli, basi mimi ningewaomba wananchi wa Zanzibar wanipe dakika tano tu za kushahadia, ili niuliwe halafu wao wapate meli. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kutoka roho yangu mimi na zikaokoka roho za maelfu ya wazanzibari basi naamini roho yangu itakuwa ni sadaka kwao, na laiti kama meli ingelikuwa inanunuliwa kwa roho hiyo, basi yangu ningeitoa na kuomba dakika tano tu za kushahadia na baadaye niuliwe ili wananchi wa Zanzibar wapate meli, lakini masikini meli haipatikani kwa roho. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wananchi waendelee kuvuta subra na serikali hii ni kaidi sana na wala haisikii, na *Inshaallah* sisi tutaendelea kusema maneno hapa, ili iwanunulie meli. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninachotoa tanbihi na kuiomba serikali itusikilize jambo moja, tena hili naomba sana kwa heshima na taadhima pamoja na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa, kwamba hizi fedha tunazopewa kwa ajili ya mafunzo, kama vile semina basi watupe mafunzo ya kuogelea, kwa sababu saa 24 Wawakilishi tumo kwenye meli na sisi, tukishajua kuogelea sisi Wawakilishi basi tutakwenda kuwafundisha na vijana wetu huko majimboni angalau yakitokea majanga kama haya na wao waweze angalau kutapatapa mle melini mana Serikali hii ni kaidi haitaki kununua meli.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Mhe. Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 47 Idara ya Mafunzo ya Ualimu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nijuilishe kwamba mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ambayo bajeti hii katika kamati yetu tumeshaipitisha. Naomba Wawakilishi wote bajeti hii muiboreshe lakini hatimaye muipitishe bajeti hii. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna pahala pa kupongezwa Serikali yetu ni katika idara hii ya mafunzo ya ualimu, kwanza wameanzisha hivi vyuo vitatu ambavyo vinatoa mafunzo ya ualimu. Mimi naamini sana kwamba vyuo hivi vitapunguza idadi kubwa ya ukosefu wa walimu katika nchi yetu. Katika hili Mheshimiwa naiomba sana Serikali pale baada ya kutumia fedha za walipa kodi kuwafundisha walimu basi wale walimu wasiwaachie kuzagaazagaa tu.

Hivi sasa kuna walimu ambao wameshamaliza chuo katika Chuo cha Kiislamu Mazizini hapo, wameshajaza mkataba na utumishi lakini mpaka sasa wanahangaishwa wale nenda huku, nenda huku ukiachia tatizo la vyeti ambalo amelisema Mhe. Hija Hassan. Sasa wale waliokuwa ni safi kwa nini hawaajiriwi, kuna tatizo gani hapa jamani, mimi sioni kama mwalimu keshamaliza mafunzo ya ualimu halafu keshajaza mkataba na Wizara ya Utumishi Serikalini leo anakwenda Wizara ya Elimu anapigwa danadana. Ala! Thamani ya fedha za walipa kodi iko wapi hapa, huyu tumemsomesha kwa fedha zetu za wavuja jasho keshapata taaluma kwa nini asiitumie na kila siku nasema walimu ni tatizo katika nchi hii mpaka mnafika Nigeria kutafuta walimu wa sayansi. Mimi kwanza napingana na wazo la kuja Wanaijeria hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kweli Wizara ya Elimu iko *serious*, wanawajua Wanaijeria hawa, wanajua sifa yao katika uso wa ulimwengu, mmefanya utafiti wa kina na upembuzi yakinifu mkawaona Wanaijeria. Mimi nadhani

tuangalieni upya jamani, mimi nadhani kuwachukua Wanaijeria tukawaingiza nchini kwa kazi hii ya ualimu huku wakisoma baadhi ya mambo yetu humu ndani ikiwemo mitandao ya mapesa ya nchi hii ni tatizo, tutafuteni njia mbadala ya kupata walimu wa sayansi, mmeshakwenda katika nchi nyengine mkakosa? Mimi nadhani ukicheka na nyani mkulima yoyote anaecheka na nyani basi atarajie kuvuna mabua, kabisa kabisa, hapa tunasema hawa ndugu zetu wa damu wee ndugu zetu wa damu leo hivi tukawakumbatie wametufikisha walipotufikisha hapa tulipo, saa hizi mafuta hatuyachimbi alimradi mashaka tu, leo tunachukua na Wanaijeria tunataka kuwatia mbavuni tatizo jengine hilo jamani.

Mimi naishauri Wizara ya Elimu waangalie utaratibu mwengine huo wa Nigeria waachane nao. Wakija Wanaijeria huku wanasomesha huku wanaangalia mtandao wa fedha wa nchi hii, ukija ukifanya mchezo hapa pesa zetu zinachukuliwa zinafanywa nini, tutakuja kuangalia fedha zetu benki hazimo tena hawa jamaa ni adui safi, hili ni tatizo. Kila ukiangalia katika mtandao wa mambo haya ya nini sijui Wanaijeria wako mbele, ulimwengu mzima ukiangalia mambo haya Wanaijeria wako mbele aah! Au wanataka *bench* la ufundi, maana yake Wanaijeria kwa ufundi hatari, kuna watu wanataka urais hapa, labda watu wengine wanataka tena uwaziri mnakwenda kuchukua mafundi, kama ni walimu achaneni nao kama ni mafundi sina la kusema mie.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tuje kwenye maslahi ya walimu. Waheshimiwa kama kuna watu muhimu sana katika kuboreshewa maslahi basi ni walimu, mwalimu huwezi ukamlinganisha na fundi charahani hata siku moja, kwa sababu fundi charahani atakuwa anadili na vitambaa tu, huwezi ukamlinganisha na sonara mwalimu kwa sababu atakuwa anadili na vito tu yeye, mwalimu huwezi kumlinganisha na fundi vyuma kwa sababu yeye atakuwa anazungumzia vyuma tu, mwalimu mimi naweza nikasema ni chemchem tena si ya maji tu, katika chemchem hiyo unaweza kupata maziwa, asali, maji, ukapata kila unachokitaka katika chemchem hiyo. Kwa hivyo, walimu ni hazina, walimu katika nchi zinazoendelea wanathaminiwa, lakini baada ya kufanya upembuzi yakinifu na utafiti wa kina nimeona katika nchi zilizomo Kusini mwa Jangwa la Sahara katika nchi iliyokuwa haiwathamini walimu basi ni Zanzibar.

Mhe. Mewnyekiti, inasikitisha mno kwamba mwalimu wa Zanzibar wa Sekondari hawezi kumudu hata kupata *laptop*, unapotaka kumtayarisha mwalimu wa sayansi lazima umuwezeshe, mshahara wa mwalimu haumsaidii kupata hata buni wakuu wenu wanavaa yeboyebo. Pale Haile-es-Selassie Sekondari mimi nilipokuwa nikisomesha navaa veo yebo yebo *I can't afford to have a boot.*

Wakati wanafunzi wangu wanakuja wana buti Mhe. Mwenyekiti, mimi nina yeboyebo, wanafunzi wanakuja pale wame-*look smart* mimi nikiangalia nina viraka suruali yangu sithubutu kuchochomelea naiweka hivi tu ili kuficha viraka. Jamani hamuwaenzi walimu nyinyi na ikiwa hamuwaenzi mtapata matatizo mimi ndio nikaondoka kusomesha hapa nikenda pale **Popatlal** tu, hapo Bubat learn niliondoka pale Shamiani nikakimbilia Bubat learn Tanga basi nilikuwa nikilipwa shilingi elfu arobaini mwalimu wa sayansi pale Shamiani kufika kule mwanangu shilingi laki moja tena kipindi kile. Pale pale nikaja nikachukuliwa **Popatlal** kupelekwa *Jabal-hiraa Islamic Center* shilingi laki moja na nusu mwanangu kipindi kile nitarudi Zanzibar? Haparudiki na ukikohoa Mwarabu anakuuliza unataka nini, unataka suti au unataka nini? Leo Wizara ya Elimu mwanangu *bus fair* walimu wanachukua miezi mitano hawajaipata anapiga mguu ni pema hapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Wizara ya Elimu kwa kuweza kuwalipa walimu kwa mujibu wa taaluma zao, hili nawapongeza sana. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna walimu ambao ni wazee, kuna walimu ambao wamemaliza darasa la nane miaka ya nyuma sana, kuna walimu waliomaliza *Form III* wakenda pale Nkrumah kufanya cheti cha *grade B*, lakini wana uzoefu mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba ongezeko la mishahara la mwaka huu halikuwanufaisha walimu hao badala yake limewaathiri.

Mhe. Mwenyekiti, nina barua hapa naomba kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu sana nakuomba uniruhusu niinukuu ya Mwalimu Mkuu mmoja. Mhe. Mhe. Mwenyekiti, jina nalihifadhi, inasema hivi:

"YAHUSU LALAMIKO LA MSHAHARA.

Kwa wingi wa heshima naomba uhusike na mada iliyopo hapo juu, nilimaliza masomo yangu Kidato cha Nne mwaka 1973 nilisomea ualimu kwa muda wa miaka miwili mwaka 1974/1975 katika Chuo cha Ualimu Nkrumah. Niliajiriwa kazi ya ualimu nikiwa mwalimu niliyekwishasomea kuanzia tarehe 1 Januari, 1976, mwezi wa Septemba, 1990 niliteuliwa kuwa Mwalimu Mkuu", sitaki niitaje hiyo skuli.
"Nilipandishwa daraja na kuingizwa katika ngazi ya utaalamu kwa barua yenye *reference* 7 EPP154/3/90 ya tarehe 01/06/1995 na mshahara wangu ulikuwa shilingi 14,055 (kiwango cha MW II)".

Alipandishwa daraja huyu kwa barua niliyoitaja naomba niinukuu tena barua hiyo Mhe. Mwenyekiti, ambayo imetiwa saini.

Hii barua ya kumuingiza mwalimu katika ngazi ya utaalamu ambayo inasema kwamba,

"KUINGIZWA KATIKA NGAZI YA UTAALAMU.

Nina furaha kukuarifu kwamba umepandishwa daraja kuingizwa katika ngazi ya utaalamu mshahara wako hivi sasa utakuwa shilingi 14,055 MW II, marekebisho hayo yanaanza mwezi wa Juni, 1995. Wizara imechukua hatua hiyo ya kukupandisha daraja kutokana na jitihada uliyoonesha katika kuutumikia umma.
Ni matumaini yangu kuwa utaipokea heshima hiyo kwa moyo mkunjufu na kwamba utakuwa ni motisha ya kuzidisha bidii katika utumishi wako. Nakupongeza na nakutakia kila la heri.
Kombo Hassan Juma
Afisa Mdhamini,
Afisa Wizara ya Elimu Pemba".

Huyu alipandishwa daraja baada ya kuonekana utumishi wake anawatumikia watu katika utumishi uliotukuka basi Afisa Mdhamini na wataalamu wake waliomzunguka wakampandisha daraja huyu mwalimu kwa barua hii niliyoitaja, leo la kushangaza anasema kwamba katika barua yake ile ya mwanzo, katika mabadiliko ya Oktoba yaliyofanyika mwaka 2011 kilichofanyika upande wangu mshahara wangu ulipunguzwa badala ya kuongezwa. Mshahara wangu uliopunguzwa ni kutoka shilingi 241,005/- hadi kufikia shilingi 219,000/-, mshahara nliopewa mwezi wa Disemba ni kiasi hicho cha shilingi 219,000/-. Kwa hivyo naomba mshahara wangu uangaliwe, sababu zilizonisababisha mimi nipunguziwe badala ya kuongezwa ni ipi?

Sasa Mhe. Mwenyekiti, uone jinsi ya Mwalimu Mkuu anavyonyanyasika huyu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani ukipanda mchongoma usitegemee kuvuna nanasi siku zote, ikiwa umemdharau mwalimu basi ina maana unateremsha elimu katika nchi, usitegemee hata siku moja kupandisha elimu kwa kuwadharau hawa walimu lazima tusikilize kilio cha walimu na haya makosa hawa ni wengi, mimi ninazo zaidi ya ishirini lakini natoa *sample* barua moja tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika hili Wizara ya Elimu isikie kilio cha walimu, Wizara ya Utumishi Serikalini vile vile isikie kilio cha walimu hawa walimu ndio msingi lazima tuwaangalie ili tuweze kupata maslahi hapo mbele.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo jengine lililojitokeza katika maslahi ya walimu, kama kuna Wizara ambayo mpaka sasa hivi imetumia muda mwingi

kunidanganya mimi basi ni hii Wizara ya Elimu ishanidanganya sana. Nilikuwa natetea maslahi ya walimu waliosomea *Teachers Advancement Program (TAP)* nikawahi kuuliza swali hapa na nikenda kwa watendaji kule ofisini basi siku hiyo niliambiwa katika suala langu kwamba walimu hao maslahi yao yapo karibuni huu ni mwaka mmoja na nusu. Kama mtakuwa na kumbukumbu niliuliza swali la nyongeza kwamba, haki ikichelewa kutolewa ni sawa sawa na kwamba haikutolewa kabisa. Sasa mimi hapa nataka nikizuie kifungu hiki mpaka Waziri aje anambie ni lini atawalipa walimu hawa waliomaliza *Teachers Advancement Program* ambao alisema atawalipa ni lini atawalipa na aliahidi atawalipa ***arrears*** zao tangu walipomaliza *course* hii mpaka leo hii mwanangu.

Mhe. Mwenyekiti, tasnia ya taaluma katika nchi ni tasnia kubwa sana na inahitaji elimu ya Zanzibar iwe *harmonized* kwa sababu visiwa vyetu ni viwili. Watendaji wa Wizara ya Elimu lazima wahakikishe wanajenga *unity* katika tasnia hii ya taaluma katika visiwa viwili vyote, sio ku-*harmonize* taaluma tu, lakini hata utendaji mwanangu ulikuwa unahitaji kuwa sawia baina ya Unguja na Pemba.

Lakusikitisha Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma): Mhe. Mjumbe una dakika chache tu za kumalizia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nitazitumia vizuri. La kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, inaonekana Wizara ya Elimu wanawabagua walimu baina ya walimu wa Pemba na walimu wa Unguja. Nataka Waziri atakapokuja anijibu ni sababu gani inayopelekea mitihani isainishwe Unguja tu Pemba isisainishwe na kule mabanda yako, nyumba za kukaa walimu kutoka Unguja wakenda kusainisha ziko, umeme uko, hali ya hewa nzuri marashi ya karafuu yako Pemba, ni sababu gani ambazo hawendi kule kusainisha mitihani wanasainisha Unguja tu. Hilo aje anijibu Waziri.

La pili ni sababu gani ambayo nadhani Prof. Mohammed Haji Khalid pale asubuhi alitoa takwimu zilizoonesha kwamba, katika walimu 847 waliosainisha pamoja na kusimamia mitihani kipindi hiki, walimu 813 walitokea Unguja na hawa 34 walitokea Pemba ni sababu gani zilizopelekea tofauti kubwa kiasi hiki jamani. Ni sababu gani au tuseme hawana *qualification* au vipi, kwa sababu pesa zinazotumika kulipwa hawa walimu wanaosainisha mitihani Mhe. Mwenyekiti, ni pesa za walipa kodi ambapo walipa kodi hawa ni kutoka Unguja na Pemba sasa kwa nini muwabague kiasi hicho walimu hawa huku mtoe 34, huku mia nane na zaidi, Waziri nataka na hili anijibu. Hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa inatakiwa *national unity*

iwepo na kuwe na umoja hasa ndani ya visiwa vyetu. Kwa hivyo, naomba hii unieleze Mhe. Waziri.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Mafunzo ya Amali, lakini nahofia muda kwanza niende Chuo Kikuu cha Taifa haraka haraka kama nitawahi nitakwenda na huko kwengine.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA* ni chuo pekee cha Serikali hapa nchini. Mhe. Mwenyekiti, kama kuna kitu cha kukienzi na kukitunza ni hiki Chuo cha SUZA. Hawa wataalamu waliokuwepo SUZA napenda niwapongeze sana kina Profesa Idrissa Rai na Dokta Hamad na wataalamu wetu wote pale kwa kuwa makini katika kutoa taaluma. Lakini jambo la kusikitisha Mheshimiwa hawa watu wa Chuo Kikuu cha SUZA wao wanafanya programu zao kwa mujibu wa mazingira.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Wanawake na Watoto, tulipotembelea pale mwaka jana hawa waliona kama kuna mabadiliko ya tabia nchi na wakaona kwamba kisiwa wakati wowote cha Mhe. Haji Faki Shaali kitazama, wakasema katika hili ili kunusuru hili ni lazima tuanzishe *program* ya digirii ya *environmental science* akaandaa *program* yao ili iwasaidie wananchi kupata kuhifadhi mazingira yao wakitoa wataalamu wale lakini Serikali imeshindwa kuwa *supports*.

Mwisho walitaka kuisaidia Serikali hawa watu wa SUZA kwa kuanzisha *faculty of Agriculture*, Pemba *branch* ili kuweza kufanikisha hili suala la mpango wa kubadilisha kilimo. Lakini Mheshimiwa mpaka sasa hivi *program* zile haziku *supports*. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru *Allah* kwa kujaalia jioni hii kupata nafasi hii adhimu kuweza kutoa mchango wangu japo kuwa mfupi kutokana na muda.

Kabla ya hapo na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Tumbe sina budi kuwatakia na kuwapa mkono wa pole wale wenzetu wote waliofikwa na msiba huu ambao na mimi binafsi katika jimbo langu umenigusa sana. Kwa kushirikiana na majimbo mengine Zanzibar nzima na kwa Tanzania na *East Africa* tunawapa pole wote wale ambao wamepatwa na msiba huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kuiombea Wizara hii ya Elimu katika asilimia 25 iliyotoa Serikali ya mishahara, tuseme kwamba katika Wizara mama basi ni Wizara ya Elimu. Wizara hii ndiyo ukombozi wa Wizara nyengine mbali mbali na maendeleo ya nchi. Kwa sababu huwezi kupata uchumi bora kama

huna wataalamu wenye kusomea mambo ya uchumi. Huwezi kupata madaktari bora kama hawakupita katika sehemu ya elimu. Nahisi mimi kwamba wizara hii ndiyo wizara iliyochini kabisa, imefanywa kama vile mfinyanzi, kawaida ya mfinyanzi hufinyanga vyungu vyake lakini katika matumizi yake binafsi cha kutumia yeye huwa kinamshinda.

Wizara hii ningeioyomba sana Serikali inapoweka asilimia 25 za mshahara basi itenge asilimia 5 kwa niaba tu ya Wizara ya Elimu. Hawa ndio waliotuwezesha, hawa ndio waliofanya wengine kuwa mawaziri, wengine Maraisi, wengine madaktari. Kwa hivyo kama hatutowapa kipaumbele Wizara hii ya Elimu, itakuwa siku zote nchi yetu haipigi hatua ya maendeleo. Ndio ukakuta Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wenye elimu zao wanakataa kwenda Wizara ya Elimu. Kwa sababu kilichopo hapo zamani ilikuwa ni chaki na mabuku. Sasa hivi yote hayo yanakosekana, ile chaki wahudumikie wanafunzi na wazee wa wanafunzi, hakuna motisha wa aina yoyote. Ni vyema Serikali ikaangalia kwa jicho la huruma na wakawapa motisha walimu na Wizara ili iweze kupambana na hali ngumu hii ya elimu.

Mhe. Mwenyeki, nikitoka hapo nataka nije katika ukurasa wa 9 kifungu cha 21 katika elimu ya Maandalizi. Nakumbuka miaka ya hivi karibuni Wizara hii ilianzisha elimu ya maandalizi na ilikuwa kuna skuli tunaziita “tutu”. Skuli hizi zimo katika vijiji vyetu mbali mbali hapa Zanzibar. Lakini wanafunzi hawa bado wanaishi katika miembe na maeneo ya miti mengine, hawana mabanda ya kusomea, walimu wenyewe ni hivyo hawana mshahara, posho wanalopata walimu hawa nasikia kwamba ni chini ya Sh. 20,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali ngumu ya maisha tunaliyonacho mtu anampa elfu ishirini kwa mwezi, zimsaidie nini pesa hizi, elfu ishirini mtu unatumia kwa siku moja tu. Leo mtu unampa mwezi mzima shilingi elfu ishirini, hana shughuli nyengine anayoifanya isipokuwa kushughulika na watoto wale wadogo. Halafu mazingira wanayofanyia kazi hayaridhishi ni ovyo kabisa. Mimi nasema kama huu mradi ulileltwa kwa niaba ya kuwanyanyua vijana wetu wadogo wadogo. Kama Serikali imeshindwa, kushindwa si vibaya ni kunyanyua mkono, wakawatangazia wale walimu pamoja na wahusika kwamba skuli ya msingi hii sisi kama Serikali basi tunaondosha mkono wetu.

Mhe. Mwenyekiti, inachukua miezi imitatu, mine, mitano au site elfu ishirini hizi bado hazijapatikana. Kwa kiasi fulani ni kuwadhalilisha walimu wetu hawa. Kwa hivyo naiyomba sana Wizara kama bado wanataka kuziendeleza zile skuli basi waziendeleze na wawaone kama na wale ni binaadamu wanahitaji kuishi, kunywa na kuvaa na hili posho lililowekwa kwa kweli halendi tena na wakati huu tulionao.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika elimu ya msingi kwa kiasi fulani wananchi kwa kushirikina na serikali yao wamepiga jitihada kubwa ya kuongeza madarasa katika maeneo mbali mbali. Mpaka hivi sasa baadhi ya skuli nyingi za msingi inayosubiriwa ni Serikali kukamilisha majengo kwa ajili ya kuezeka na kuyaingiza saruji na mambo mengine. Lakini maeneo mengi tayari mskuli hayo hapo. Lakini pia tuishukuru Wizara ya Elimu wamepita hatua kwa kiasi fulani katika kuyaezeka haya mabanda kwa kuyatia saruji na mambo mengine. Kwa kweli wamepiga hatua. Juu ya hayo ni vyema kuhakikisha kwamba zile nguvu za wananchi washezozitoa basi Wizara inajikaza kuhakikisha mabanda yale yameezekwa na kupewa huduma nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo lililopo jengine ni baadhi ya shule zetu bado zipo msingi na Sekondari pahali pamoja, hili linakuwa ni tatizo kumfanya mwalimu mkuu moja ashughulikie mitihani ya darasa la saba, mitihani ya darasa la kumi na mitihani ya darasa la kumi na mbili. Kwa kweli hii ni kazi ngumu. Kila kazi mtu anahitaji kupata muda wa mampumziko ili kuweza kuitulazinisha akili na kujiandaa na mambo mengine.

Kwa hivyo tukiweka bado tukiwa na ulazima huu, hili ni tatizo ambalo lipo katika skuli yangu ya Sizini, bado skuli ya hii hakujawa na ubagufu baina ya sekondari na msingi. Kwa hivyo ningeliomba sana wizara kwamba hili tatizo waliondoshe wawasaidie hawa walimu, kwa sababu walimu wenyewe ni kidogo wana upungufu mkubwa lakini majukumu yaliopo ni makubwa zaidi.

Kwa hivyo ningeomba sana wizara hii suala hili walihangaikie na walishughulikie na walipe kipa umbele ili walimu hawa waweze kufanya kazi zao vizuri na watu hawa wa msingi waweze kushughulikia mambo yao ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, tokea asubuhi wenzangu wamechangia mambo mengi hapa kuhusu Wizara ya Elimu na suala zima la kufutiwa mtihani mwaka jana, lakini mpaka tunaingia kwenye bajeti hii hatujaona dalili zozote zilizochukuliwa na wizara hii kwa wale walimu waliosababisha matokeo haya. Kwa hivyo mimi ningelimuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze wizara yake imechukua hatua gani kuhusu sakata zima la mitihani iliyofanyika mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika skuli zangu za Jimbo la Tumbe. Mhe. Mwenyekiti, tuna tatizo katika Skuli ya Tumbe muda mrefu kuhusu suala zima la kuanzisha darasa maalum hasa wakati ule wa maandalizi ya mtihani. Tatizo la skuli ya Tumbe ni tatizo la umeme, ni muda mrefu skuli hii bado

haijapata umeme katika maandalizi ya vijana wetu wa darasa la saba, la kumi na la kumi na mbili.

Na ni kweli kwamba eneo lilipo skuli hii kama wizara itajiandaa basi watoto wetu pale wanaweza kusoma vizuri, kwa sababu ni eneo ambalo hapana vishawishi lakini inabidi hivi sasa hapana umeme, wanafunzi watarajiwa wa mitihani waende vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, vijijini kuna mambo mengi. Kwa hivyo bado ninaiomba wizara skuli hii pia waiangalie. Hii skuli hii inahitaji kuwa na umeme na muda mrefu tena. Kwa hivyo kwa nguvu zao zote wahakikishe skuli ile nayo imepata umeme na wanafunzi wetu wanapata kuweka darasa maalum pale ambalo la kuweza kujichukulia masomo ili unapofika wakati wa mitihani tuweze kuzalisha wanafunzi kwa wingi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Zanzibar baada ya kupanda kwa elimu, kila miaka tunayokwenda elimu Zanzibar inashuka. Mimi huwa ninajiuliza tatizo ni nini. Ni wanafunzi, ni walimu, ni wazee, kamati za skuli au ni kitu gani. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nikiungana na wenzangu wanaposema kwamba kwa upungufu wa walimu mpaka sasa Wizara ya Elimu ikataka kuleta walimu kutoka Nigeria, nahisi hapa tutakuwa hatujawatendea haki Wazanzibari.

Ni vyema wanaolipa kodi kuwalipa walimu ni Wazanzibari na walimu wa kuwafundisha Wazanzibari masomo ya sayansi na hesabati, mimi ninadhani si maskini wa masoko hayo na walimu hao. Si dhambi mwalimu anayestaafu kazi tukamchukua kwa mkataba maalum mwenye sifa hii ya sayansi na hesabati wakaweza kuwasaidia Wazanzibari ndugu zao.

Mhe. Mwenyekiti, utakapowaleta hawa Nigeria, wanafunzi watakuwa na kazi mbili mpaka tatu. Kwanza kumfahamu Mnigeria kiingereza chake, Kiswahili chake, mwenendo wake na tabia yake. Hiyo ndio kazi itakayomkumba Mzanzibari mwanafunzi.

Kiingereza cha Kizanzibari basi tunaelewana lakini ukimleta Mnigeria hapa, mimi ninahakikishia kwa muda wa miaka miwili hatujapata mwanafunzi. Kwa hivyo ni vyema Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri watu wenye taaluma hii Zanzibar tunao, hawa ni wenzetu wapewe hizi nafasi waweze kuwasaidia ndugu zao.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nichukue muda mrefu kutokana na muda na kuna wenzangu wanataka kuchangia. Kwa hivyo hayo machache iwapo Mhe. Waziri atakapokuja kutuelimisha haya na kunipa lini skuli yetu ya Tumbe

itapata umeme basi mimi sina matatizo na hotuba yake hii. Naunga mkono hoja.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwenye Wizara yetu hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kabla sijatoa mchango wangu pia ninataka nitoe rambi rambi zangu kwa matokeo ya ajali ya meli iliyotokezea jana na juzi ile. Kwa kweli tunawapa pole wote wale waliokuwa wamefiwa na watu wao na wale ambao wengine waliokuwa wameokolewa lakini hali zao hazijakuwa nzuri. Pia tunaomba Mwenyezi Mungu wote wale waliopata faradhi Mwenyezi Mungu awasamehe na awalaze mahala pema peponi.

Lakini pamoja na hilo, tunataka kuishauri serikali kwamba kutokana na hili ambalo limetokezea hii ni mara ya pili au mara ya tatu kwa ajali mbali mbali ambazo zimetokezea, ningeishauri serikali kwamba kwa historia ya Zanzibar tunahitaji kuwa na meli ambayo iliyokuwa na uwezo wa kukabili mawimbi makali ya hapa Unguna pamoja na Pemba.

Hali ya historia ya Zanzibar tunajua sote kwamba meli za hapa ni lazima ziwe kubwa ambazo zinaweza kukabili mawimbi makali yaliopo Nungwi pamoja na Dar es Salaam ambapo tunakwenda mara kwa mara. Kwa hivyo ningeishauri serikali suala hili la kuweza kupatikana meli iliyokuwa kubwa ya kuweza kukabili matatizo haya.

Nikiingia katika mchango wangu wa sasa hivi ni kwamba nikitaka nizungumzie juu ya suala zima la upungufu wa walimu. Mhe. Mwenyekiti, katika maskuli yetu yote kwa wakati tulionao hivi sasa tuna upungufu wa walimu na hili linaeleweka na ni suala la muda mrefu.

Upungufu huu hasa unakabili kwa masomo maalum. Kuna masomo haya ya sayansi, *physics*, *maths*, *biology*, katika upande wa sekondari, huo ni upungufu mkubwa sana. Hili linawafanya wanafunzi wetu wengi wasiweze kukabili mitihani yao ya sekondari kutokana na kutokuwa na uwezo walimu wa kusomesha masomo hayo.

Masomo haya ya *physics*, maths pamoja na *biology* ni masomo muhimu sana lakini mara nyingi katika maskuli yetu utakuta walimu hawa hawapatikani ni adimu kabisa. Upungufu huu upo na zaidi ya hivyo hata katika sehemu ya msingi vile vile kuna upungufu wa walimu. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri hili suala akaliangalia kwa vizuri zaidi ili upungufu huu wa muda mrefu uweze kuondoka.

Ukitazama hata ile ratio wise ambayo walimu hawa wanapata kila siku, *ratio* yao inakuwa si nzuri. Utakuta mtu mwalimu ambaye anatakiwa yeye awe na idadi maalum ya masomo inabidi awekwe na vipindi vingi zaidi kwa sababu ya kufidia wale wengine waliokuwa hawapo. Kwa hivyo huo ni mzigo kwa kawaida mwalimu anatakiwa apate vipindi vya mapumziko kuweza kusahihisha kazi zake.

Sasa kama mwalimu unamtwika vipindi vyote hana mapumziko hata ya period moja, hii inakuwa ni suala gumu sana. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri aangalie idadi ya vipindi kwa walimu kwa wiki ni kiasi gani ambapo anavyopewa.

La pili Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikitaka kutizama suala zima hili la upungufu katika skuli za sekondari. Inaonekana vile vile katika sekondari au elimu ya juu kama kuna upungufu wa walimu. Siju walimu hawa waliokusudiwa, hawa waliotakiwa kutoka nje walikuwa na sifa zipi ata waje kutusaidia. Ni lipi lililokuwa zito sana ambalo sisi hatuwezi kulikabili. Hata kwa majirani zetu waliopo Dar es Salaam ninafikiri tunaweza tukapata walimu wa aina hiyo, lakini kuingiza watu ambao kidogo lafdhi yao si nzuri, yaani tunaita pronunciation ya lugha ya kiingereza, kwa kweli itatutaabisha kwa wao.

Kwa hivyo watu kama hawa, Wazanzibari wanasifikana sana kwa matamshi ya lugha ya kiingereza lakini kwa watu wanaokuja kutoka Nigeria, matamshi ya kiingereza hayapo sahihi na mazito sana na yanatapisha mdomoni. Kwa hivyo haidhuru wameshaletwa na wapo tunao, lakini hii ni hali iliyokuwa kidogo si nzuri.

Lakini jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti, ambalo ninataka kulizungumza ni suala la ajira ya walimu wa sayansi. Kwa kweli si vibaya kupendelea zaidi kufanya ajira ya walimu wa sayansi. Lakini tuangalie kama tunatoa ajira kwa walimu wa sayansi tu peke yao, hatutoi ajira kwa walimu wa masomo ya art, hii kidogo itakuwa si halali. Kwa sababu humu ndani ya maskuli kila mmoja ana uwezo wake wa kufahamu, tumewakubali waiingie katika maskuli yetu ya msingi, sekondari mpaka elimu ya juu, tuna watu wa aina mbili, tuna watu wa sayansi na watu wa art.

Lakini leo ikiwa fursa za namna hizo, *privilege* kubwa zinakwenda kwa walimu wa sayansi, walimu wa art hawakupewa, wanafunzi wale watakuwa vipi. Hisia za wanafunzi ndio tutakazopata hivyo lakini hisia za walimu ambao wanaosomesha masomo ya art watavunjika moyo, wakiona kwamba wanafunzi wao wa art hawachukuliwi wanachukuliwa watoto wa masomo ya

sayansi tu peke, hii itakuwa si suala zuri. Kwa hivyo katika hizi ajira ambazo tunazitegemea za walimu wa sayansi pia hapa Mhe. Waziri nimuombe afikirie zaidi na walimu wa art vile vile kuweza kuwapa ajira. Ingawa tunasema kwamba walimu wa art au masomo ya art hivi sasa hayana soko sana kuliko masomo ya art, lakini sasa tutafanya nini na sisi katika curriculum zetu tunaweka masomo yote haya ya sayansi na art.

Kiustaarabu ni lazima na wao tuwape ajira tusiangalie upande mmoja tu. Ningemuomba Mhe. Waziri kwenye suala hili akaangalie vile vile ajira ya wale wenye high competency ya kusomesha au ya elimu yao ya juu wakapata nafasi ya kuendelea kuwa na wao ni walimu wa art, ambao hawa vile vile wanaweza wakawasaidia wale walimu ambao wengine watakuwa wamestaafu baada ya muda wao kufika, wanaweza kuchukua nafasi zao. Haina maana kwamba wao tusiwachukue kwa sababu walimu wa art wapo wengi, lakini *periodical* kila mwisho wa mwaka tunatoa walimu chungu nzima ambao wanastaafu na miongoni mwa wanaostaafu ni walimu wa art wamo. Kwa hivyo hakuna ubaya walimu na art nao wakaajiriwa.

Nikiondoka hapo nitaingia kwenye suala jengine la uhaba wa vyumba vya kusomea. Mhe. Mwenyekiti, suala hili la uhaba wa vyumba limekuwa ni maarufu sana. Vyumba ni kidogo idadi ya wanafunzi ni wengi sana katika kila skuli hali ndio hiyo.

Sasa hatujui kwa nini mawaziri wote wanaoingia hili suala mpaka leo hawajataka kulifikiria. Mimi ninahisi kwamba kama suala hili tutaendelea litaendelea bado kuongeza idadi kubwa ya wanafunzi, yaani kutakuwa na msongamano mkubwa sana wa wanafunzi katika darasa. Hii inampa dhiki mwalimu katika kusomesha kwa sababu mwalimu naye ni binadamu na mwalimu naye anataka watoto wake wafanikiwe wawe mahodari na wajue kila kitu.

Lakini kila idadi kubwa ya wanafunzi ndani ya darasa ni ule ugumu wa mwalimu kuweza kutoa huduma kwa mwanafunzi. Kwa sababu watoto wakiwa wengi ina maana unapunguza huduma mwalimu kwa ajili ya wanafunzi wake. Kwa hivyo hili suala la idadi kubwa ya watoto hufikia 80 au 90 au mpaka 120 kwa darasa, hasa katika sehemu ya madarasa ya chini ambao kule kuna *junior work*. Mwalimu wa kawaida anatakiwa kila mwanafunzi aweze kukaa naye kumuelekeza kumpiga mstari na kila mwanafunzi lazima ampitie.

Sasa wanafunzi watakapokuwa wengi katika darasa, hivyo kweli mwalimu ataweza kuwahudumia wanafunzi wale kuweza kuwapitia, mwenye matatizo akamjua, aliyeshindwa kuweza kuandika aweze kumrekebisha hawezi

kumjua. Atasomesha hivyo hivyo kwa mujibu wa wakati wake na *period* yake ikimalizika itabidi atoke nje.

Kwa hivyo mimi ningemuomba Mhe. Waziri kwamba hivi sasa kwa mwaka huu amekamata Wizara ya Elimu tunataka tumuone yeye na juhudi zake kupunguza idadi ya wanafunzi au kuongeza idadi ya vyumba. Hawezi kupungua hawa wanafunzi katika darasa ikiwa hatukuongeza idadi ya madarasa. Tuongeze idadi ya madarasa ili tupunguze wanafunzi katika madarasa angalau mwalimu ajisikie aone raha. Kwa wenzetu idadi ya wanafunzi 20 mpaka 25 ni kitu cha kiasi, lakini kila idadi ya wanafunzi wakiwa wengi ndio matatizo ya walimu kutoweza kuwafundisha kwa vizuri wakafahamu na wakaweza kumuuliza maswali. Kwa sababu kuna wakati mwalimu anataka yeye aaulizwe maswali na wanafunzi lakini anaona pale kwa wakati wake alionao na idadi ya wanafunzi itabidi asomeshe hivyo hivyo.

Lakini tuangalie vile vile kila idadi kubwa ya wanafunzi, *quality* ya *education* inakuwa si nzuri. Kila mtu anaamini hivyo kwa sababu msimamizi wa darasa lile ni mtu mmoja, mtu huyo mmoja aweze kusimamia mambo yote, kuweza kuwasahihishia kwa uzuri na kuweza kuwafahamisha. Kwa hivyo ile quality ambayo inapatikana ambayo mwalimu alitakiwa yeye atoe huduma yake kwa kila mwanafunzi hii itakosekana haipatikani kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi.

Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri kwenye suala hili la msongamano wa wanafunzi katika darasa basi ningelimuomba afanye utaratibu apite yeye mwenyewe aone ile hali halisi. Wanafunzi hawa pia inatokezea mara nyingi hawana hata vikalio wanakaa chini.

Katika sheria za kuandika kukaa chini ni moja katika sheria mbovu, kwa sababu ile anapinda mgongo, ina maana katika maisha yake mwanafunzi ikiwa unamsomesha kwa miaka minne au mitano mtoto anakaa chini basi ile itakuwa ni moja katika tabia yake hata akiwa mtu mzima na nyumbani kwake atakapokuwa itakuwa maandishi yake ya kuinama ya kuandika. Kwa hivyo hilo si jambo zuri.

Unatakiwa hata ukiwa dereva wa gari, unatakiwa usipinde mgongo, mgongo wako unatakiwa uwe straight. Sasa mgongo hauwezi kupatikana straight ukiwa dereva ikiwa mzembe hujui wewe unatakiwa ufanye nini ukiendesha gari kwa kupinda mgongo utakuwa na matatizo. Kwa hivyo ni sawa sawa na mwanafunzi aliyeopo darasani, hatakiwi kupinda mgongo wakati akiandika. Kwa hivyo hili ni suala Mhe. Waziri uliangalie sana.

Jambo jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti, ninataka nilizungumzie ni suala zima la uhamisho wa wanafunzi. Mimi kuna hili suala ambalo linanistajaabisha sana kwa nini uhamisho wa wanafunzi kutoka Pemba kuja Unguja haupatikani. Kuna complains nyingi sana za wazee kwamba sisi tunapokwenda Wizara ya Elimu, tunapotaka kuhama na watoto wetu tunakuja Unguja, uhamisho wa watoto hatupewi. Sasa ina maana ikiwa mwanafunzi hapewi uhamisho akaondoka na wazazi wake, ina maana yule mzazi unamfunga pengine maisha ni magumu, anataka kuondoka akatafute mahala pengine ambapo atapata maslahi ya kimaisha.

Kwa hivyo mimi hili suala Mhe. Waziri ningelikuomba, hii tabia ya kuwazuia, kwa nini wazuiliwe watoto kuhama. Kwa nini wasije Unguja, mbona wanafunzi wa Unguja wanatoka wanakwenda kusoma Pemba, wanafunzi wa hapa Unguja wanatoka wanapata uhamisho na wanakwenda Pemba wanasoma na wazee wao wanakwenda nao pamoja au peke yao, lakini mwanafunzi wa Pemba kutoka Pemba akaja Unguja hapewi uhamisho, kwa nini iwe hivyo. Hilo ni suala ambalo Mhe. Waziri utakapokuja hapa uje unieleze kwa nini wanafunzi wa Pemba na wazee wao wanapotaka kuondoka kuja huku hawapewi uhamisho, *why*.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, ninataka nizungumzie suala zima la posho la walimu. Hili suala hili limegusiwa na kila mtu na si vibaya kila mtu akaligusia kwa sababu sisi ndio tunaopata malalamiko ya walimu wetu. Kwa sababu mimi sioni sababu kwa nini mwalimu akadharaliwa kiasi hicho na kwa nini na mwalimu ni mtu ambaye tunayemtegemea sana kwa maisha ya wanafunzi wetu. Yeye ndiye ambaye tunayemtegemea kwa wanafunzi atoe quality nzuri.

Lakini leo motisha inakuwa hapati, anapewa shilingi elfu kumi au kumi na tano, what's fifteen thousand ni kitu gani shilingi kumi na tano kwa kumpa mwalimu. Aangalia mwalimu mkuu huduma ambao anaitoa, aangalia kazi ya mwalimu aliyenayo, ana dhamana ya skuli, watoto elfu moja au elfu mbili alionao si watoto kidogo, ana dhamana ya wanafunzi, ana dhamana ya walimu, ana dhamana ya wanafunzi kila mmoja aje kwa wakati, ana dhamana ya kuangalia kazi za wanafunzi, ana dhamana ya kuangalia wanafunzi wanakuja katika hali ya usafi na wanafanya kazi zao. Mwalimu Mkuu hakai katika darasa kutwa anaangalia kuna matatizo chungu nzima.

Hivyo mimi ninahisi kwamba kama ikiwa posho la mwalimu mkuu ni dogo, hivyo kweli atakuwa na motisha ya kufanya na majukumu bado tunampa sisi kujenga maskuli, aisimamie skuli katika skuli yake kama mbili au tatu anajenga, iwe kazi yake kutwa anakwenda na akirudi. Angalau hili posho ni dogo sana jamani, tuangalie majukumu aliyonayo mwalimu mkuu, tuangalie

majukumu mengine ambao yeye katika wizara anayo, anatakiwa kupeleka return za maafisi, inabidi atoke skuli aache siku ile, akirudi ana majukumu chungu nzima, yaliyotokezea yote asawazishe yeye. Basi alau haongezwi akapewa motisha zikaongezwa hizi pesa kidogo na yeye akajisikia akafanya kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa dakika 5 malizia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ninalotaka kulizungumzia haraka haraka ni maslahi ya walimu. Mhe. Mwenyekiti, maslahi ya walimu ni maslahi duni kabisa. Kwa kweli bado mishahara ya walimu haikidhi haja. Tunaomba Mhe. Waziri walimu wana kazi kubwa sana na ni walimu hawana kazi nyengine ya kufanya zaidi ya ualimu. Hawezi mwalimu baada ya kazi ya kusomesha asubuhi na jioni, halafu akatoka akenda kufanya kazi nyengine ya ziada angalau ya kwenda kuongeza pato. Hata shamba ya muhogo hana.

Basi angalau haya maslahi yake mwalimu yawe mazuri kutokana na majukumu tuliyompa na idadi ya wanafunzi wengi na kusimamia wanafunzi. Angalia sisi wazazi mtoto mdogo tu unaweza kumfukuza nyumbani, nenda skuli huko! Angalau na mimi nipumzike.

Sasa wewe unampelekea mtu, wewe mwenyewe hutaki kuwalea akalee mwalimu kule. Hilo ni jukumu kubwa sana. Kwa hivyo walimu wana kazi kubwa sana na kwa kweli maslahi yao ni duni, bado Mhe. Waziri tunakuomba, hichi walichokipata kwa walimu bado ni kidogo na tunakuomba ufanye angalau fungu la huruma kwa walimu wapate scheme of service hasa kuna walimu ambao wameumia kwa muda mrefu kutokana na scheme of service. Kupandisha mshahara bila ya kutengeneza scheme of service hapa ni kuwauwa walimu. Hii itakuja bado mwalimu mkongwe apite na mwalimu aliyeingia leo kwa sababu hakuna *scheme of service*. Ile *scheme of service* kutokana na daraja yake itaweza kumsaidia kupandisha mshahara wake ukawa mkubwa asipite na mtu mwengine. Lakini tukiweka nyongeza tu ya kitu, kila siku itakuwa yeye anapitwa. Kwa hivyo maslahi Mhe. Mwenyekiti, ni magumu.

Lililobakia Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie ni suala zima la mikopo. Mhe. Mwenyekiti, suala hili la mikopo limezungumzwa katika kipindi kilichopita na limeonekana athari kubwa za mikopo hii. Kwa kweli tunaitegemea Wizara ya Elimu iweze kuwasaidia wanafunzi wetu.

Wanafunzi kwa kweli ni wengi na wanafunzi wengine ni wazuri lakini wanashindwa kupata nafasi ya kuendelea kutokana na mikopo. Tunajua kwamba mikopo ipo Bodi ya Mikopo ambapo bodi hii ndio inayosimamia wanafunzi wote, inasimamia wafanyakazi wote katika bodi hii kuhakikisha kwamba watu wanapata mikopo.

Lakini la kushangaza ni kwamba mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wetu ni kidogo sana wanaopewa, hawapati wanafunzi wengi. Tuangalie kwamba mwanafunzi au mfanyakazi wa serikali anapojaza fomu, yeye fomu ile anainunua na kuna ada nyengine yule itabidi alipe, kabla ya kusajiliwa itabidi kuna mambo chungu nzima inabidi yeye atoe pesa nyingi sana kabla ya hilo suala yeye hajapata na matokeo yake anaweza kuambiwa kwamba wewe hukupata.

Sasa mimi naona bora kuambiwa moja kwa moja tu wewe hupati au utapata kuliko kuja mafomu ya gharama kubwa na halafu yeye asiweze kupata kitu chochote. Kuna gharama nyingi sana na pesa tunaona kwamba pesa za mkopo zinazotolewa ndani ya wizara yenyewe ni kidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Hivyo ningekuomba Mhe. Waziri suala hili alisimamie kwa vizuri zaidi ili wanafunzi wetu kwa baadae waweze kuwa wengi na waweze kupata mikopo hii, waweze kuendelea na elimu ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na wakati wako ambapo time ni kidogo na mimi ninapenda nisite hapa, ninakushuru sana na mimi ninaunga mkono yote ambayo niliyokuwa nimeyazungumza. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii nikawa mchangiaji inawezekana pengine kwa jioni ya leo ikawa ndio wa kufungia dimba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza ninataka nimpongeze kwanza Mhe. Waziri, kwanza kwa style yake ya usomaji. Maana yake style ile tokea hapa Barazani sijawahi kuiona, maana yake alikuwa anakaa mpaka kwa style maalum, mheshimiwa tunakupongeza.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu ninataka niungane na hotuba ya Mhe. Waziri kwa kutoa pole ingawa siku aliyosoma hotuba yake hakuwi kutoa pole kwa msiba huu wa mwisho, lakini ninaamini kwa kuwa nia yake ilikuwa ni kutoa pole basi ninaamini atamujuisho vile vile na pengine

atakapokuja kutoa majumuisho ataunganisha kutoa pole zake na kwa msiba mzito ambao uliotukuta ni juzi tu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka niseme katika mtu ambaye anaendelea kupata machungu katika misiba hii ya ajali za meli mheshimiwa mimi ni mmoja wao. Ajali ya mwanzo nilipoteza watu karibu 98 ambao walitokezea au familia zao zipo ndani ya jimbo langu na katika msiba huu tayari nina familia karibu 6 ambazo zimeathirika na kwa bahati mbaya mtu mmoja ni mtu wangu wa karibu sana; mwenyewe alikuwa ni mwenyekiti wangu wa kamati ya maendeleo ya Jimbo la Kwamtipura, Mzee Hemed mpaka sasa hivi sijamuona, ninasikitika sana na kwa kweli nina uchungu mkubwa sana.

Maendeleo ya Jimbo la Kwamtipura Mzee Hemed sijui nimwite ni marehemu au sijui nimwite vipi, kwa sababu mpaka sasa hivi hatujamuona. Tumejenga skuli ya Kwamtipura, chekechea, tumejenga tena hospitali ya Kwamtipura, tumeweka mradi wa maji, Mzee Hemed alikuwa ni mwenyekiti wangu wa kamati ya maendeleo, alikuwa mstari wa mbele katika maendeleo katika jimbo langu. Kwa bahati mbaya leo simjui hali yake ipo vipi, simjui yupo wapi. Kwa kweli nina masikitiko makubwa sana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, sote tunamuamini Mwenyezi Mungu na tunaamini kuwa Mwenyezi Mungu yupo na mitihani ipo. Lakini Mwenyezi Mungu huyu huyu sisi binadamu ametupa akili na maarifa.

Mtume wetu Muhamad (SAW) alipopewa Utume, kitu cha mwanzo aliambiwa vipi “Iqra”, soma kwa sababu Mwenyezi Mungu hakutaka watu wajinga. Alitaka watu wake walimwengu wake wawe ni watu wamesoma na wawe na taaluma.

Mhe. Mwenyekiti, ukishasoma baadae unafika pahala mpaka unakuwa kiongozi. Unapewa fursa uongoze na wenzako. Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya kazi yetu hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi kutunga sheria za nchi, lakini vile vile kuhakikisha sisi Baraza la Wawakilishi tunaisimamia serikali katika kutekeleza sheria zile. (Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kweli Mwenyezi Mungu yupo na yeye ndiye anayetulete mitihani. Lakini tujiulize sheria zetu tunazifuata.

Mhe. Mwenyekiti, narejea tena siku moja serikali yetu tufanye sherehe ya kuchoma sheria zetu zote tulizozitunga kwa sababu hazina maana. Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa hatuji na jembe siku zote nasema, wala panga wala shoka, tunakuja na suti na tai na wengine kofia na makoti kwa ajili ya kuja kutunga sheria. Wenzetu wanalima mikono imeota suguru kwa kulima

wanavuna walichopanda. Sasa na sisi kwa kuwa tunatunga sheria nzuri lakini tunashindwa kuzisimamia Mheshimiwa tutaendelea kuua watu siku zote halafu baadae tutamsingizia Mwenyezi Mungu. Wakati umefika Mhe. Mwenyekiti, serikali lazima iwajibike, hatuwezi kupoteza watu wetu siku zote watu wanakufa kama kuku hata habari hatuna. Mhe. Mwenyekiti, mimi sipendi sana kuona viongozi wanakwenda kutoa mkono wa pole watu wanalia na nini, tunataka taifa.

Leo kitu ninachosikitika kwamba tunapitisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuna wanafunzi wetu walikuwa wanatoka vyuoni tumepata taarifa, wanafunzi karibu 14 tunaambiwa walikuwemo katika meli wako wapi. Serikali pengine wamepata mikopo ya elimu ya juu vijana hawapo, hatuwezi kustahamili Mhe. Mwenyekiti, lazima serikali ifanye maamuzi magumu.

Mhe. Mwenyekiti, hayo yote nayazungumza kwa sababu nina uchungu, na kwa sababu mmoja aliyesaidia maendeleo ya Jimbo la Kwamtipura nimempoteza na sijui kama nitampata tena.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache sasa naomba niingie katika hoja. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme asubuhi sikukaa humu ndani, kwa hivyo inawezekana pengine nikarejea baadhi ya mambo, lakini nilikuwa naomba kuna baadhi ya vifungu hivi nadhani tumeshatoa agizo na tunaomba agizo hili Mhe. Mwenyekiti ulisimamie. Tumetoa agizo kwamba katika zile wizara zote ambazo kuna vile vifungu tulivyokuwa na mashaka navyo, basi Idara yetu ya Utafiti yaani Wizara mafungu yale wayalete Bajeti ya Matumizi ya mwaka uliopita, na mwaka huu ili Idara ya Utafiti iweze kuwafanyia uchanganuzi kabla ya bajeti ya Wizara ya Fedha. Kwa sababu itakapofika bajeti ya Wizara ya Fedha vifungu hivi vyote tunavikusanya tunampa mwenyewe Waziri wa Fedha atafute kapu ya kuvitia tuangalie wapi tunaweza tukenda tukajazia nyama.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejaribu ku-*quote* tu, baadhi ya vifungu naamini pengine wenzangu watakuwa wamevitaja kuna kifungu 272100 hiki vile vile nitahitaji maelezo, kuna kifungu cha 220200 cha kawaida hicho lakini nitahitaji maelezo, kifungu 22015 pia nitaomba maelezo. Kwa sababu kwa kuwa vifungu hivi vimo katika vitabu sina haja ya kueleza vifungu vya nini, lakini vifungu hivyo nitahitaji maelezo kwa sababu bado yale maelezo yake yanakuwa hayatutoshelezi.

Haya Mhe. Mwenyekiti, sio kwa wizara hii tu, lakini hata katika hizo wizara nyengine tulijaribu kuangalia vifungu hivyo tukaona kwa mwaka huu vimewekwa katika mtindo ambao sisi hatuufurahii sana.

Mhe. Mwenyekiti, baadae nije katika Elimu ya Juu. Mhe. Mwenyekiti, nataka niende haraka haraka kwa sababu ya muda najua siku hizi Mwenyekiti umekuwa mkali, nataka niende Elimu ya Juu. Mhe. Mwenyekiti, bado mimi nina deni kwa Mhe. Waziri, deni langu naona bado katika kitabu chake hiki sikupata jawabu. Niliuliza katika kikao kilichopita suala zima la fedha zilizotoka za elimu ya juu lakini bado mpaka leo.Tumeangalia katika bajeti hapa tumeambiwa karibu shilingi bilioni nne ndio ambazo wamezitoa, lakini kuna fedha nyengine karibuni shilingi bilioni nne hizi hazionekani. Hizi ni fedha za walipa kodi na tulikuwa tunahitaji maelezo ya kutosha.

Mimi siku hiyo niliomba tuletewe orodha ya wanafunzi wale waliopewa ile mikopo ili kuweza kuangalia na tukasema kuwa sisi tunataka tuwasaidie. Wazanzibari sisi tunajuana, ingawa majina yetu yanafanana lakini naamini tukiletewa orodha tunaweza tukawatafuta watu hawa. Kwa sababu wengine wanafanya kazi ndani ya serikali, wengine wamekimbia wanafanya kazi Tanzania Bara na sehemu nyengine, lakini Zanzibar sisi tunajuana tunaamini fedha hizi zinaweza zikarudi zikaweza kusaidia na zikamsaidia Mhe. Waziri katika kutunisha Mfuko wake wa Elimu ya Juu.

Mhe. Mwenyekiti, nilifanya utafiti wa haraka haraka nikagundua kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo kidogo nadhani ndio yaliyokuwa yanaleta utata katika hii Elimu ya Juu. Kulikuwa kuna mwanafunzi anaitwa Juma Yussuf Khamis yeye huyu alisoma Shahada ya pili Chuo cha *Islamic Institute of Uganda* itakuwa kwa sababu wanaita *STU*, Uganda. Huyu alisoma kwa muda wa miaka miwili malipo yake yalikuwa ni shilingi milioni kumi.

Lakini kuna mwanafunzi mwengine ambaye alisoma chuo hicho hicho na katika shahada hiyo hiyo anaitwa Ali Mohammed Haji yeye alilipa shilingi milioni tatu na laki tatu kwa miaka miwli hiyo hiyo. Sasa chuo hicho hicho, elimu hiyo hiyo lakini mmoja shilingi milioni kumi na mmoja shilingi milioni tatu inaonesha haya ndio yaliyokuwa yanasababisha pengie upotevu wa hizo fedha. Lakini vile vile kuna mwengine akiitwa Ali Khamis Shehe, yeye alisoma kwa muda wa miaka miwili na alilipiwa shilingi milioni nne. Sasa ndio maana tukasema kwamba katika kozi hiyo hiyo, chuo hicho hicho kwa nini na miaka hiyo hiyo ikawa malipo yao yamekuwa tofauti tofauti, pengine hii itaweza kumsaidia Mhe. Waziri kuweza kujua hasa upotevu wa fedha ulikwenda vipi.

Lakini vile vile kuna mwengine anaitwa Amiri Ali Mataka yeye alisoma miaka miwili shahada ya pili ya elimu. Huyu yeye alikopeshwa shilingi milioni tano, lakini kuna Maryam Khamis Ramadhan yeye shahada ya pili vile vile ya elimu alilipiwa shilingi milioni tisa. Sasa ndio maana tukasema kwa nini mbona hii elimu kozi ni ile ile na chuo ni kile kile ikawa malipo

yanakuwa tofauti. Pengine labda hizo ndizo zilizosababisha kwamba tukahisi zimepotea lakini labda zimetolewa katika njia ambayo sio sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna wengine kama Ndugu Suleiman S .Mohamed yeye amesomea shahada ya kwanza *engineering*, kitu cha kushangaza huyu unaambiwa alisoma mwaka 2001 mpaka mwaka 2008 lakini alilipiwa shilingi milioni moja klaki ane. Lakini kuna Amour Rajab *Civil Engineering* mwaka 2007/2009 yeye alilipwa shiligi milioni nne. Kuna mwengine huyu Moahd Hamd Haji uhandisi mwaka 2009/2011 yeye alilipiwa shilingi milioni moja na elfu ishirini. Sasa Mhe. Waziri baadae labda baadae akitaka hizi takwimu kwa usahihi tunaweza tukawasiliana kwa sababu najua kwa hapa nitamzonga kidogo, hawa walisoma *DIT*. Kwa hivyo, tunaweza tukamsaidia vile vile kwa sababu haja yetu sio kukomoana, haja yetu ni kusaidiana ili fedha ziweze kutumika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulisema kwamba Mhe. Waziri katika hotuba yake alieleza kwamba watatoa elimu au mkopo kwa wanafunzi ya elimu ya juu katika wale waliochukua shahada ya uzamili tu, lakini katika ngazi ya *PhD* hamna. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tunahitaji kujenga taifa ambalo lina wasomi na tutengeneze wasomi wetu wenyewe ili na wao watengeneze wasomi, lakini tunapowazuia hawa wanafunzi ambao wanachukua *PhD* na ukiangalia Zanzibar tuna uchache sana wa wanafunzi ambao wenye shahada za *PhD*, na ukiangalia hata yanapokuja Mashirika ya Kimataifa haya wanahitaji ma-*consultant* na moja katika sifa wanazozitaka wanataka watu wenye *masters.*

Mimi unajua *degree* yangu ya *Form IV* niliichukulia Kwamtipura, lakini nadhani hawa wenye *masters* hawa nadhani wanasomeshwa na watu wenye *PhD*. Sasa hawa vijana wapo wanataka kusoma na uwezo wao unajua watoto wetu wa kinyonge wazee wao uwezo hawana, na kwa kuwa wako wachache kwa nini tushindwe kuwasomesha, kwa nini tushindwe kutoa huu mkopo ili hawa vijana waweze kuwa walimu na badae waje wawasomeshe hawa wengine.

Sasa Mhe. Waziri nilikuwa naomba sana sana, kwa kuwa hawa wanafunzi wanaotaka kusoma *PhD* sio wengi basi nadhani hizi fedha mnazozitenga mwaka huu na kwa bahati nzuri umetenga fedha nyingi kidogo mwaka huu, tunakushukuru sana, basi fedha hizi na hawa vijana wetu wachache wanaotaka kuchukua *PhD* tuwakopeshe ili na wao waje wawe walimu waweze kuja kuwasomesha vijana wetu vile vile.

Mhe. Waziri nakujua wewe ni msikivu, naamini na Naibu waziri wako mahiri sana, msikivu, naamini kwa hili mtatukubalia ili vijana wetu hawa waweze kupata mkopo wa elimu ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mimi nina masikitiko, nina masikitiko kuna vijana miongoni mwa hawa waliopatiwa hivyo vyeti feki mimi niliwaona kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nilitokwa na machozi. Kwa sababu nilikuwa najiuliza jamani hawa wenzetu hii mikwaruzo iliyokuwepo hapa Barazani hawaioni, hawawaonei huruma hawa Mawaziri. Kwa sababu tatizo wale wanaofanya utumbo ule humu hawaingii tungeliwang'ong'ona wao hapa, lakini sasa Mhe. Waziri wewe ndiye kitambaa, ukishindwa kuwasimamia hawa itabidi sasa uwajibike wewe, kwa sababu sisi tunayemuuliza maswali kwa mujibu wa katiba ni wewe. Sasa mimi naomba hawa watendaji wako waliochukua pesa za watu shilingi laki tatu tatu wazicheuke, fedha hizi wazicheuke, watoto wetu wa kinyonge hawana fedha wanataka kwenda kusoma leo mtu mkamtoleshe shilingi laki tatu fedha hizo mnyonge atazipata wapi Mhe. Mwenyekiti mshahara wenyewe shilingi laki moja na nusu mbali hiyo mikato. Huko madukani wanadaiwa kila kitu.

Halafu kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti, kuna hii ajira ya ualimu, na nafikiri hii ndio iliyowasababisha watu wawatoze watu shilingi laki tatu tatu. Unajua sasa hivi ajira ngumu lakini mtu tunataka apatiwe ajira hasa ya ualimu awe na sifa, leo mtu kapata *division zero* unakwenda kumpa cheti aonekane ana *diploma* pengine ya sayansi au *degree* Mheshimiwa tunatengeneza au tunabomoa taifa. Mimi nadhani hapa tunaomba tuone makali yako sasa hivi katika Wizara ya Elimu, chukua rungu na sisi kwa sababu sisi ndio tunaolinoa wewe uende ukakate tu huko katika wizara yako. Sasa Mhe. Waziri naomba tukija hapa utwambie kwamba walimu hawa nimeshawaita na tayari kuna hatua moja, mbili, tatu tutaanza kuzichukua, vyenginevyo Mhe. Waziri hii bajeti itakuwa na mtetemeko wa hali ya juu sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nina ombi jengine, sasa hivi kuna walimu ambao tunashukuru wizara imeamua kuwasomesha, wameamua wao wenyewe kujiendeleza sasa hivi wanasomea diploma ya sayansi wapo Nkrumah pale. Lakini kutokana na hali katika kuingia kwenye sifa ya kupata mikopo ya elimu ya juu bado wao hawa *qualify*, lakini kwa kuwa hawa ni walimu wako mimi nilikuwa naomba, kwa sababu nimepata barua hii ambayo wamewekewa tangazo pale chuoni, wanasema malipo ya mitihani ya *semester* ya pili mwaka 2011/2012, tunajua walimu wao wako juu pale wanatusikia kwa hivyo hii tulikuwa tunaomba kidogo afueni.

Sasa kitu ambacho tunakiomba sio wasamehewe lakini hawa wameshatishiwa amani kwamba hawatofanya mtihani mpaka wahakikishe kwamba wamelipa,

kitu tunachokuomba Mhe. Waziri hawa wanafunzi wetu na ni wanafunzi walimu, tena katika kada ambayo ni adimu kidogo ya sayansi tunawaombea na kwa kuwa hawa ni walimu sio *fresh from school* basi waruhusiwe kufanya mitihani, lakini vyeti wasipewe hata kama matokeo, lakini matokeo watayaona kwa sababu mambo ya siku hizi mambo ya sayansi na teknolojia, lakini vyeti vyao wasipewe mpaka waweze kulipa na wako tayari hata kusaini katika mishahara yao hizi fedha moja kwa moja ziende huko.

Mhe. Mwenyekiti, hawa ndio wa kutengeneza kwa sababu hawa tayari wamesoma *certificate* na *diploma*, tayari ni walimu ambao walikuwa wanasomesha, ni walimu wa sayansi kuliko kwenda kuwachukua wale ambao wamepata *division zero* halafu ukenda ukawapa vyeti feki wakenda wakasomesha. Mimi nafikiri tuwatengeneze hawa ambao wameamua kuweka kambi kwa kusoma ili waweze kufaulu na vijana wetu hawa wasivunjike moyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi walimu hawa wameweka kambi na kwa bahati hii kambi moja imo ndani ya Jimbo langu la Kwamtipura. Sasa siku hiyo nakwenda wanalia nawauliza vipi, tushatishiwa amani, sasa Mheshimiwa mshahara wenyewe unaujua ndio tunaopewa hapa nikisema niwalipie wale hiyo ada ya mitihani mimi nitakuwa sina kitu na Ramadhani hii hali mbaya. Sasa kwa kuwa wao wenyewe wameamua watajilipia wao wenyewe Mhe. Waziri naamini ni mtu msikivu utaweza kutusikiliza kilio chetu cha hawa vijana wetu.

Lakini vile vile kuna wanafunzi wengine ambao hawa nadhani wanafanya mitihani yao mwezi wa Oktoba, vile vile *degree* nafikiri katika masuala ya sayansi. Hawa Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna hizi nafasi za ajira wao walipotaka kwenda kuomba wameambiwa wasubiri mpaka wamalize mitihani na mitihani inamaliza mwezi wa Oktoba, ajira nafikiri tukimaliza bajeti itaanza kutolewa kwa walimu, sasa kwa kuwa kuna watu ambao walikuwa weshataka kutengenezewa vyeti feki kwa kuwa kuna vijana wetu hawa wamemaliza *Form VI* tayari wameshakwenda kuchukua na *degree* ya sayansi, na wanaamini wenyewe wanaweza wakafaulu vizuri tungelijaribu kuangalia uwezekano wa ku-*by time* ili na hawa tukaangalia wale waliofaulu basi tukawaingiza katika hii kada ya elimu.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi wenzetu Bara wanatuchezea kiguru cheche, wakisikia wanafunzi wanakaribia kumaliza tuseme *diploma* au *degree* katika masuala ya sayansi tayari wanaanza kuleta *application* bwana wee mimi nakutaka uje unisomeshee huku. Mhe. Mwenyekiti, wengine katika hawa baada ya kuona kwamba hapa ajira inawezekana kwamba hata wakishamaliza wao itakuwa hawaipati, tayari wameshafanya *application* ya

kuomba ajira kule Bara. Mhe. Waziri sisi tutakuwa tunasomesha lakini baadae matunda wanakwenda kutumia wenzetu kule. Kwa hivyo, hili nilikuwa naomba sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda umebakia mchache malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namalizia katika suala zima la miradi ya *tender* hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Wizara hii ina miradi mikubwa mingi lakini tunaomba, sasa hivi kuna malalamiko ya wakandarasi na kwa kuwa wanatulalamikia sisi ndio wasemaji wao basi tunasema hizi *tender* safari hii zinapotolewa kuanzia sasa hivi zitoke *open tender*, halafu vile vile baada ya matokeo yule aliyeshinda utaratibu wa *transparency* inakuwa mpaka yanatolewa matangazo na vile vigezo vyote vinabandikwa pale, wale wakandarasi wote ambao waliomba wanakuja kuona ni vitu gani vilivyomfanya yule wa mwanzo aka-*qualify*.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nataka niipongeze sana Wizara ya Elimu kwa kuweza kunijengea Skuli ya Sekondari ya Kwamtipura, skuli ya kifahari, skuli ya kisasa kabisa. Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba sana tena Vijana wetu Wazanzibari watusikie. Wenzetu mwaka 2005 kabla ya uchaguzi ilikuwa, Mhe. Mrisho Jakaya Kikwete katika jitihada zake za kuhangaika kutafuta misaada nje Waziri wa Elimu wa Jamhuri ya Muungao alikwenda kutafuta misaada akaambiwa atupatie shilingi bilioni kumi sisi Zanzibar, lakini Mhe. Mwenyekiti, baada ya Waziri wa Elimu wakati huo swahibu wangu leo hayupo Mhe. Haroun Ali Suleiman baada ya kuona fedha zile ni chache alifanya jitihada zake yeye mwenyewe binafsi akajenga hoja kwa wenzetu wa Marekani akaweza kufanikiwa kupata US$ 45 bilioni badala ya US$ bilioni kumi. Sasa mimi nadhani matunda yake ndio hizi skuli ambazo tunazozijenga.

Leo nimeshangaa Mhe. Fatma Mbarouk Said anasema ile skuli iitwe Skuli ya Kilimahewa, ile skuli haiitwi Skuli ya Kilimahewa, ile ni Skuli ya Kwamtipura na itaendelea kuitwa Skuli ya Kwamtipura.

Tunashukuru sana Mhe. Waziri wa Elimu jitihada hizo alizozianzisha mwenzenu na nyinyi mziendeleze kwa mafanikio ya hapa Zanzibar. Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja, lakini naunga mkono hoja ikiwa masuala ya fedha za mikopo ya elimu ya juu na zile nyengine za vifungu baada ya kupata ufafanuzi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe na nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa utulivu wenu. Kuna tangazo

hapa kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe wote, mnaombwa kesho mtakapokuja kwenye semina Wajumbe wote waje ambao wana *account* ya kawaida ya *PBZ* wanaombwa waje na picha moja pamoja na kopi ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi kwa ajili ya kujaza fomu za ku-*up date account* zao. Kwa hivyo, Waheshimiwa nafikiri mmefahamu vizuri sana nini kimekusudiwa.

Waheshimiwa Wajumbe takriban Wajumbe wote ambao wameomba kuchangia wamepata fursa, ingawa kuna Wajumbe wengine wawili hawajapata fursa hiyo ya kuchangia. Kwa hivyo, nawaomba Wajumbe hao ambao ni Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad mchango wao waupeleke kwa maandishi. Tunatarajia tukijaaliwa siku ya Jumatatu, tarehe 23/07/2012 tutafanya majumuisho ya Wizara hii. Waheshimiwa Wajumbe mpaka hapa tumemaliza kwa leo na ninaomba kuakhirisha mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 23/07/2012 ahsanteni.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 23/07/2012 saa 3:00 asubuhi)